# Nipashe

Jumatano Desemba 11, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580098

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper







## Ukosefu wa madarasa wasababisha wanafunzi kwenda shuleni Februari

UK. 3

# Mfungwa agoma kutoka gerezani

**Ni** aliyepata msamaha wa JPM, mwingine atoka akiwa na mtoto, Ma-RC wasimamia mchakato... *Uk. 2*



Baadhi ya wafungwa wa kike katika Gereza Kuu la Butimba mkoani Mwanza walionufaika na msamaha wa Rais wakitoka gerezani kwenda kuungana na familia zao. Wafungwa hao walimshukuru Rais John Magufuli kwa msamaha huo. **PICHA: LUCAS MBOJE**

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

**SABABU KUPAISHA MFUMUKO WA BEI**

BIDHAA za vyakula na zisizo za vyakula vimetajwa kuchangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwa mwezi unaoishia Novemba 2019 kwa asilimia 3.8.

**UKURASA WA 5**

**MAWAKALA WA VYAMA RUKSA UBORESHAJI DAFTARI**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imesema mawakala wa vyama vya siasa wanaruhusiwa kuwapo katika vituo vya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ili kuwapo uwazi katika uandikishaji wapigakura.

## MIKOPO ELIMU YA JUU KAA LA MOTO

UK.3

## Balozi Marekani amwaga chozi kumlilia Mufuruki

UK. 2

**MICHEZO** YANGA: TUMEELEMEWA MADENI, SADNEY ONDOKA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# Mfungwa agoma kutoka gerezani

**Na Waandishi Wetu**

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, Merard Abraham, ambaye ni miongoni mwa wafungwa waliopewa msamaha wa rais na kutakiwa kutoka gerezani mkoani Mbeya, amegoma kutoka kwa madai kuwa hana mahali pa kwenda kuishi.

Mfungwa huyo ameiomba serikali kuachana na uamuzi wa kumwachia huru na badala yake wamuhamishe kutoka katika Gereza la Ruanda, lililopo jijini Mbeya na kwenda Gereza la Ukonga lililopo jijini Dar es Salaam.

Alitoa kituko hicho jana muda mfupi baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuzungumza nao na kuwaasa waende kuishi kwa amani na kwa kufuata maadili mema wanaporejea nyumbani.

Mfungwa huyo ambaye alionekana kama kuwa na matatizo ya akili, alionyesha msisitizo wa kutotaka kurudi nyumbani na katika tukio ambalo halikutarajiwa aliokota jiwe na kujibamiza usoni hali ambayo ilimsababishia majeraha na hivyo kukimbizwa katika zahanati ya gereza hilo.

Mwandishi wa gazeti hili ambaye alikuwa miongoni mwa waandishi wa habari walioruhusiwa na kuzungumza na wafungwa hao waliosamehewa, alishuhudia mfungwa huyo akisisitiza msimamo wake wa kutotaka kwenda nyumbani baada ya yeye na wafungwa wenzake kutolewa nje na kutakiwa kupewa nauli ya kuwafikishwa makwao.

Lakini katika hali ambayo alionyesha kutokubaliana nayo, ndipo alipochukua uamuzi wa kujijeruhi na jiwe hilo.

Kabla ya hatua yake hiyo, alisema alikuwa anakabiliwa na kesi ya ubakaji na kuhukumiwa kwenda jela miaka 30, mwaka 2000 na kwa sasa alikuwa tayari ameshatumikia miaka 19 gerezani.

"Kwetu ni Busokelo (Rungwe, Mbeya), lakini mimi kwa sasa sitaki kutoka gerezani, nataka nipelekwe Gereza la Ukonga, sina pa kwenda na naomba nirudishwe ndani niendelee na maisha yangu," alisema Abrahamu.

Hata hivyo, wakati mfungwa huyo akichukua hatua hiyo,

INAENDELEA UK. 26




Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Fizikia ya Uingereza, Rachel Youngman, akizungumza na washiriki wa mradi wa Future STEM Leaders jijini Dar es Salaam mwishoni wiki. Taasisi hiyo iliandaa tukio hilo kwa ajili ya kuwapa fursa wanafunzi wa shule za sekondari kuandaa mradi wowote ambao unatoa suluhisho la changamoto zinazoizunguka jamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Balozi Marekani amwaga chozi akimuaga Mufuruki

**Na Maulid Mmbaga**

KAIMU Balozi wa Marekani nchini, Dk. Inmi Patterson, jana alijikuta akimwagaza chozi alipopewa wasaa wa kutoa salamu za pole kwa familia ya mfanyabiashara maarufu Ali Mufuruki.

"Ali (Mufuruki) alikuwa chanzo cha hekima na ushauri kwangu wakati nikijaribu kuelewa na kufanya kazi kwenye mazingira ya kisiasa yanayobadilika kwa haraka Tanzania," Balozi huyo alitamka kwa huzuni, akimwelezea kuwa alikuwa mwenye nidhamu ya kazi, pia mapenzi mema kwa nchi yake.

Shughuli za kuaga mwili wake zilifanyika jana jijini Dar es Salaam zikiongozwa na Rais mstaafu Benjamin Mkapa. Pia alikuwapo Waziri Mkuu mstaafu, Joseph Warioba na viongozi mbalimbali wa serikali, wafanyabiashara na wawakilishi wa kidiplomasia kutoka nje ya nchi.

Mufuruki ambaye alifariki dunia Jumamosi iliyopita Afrika Kusini kwa maradhi ya kifua alizikwa katika makaburi ya Kisutu.

Mfanyabiashara huyo licha ya kushika nyadhifa mbalimbali ndani na nje ya nchi, alikuwa mmiliki na Mwenyekiti Mtendaji wa Infotech Investments Group Limited iliyokuwa na kampuni mbalimbali kama vile W-Stores Limited (Woolworth), Infotech Computers Limited na Infotech Place Limited.

Akizungumza mbele ya hadhira ya waombolezaji, balozi huyo alianza kwa kutaja majina ya mke na watoto wa Mufuruki, huku sauti yake ikizidi kufifia na mwisho alishindwa kutamka, akaishia kutokwa machozi akigugumia.

"Nilipokutana naye kwa mara ya kwanza, alinipa nakala ya kitabu chake cha maono. Kitabu hicho kilibeba matumaini yake yote kwa Tanzania na kwenu ninyi Watanzania.

"Inaonyesha jinsi alivyo mkarimu na mwenye moyo mwema. Alikuwa zaidi ya hapo, alizaliwa katika familia maskini, alikuwa 'kitu' ambacho sisi Wamarekani tunakiheshimu.

**ALIJITENGENEZA**

"Alizaliwa maskini na wazazi wake hawakuwa wamesoma sana, lakini alijisomesha, alijifunza kukubaliana na hali ngumu na alifanikiwa.

"Nitamkumbuka sana, Tanzania itamkumbuka. Ali nitakumbuka, Tanzania itakukumbuka," alitamka.

Katika kundi la mamia waliokuwapo katika ibada ya kumuaga, pia walikuwapo Waziri Angellah Kairuki, Balozi Joseph Sokoine, Dk. Martiki Mani (Kenya) na Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye.

Mafuruki alikuwa mhandisi kitaalamu na mzoefu katika uwekezaji na usimamizi wa biashara. Pia aliwahi kuziongoza kampuni mbalimbali zikiwamo Vodacom, Chai Bora, Netherland's AMSCO na Legacy Capital Company.

Mufuruki ni mwanzilishi wa kikundi cha viongozi wa kampuni kijulikanacho kama CEO Roundtable of Tanzania (CEOrt) na kikundi cha viongozi wa Afrika (Africa Leadership Initiative -ALI) Afrika Mashariki.

Mufuruki pia alikuwa mshiriki na mtoaji ushauri katika masuala ya mazingira na biashara katika

INAENDELEA UK. 8

## Mwanamke aelezea maisha yake akiwa gerezani na mwanawe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKAZI wa Chamwino mkoani Dodoma, Martha Mathew, ambaye alikuwa akitumikia kifungo cha mwaka mmoja katika Gereza la Isanga mkoani hapa, amefunguka maisha aliyokuwa akiyaishi yeye na mwanawe ndani ya gereza hilo.

Mfungwa huyo alitoka jana gerezani kwa msamaha wa Rais John Magufuli alioutoa juzi kwa wafungwa 5,533 ikiwa sehemu ya Sherehe za Miaka 58 ya Uhuru wa Tanzania Bara, ambazo kitaifa zilifanyika jijini Mwanza.

Akizungumza jana baada ya kutoka gerezani, Mathew alisema alihukumiwa kifungo cha mwaka mmoja kutokana na kosa la kumpeleka mtoto kufanya kazi za ndani bila ridhaa ya mzazi wake.

"Kwa kweli maisha ya gerezani si mazuri kutokana na msongamano uliopo. Unaweza kusababisha kupata magonjwa mbalimbali. Tunaomba Rais kuliangalia hilo ili kusaidia kuboresha mazingira ndani ya magereza," alisema.

Mwanamke huyo alihukumiwa Julai, mwaka jana akiwa na mtoto wake mwenye umri wa mwaka mmoja na nusu ambaye aliingia naye gerezani.

"Maisha kule gerezani si mazuri kwa sababu mtoto na yeye anakuwa hayuko huru kama anavyokuwa uraini japokuwa kuna sehemu ya kucheza wakati mie nikifanya kazi za gerezani.

"Nilipoingia gerezani nilikuwa na mtoto na ikifika muda wa kufagia au kufanya kazi zingine, yeye namweka sehemu ya ukumbi anacheza na watoto wengine kama wanakuwapo na wazazi wao ambao wanatumikia kifungo," alibainisha.

Haya hivyo, alisema alikuwa anakula vizuri, lakini shida ipo zaidi katika msongamano wa sehemu ya kulala.

**MAZINGIRA YAKOJE?**

Naye mkazi wa Ibaga mkoani Singida, Ramadhan Abdallah, ambaye alihukumia kifungo cha miaka 30 jela kwa kosa la ubakaji mwaka 2000, alisema kifungo chake amekitumikia katika mazingira magumu kutokana na mke wake ambaye ndiye aliyekuwa akienda mara kwa mara kumjulia hali kufariki dunia kwa ajali ya gari.

Ramadhan ambaye alikuwa mfanyabiashara wa madini, alisema anakwenda mkoani Singida lakini hajui ni maisha gani anakwenda kuanza kuyaishi.

"Unajua awali nilikuwa nafan

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Rais mstaafu Benjamin Mkapa, akitoa heshima za mwisho mbele ya jeneza lililobeba mwili wa aliyekuwa mfanyabiashara maarufu, Ali Mufuruki katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam jana. Mufuruki alizikwa katika makaburi ya Kisutu.
**PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ukosefu madarasa wachelewesha wanafunzi kujiunga elimu sekondari

**Na Waandishi Wetu**

WANAFUNZI 5,970 waliofaulu na kukosa nafasi ya kuchaguliwa kuendelea na elimu ya sekondari mkoani Dar es Salaam, sasa wataanza masomo yao Februari mwaka 2020.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo. Aliwaagiza wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi, kuhakikisha ifikapo Februari 29, mwakani, wanakamilisha ujenzi wa madarasa.

Alitoa maagizo hayo ili wanafunzi waliokosa nafasi awamu ya kwanza, wajiunge na kidato cha kwanza na kuanza masomo ifikapo Machi 3, mwakani.

Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam Hamisi Lissu, wakati alipozungumza jana na Nipashe ofisini kwake alisema juhudi za dhati zinafanywa kufanikisha hilo.

Alisema mpango mkakati umewekwa ili kuhakikisha jambo hilo linafanikiwa, hivyo kutowachelewesha kwa muda mrefu wanafunzi hao kuanza masomo yao.

"Mpango wa 'double shift' tumeshindwa kuufanya mwaka huu kwa kuwa bajeti imebana, lakini tutahakikisha watoto wetu hao wanaanza masomo yao mwishoni mwa Februari mwakani," alisema Lissu.

Lissu alisema Wilaya ya Temeke ina idadi ndogo ya sekondari, wakati ina wengi waliokosa nafasi, hata hivyo hakuitaja kwa kuwa aliitwa kwenye kikao.

Mkoa huo uliongoza matokeo ya mtihani wa kuhitimu Darasa la Saba Baraza la Mitihani Tanzania (Necta) kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia 2017 na 2019.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Lusubilo Mwakabibi, hakuwa tayari kuelezea kuhusu changamoto hiyo, akidai kuwa REO ndiye anapaswa kuizungumzia.

Kwa upande wake Naibu Meya wa Manispaa ya Temeke, Juma Mkenga, alisema suala la wanafunzi kufaulu na kukosa shule ni changamoto ambayo anaamini katika kikao chao cha Baraza la Madiwani (leo), watapata taarifa ya nini kinakusudiwa kufanywa ili kuikabili.

Jafo alipozungumza mwishoni mwa wiki iliyopita kuhusu wanafunzi waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza kwa shule za serikali alisema, wanafunzi 701,038 sawa na asilimia 92.27 ya waliofaulu ndiyo waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwezi Januari 2020.

Alisema kati yao wavulana ni 335,513 sawa na asilimia 47.86 huku wasichana ni 365,525 sawa na asilimia 52.14.

Kadhalika alisema wanafunzi waliochaguliwa, 3,145 sawa na asilimia 0.41 ya waliofaulu wamechaguliwa kujiunga kwenye shule za bweni, wanafunzi 970 watajiunga na shule za ufaulu wa alama za juu, wengine 1,095 watajiunga katika shule za ufundi na wanafunzi 1,080 wamechaguliwa kwenda shule za bweni.

**MAELFU WAKOSA NAFASI**

Alisema wanafunzi 58,699 sawa na asilimia 7.773 wakiwamo wavulana 28,567 sawa na asilimia 48.53 na wasichana 30,132 sawa na asilimia 51.33 ya waliofaulu, hawakuchaguliwa kwa sababu ya ufinyu wa madarasa.

Pia alitaja mikoa ambayo ina wanafunzi waliokosa fursa hiyo na idadi yao kwenye mabano kuwa ni Arusha (4,739), Dar es Salaam (5,808), Manyara (728), Mara (9,493), Iringa (3,480), Songwe (4,684 ), Kigoma (12,092), Lindi (1,665), Tanga (3,044), Mbeya (2,716), Pwani (2,918), Rukwa (686) na Simiyu (6,616),

**UHABA MADARASA LINDI**

KATIBU Tawala Mkoa wa Lindi, Rehema Madenge, amewapa wiki mbili wakurugenzi wa halmashauri nne kujenga vyumba 44 vya madarasa kuwawezesha wanafunzi 1,695 waliokosa nafasi ya kujiunga kidato cha kwanza, wanaanza masomo.

Halmashauri zinazokabiliwa na upungufu huo ni Kilwa, Nachingwea, Ruangwa na Lindi/Mtama.

Madenge alitoa agizo hilo, alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari.

Akitoa takwimu, alisema wanafunzi 18,197 wakiwamo 8,575 wavulana na 9,622 wasichana, walifanya Mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi (PSLE), mwaka huu na 13,916 kati yao wavulana 6,736 na wasichana 7,180 wamefaulu.

INAENDELEA UK. 8

# Mikopo elimu ya juu kaa la moto

**Na Romana Mallya**

MTANDAO wa Wanafunzi Tanzania (TSNP) umesema kama serikali haitaingilia kati kuhusu mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu, mamia watashindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa haki hiyo.

Katibu wa TSNP, Joseph Malekela, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia kuhusu changamoto ambazo wanafunzi wanazipitia kwa sasa, huku baadhi wakikosa mikopo na wengine kulipwa kwa kupunjwa.

Akizungumzia rufani za wanafunzi walizokata Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) zilizotoka Jumamosi, Malekela alisema zaidi ya wanafunzi 600 ndiyo wameshinda.

"Katika taarifa ya bodi imeonyesha zaidi ya wanafunzi 600 wameshinda rufani zao za mikopo baada ya kukosa awali, kwa bahati mbaya Bodi ya Mikopo haijasema ni wanafunzi wangapi walikata rufani hizo," alisema.

Malekela alisema wasiwasi walionao kama mtandao ni kwamba wanafunzi wengi waliokata rufani na hawajashinda, watashindwa kuendelea na masomo yao licha ya kuwa na uhitaji wa kupata fedha hizo.

"Tunataka kuwe na uwazi... ni wangapi walikata rufani na kwa nini wachache wamepata, na hao wengine ambao idadi yao hatujaelezwa wamekosa," alisema.

Malekela alisema mtandao unataka kufanyike mapitio ya rufani hizo kwa sababu wapo wanafunzi ambao ni yatima, na wengine wenye mzazi mmoja na wenye ulemavu ambao kwa sasa hawajui hatima yao baada ya mchakato huo kutolewa.

Pia alisema jambo lingine ni kuhusu wanafunzi ambao wanaendelea na masomo na wana sifa ya kupata, lakini baadhi bado fedha zao hawajapata.

"Wanafunzi hawa wapo chuoni na sasa ni zaidi ya mwezi, lakini fedha za chakula, malazi wala ada hazijaletwa, tumefuatilia wanasema mwanafunzi aliyehama mafunzo yake wanasubiri TCU (Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania) iwathibitishe.

INAENDELEA UK. 8


**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la upimaji wa viwanja limekamilika na kuanzia **TAREHE 3/12/2019** viwanja vitaanza kuuzwa kila siku za Jumatatu hadi Ijumaa katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 2 Asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri.

**Viwanja vinavyouzwa ni katika maeneo ya:**

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| NALA (Karibu na Chuo cha IFM na Kituo cha kupaki Malori) | • Makazi 4,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| CHAHWA (Karibu na Ikulu) | • Makazi 3,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| Mahoma Makulu (Nyuma ya Mji wa Serikali) | • Makazi 3,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| KIKOMBO (Karibu na Bandari kavu na Makao Makuu ya Ulinzi ya Taifa) | • Makazi 2,000/=<br>• Makazi na Biashara 3,500/= |
| MTUMBA (Karibu na Mji wa Serikali na Ikulu) | • ZONE I Makazi 8,000/= Makazi na Biashara 8,500/=<br>• ZONE II Makazi 6,000/= Makazi na Biashara 7,500/=<br>• ZONE III Makazi 3,000/= Makazi na Biashara 5,500/= |

**NB: Malipo yote yafanyike ndani ya Siku 90 baada ya kupata hati ya madai.**

***Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba 0714 785513.***

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

215542002




Mratibu wa Vipindi wa EATV, Sophia Proches (kulia), akimkabidhi zawadi Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipakodi wa TRA, Richard Kayombo, baada ya kumaliza mahojiano kwenye kampeni ya 'Kibiashara Zaidi' inayolenga ukuzaji wa sekta ya biashara nchini, ambayo inaendeshwa na kituo hicho. **PICHA: EATV**

# Vyakula, bidhaa zapaisha mfumuko bei

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BIDHAA za vyakula na zisizo za vyakula vimetajwa kuchangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei kwa mwezi unaoishia Novemba 2019 kwa asilimia 3.8.

Bidhaa hizo ni mchele, nyama, unga wa muhogo, mihogo, mafuta ya kupikia, mboga, maharage, mavazi, mkaa, samani, mazulia na huduma ya malazi ya nyumba za wageni.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ruth Minja, alipokuwa akitoa taarifa ya mfumuko wa bei kwa mwaka unaoishia Novemba 2019.

Alisema bei zinaongezeka kutokana na mahitaji ya bidhaa hizo sokoni kuwa makubwa.

"Mahitaji ndio yamesababisha kupanda kwa bei za bidhaa hizi na inawezekana inachangiwa na uhaba wa uzalishaji na usafirishaji," alisema Minja.

Alieleza kuwa mfumuko huo umeongezeka kutoka asilimia 3.6 kwa mwaka ulioishia Oktoba 2019 na kufikia asilimia 3.8 mwaka unaoishia Novemba 2019.

"Hii inamaanisha kuwa, kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia Novemba 2019, imeongezeka ikilinganishwa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia Oktoba 2019," alisema.

Alibainisha baadhi ya bidhaa za vyakula zilizoongezeka bei kwa Novemba 2019 zikilinganishwa na mwezi Novemba 2018, ni pamoja na mchele kwa asilimia 6.6, unga wa muhogo kwa asilimia 7.8, nyama kwa asilimia 2.6, mafuta ya kupikia kwa asilimia 7.2.

Zingine ni maharage kwa asilimia 8.6, mboga kwa asilimia 6 na mihogo kwa asilimia 5.8.

Kadhalika, alisema kwa upande wa bidhaa zisizo za vyakula zilizoongezeka bei ni pamoja na mavazi kwa asilimia 2.7, mkaa kwa asilimia 4.4, samani kwa asilimia 3.1, huduma ya malazi kwenye nyumba za wageni kwa asilimia 5 na mazulia kwa asilimia 6.3.

"Mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia Novemba 2019, umeongezeka hadi asilimia 6.1 kutoka asilimia 5.1 kwa mwaka ulioishia mwezi Oktoba 2019,"alisema.

Kuhusu mfumuko kwa nchi zingine, Mkurugenzi huyo alisema nchini Kenya mfumuko umeongezeka hadi asilimia 5.56 kutoka asilimia 4.95 kwa mwaka ulioishia Oktoba 2019.

"Kwa upande wake Uganda mfumuko umeongezeka hadi asilimia 3 kutoka asilimia 2.5 kwa mwaka ulioishia Oktoba 2019," alisema.

# Raia wa kigeni wakwamisha kesi ya MO

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa Jamhuri katika kesi ya kutekwa Mfanyabiashara Mohammed Dewji maarufu kama Mo, umedai kuwa kesi hiyo haiwezi kuendelea na mshtakiwa mmoja mpaka watakapopatikana wote.

Kesi hiyo inayomkabili dereva wa taksi, Mousa Twaleb na wenzake wanne ambao hawajakamatwa, ilipangwa kutajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Wakili wa utetezi Maufudhu Mbagwa, alidai kuwa mshtakiwa amekaa mahabusu muda mrefu na wengine wako nje ya nchi.

"Tunaiomba mahakama kuendelea kusikiliza kesi dhidi ya mshtakiwa huyu aliyepo mahakamani anateseka kukaa mahabusu," alidai wakili Mbagwa.

Wakili wa Serikali Glory Mwenda, alidai kuwa kesi hiyo haiwezi kuendelea mpaka washtakiwa wengine wakamatwe.

Hakimu Shaidi alisema kesi hiyo itatajwa Desemba 23, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Watuhumiwa wengine ambao upande wa mashtaka inawatafuta ni raia wanne wa Msumbiji na mmoja wa Afrika Kusini wanaodaiwa kumteka mfanyabiashara huyo.

Washtakiwa hao ambao hawajakamatwa ni, Phila Tshabalala, raia wa Afrika Kusini, Henrique Simbine, Daniel Manchice, Issac Tomo na Zacarious Junior, wote raia wa Msumbiji.

Katika kesi hiyo inadaiwa Mei Mosi na Oktoba 10, 2018, katika maeneo ya jiji la Dar es Salaam na Johannesburg Afrika Kusini, kwa makusudi waliendesha genge la uhalifu.

Pia inadaiwa Oktoba 11, mwaka jana maeneo Hoteli ya Colloseum, wilayani Kinondoni Dar es Salaam, Twaleb pamoja na watu wengine ambao hawapo mahakamani, walimteka nyara Mo kwa nia ya kumhifadhi kwa siri na kumuweka maeneo ambayo ni hatari.

Pia inadaiwa Julai 10, mwaka jana maeneo ya Mbezi Beach, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, Twaleb alitakatisha fedha ambazo ni Sh. 8,000,000 wakati akijua ni kosa la kushiriki genge la uhalifu na makosa ya kupanga.

Mo alitekwa nyara Oktoba 11, mwaka jana alfajiri maeneo ya Hoteli ya Colloseum wakati akienda kufanya mazoezi na alipatikana Oktoba 20, mwaka huo huo, eneo la Gymkhana.

**CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)**
(Tanzania Teachers' Union – TTU)

P.O. Box: 3077 DODOMA | Fax: 255 262323452
Cable: WALIMU DODOMA | Telephone: 255 262323451
E-mail: info@ttu.or.tz

**GENERAL PUBLIC**

**RE: NOTICE OF CANCELLATION OF INVITATION FOR PRE QUALIFICATION FOR PROPOSED CONSTRUCTION OF OFFICE BUILDING AT CHATO**

The general public is hereby notified that on 6th day of December, 2019 through Mwananchi and Nipashe Newspapers, TTU published the notice of invitation for pre-qualification for proposed construction of office building at Chato.

Take notice that, the said notice dated **6th day of December, 2019** is cancelled, hence be disregarded.

We regret.

Mwl. Deus G Seif
GENERAL SECRETARY
TANZANIA TEACHERS UNION

GENERAL SECRETARY
TANZANIA TEACHERS' UNION (TTU)
DODOMA - HEADQUATERS

215549902

# Tume yawaonya watumishi umma

**Na Mwandishi Wetu**

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imewataka watumishi wa umma kuzingatia haki za binadamu na msingi ya utawala bora katika utekelezaji wa majukumu yao.

Pia imewahimiza wananchi na watumishi wa umma kuwasilisha malalamiko kwenye Tume, wanapoona haki zao za msingi zimeingiliwa au kuvunjwa na viongozi au watendaji katika utumishi wa umma kwa kutumia madaraka kinyume cha sheria.

Kwa mujibu wa taarifa kuhusu maadhimisho ya siku ya haki za binadamu iliyotolewa jana Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, kaulimbiu ni vijana piganieni haki za binadamu, ikiwa inatambua wajibu na nafasi ya vijana katika kuhakikisha zinaheshimiwa na kufurahiwa na watu wote.

"Kaulimbiu inawahamasisha kuzipigania haki hizo pale zisipopatikana, hivi sasa duniani kote tunashuhudia vijana wakipaza sauti zao wakipigania haki mbalimbali, zikiwamo haki ya usawa, ya kufanya kazi, ya kushiriki katika kufanya uamuzi na nyingine," alisema.

Tume hiyo vile vile, imewakumbusha wananchi hususan vijana kutimiza wajibu wao wa kutii na kuheshimu sheria za nchi na kutumia mifumo na njia sahihi katika kudai haki na kuepuka kutumia na watu wasiolitakia mema taifa.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Maadili katika utumishi wa umma ni nguzo muhimu katika kuimarisha utawala bora na haki za binadamu'. Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, Tanzania inatambua na kuthamini uwezo na mchango wa vijana katika kuleta maendeleo endelevu ya taifa.

"Zipo jitihada mbalimbali za serikali zinazolenga katika masuala ya maendeleo ya vijana nchini; hii ikiwa ni pamoja na kuwapo kwa mifumo, sera, mipango na mikakati inayokidhi mahitaji mbalimbali ya vijana kama vile sera ya taifa ya maendeleo ya vijana mwaka 2007," alisema.

Alieleza changamoto zinazowakumba vijana na kama kufahamika kwa mifumo, mikakati, fursa, upatikanaji na utolewaji wa taarifa kwa vijana, upatikanaji wa mikopo, na uelewa mdogo wa sera ya maendeleo ya vijana.

"Tunaziomba mamlaka husika, serikali na wadau kutoa elimu ya kutosha kuhusu uwapo wa fursa kwa maendeleo ya vijana na wasimamizi kuhakikisha fursa zinatolewa kwa usawa kwa vijana wote bila ubaguzi, jambo litakalosaidia kuepusha vurugu na ukosefu wa amani na utulivu katika taifa," alisema.

"Tume inaendelea kuwahimiza wananchi kuwasilisha malalamiko yao kwa taasisi husika na pale wanapoona wametendewa kinyume na sheria, watakapoona kuna usumbufu au malalamiko yao hayashughulikiwa ipasavyo wasisite kuwasilisha malalamiko kwa kuiandikia tume au kufika ofisini," alisema.

# Mawakala vyama ruksa uboreshaji wa daftari

**Na Renatha Msungu,** DODOMA



TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imesema mawakala wa vyama vya siasa wanaruhusiwa kuwapo katika vituo vya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura ili kuwapo uwazi katika uandikishaji wapigakura.

Hata hivyo, mawakala hawatakiwi kuingilia watendaji wanapotekeleza wajibu wao.

Hayo yalisemwa na Makamu Mwenyekiti wa NEC, Jaji mstaafu Mbarouk Mbarouk, (pichani) wakati akifungua semina ya mafunzo ya uandikishaji yaliyowahusisha mratibu wa uandikishaji wa mkoa, ofisa waandikishaji, maofisa waandikishaji wazaidizi, maofisa uchaguzi na maofisa Tehama wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa.

Mafunzo hayo yamelenga kuwapatia uelewa wa jinsi ya kutumia vifaa kwa ajili ya uboreshaji huo, ili kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo kwa maofisa waandikishaji wasaidizi ngazi ya kata ambao nao watatoa mafunzo kwa waandishi wasaidizi ambao ndio watahusika na uandikishaji wapigakura vituoni. "Kwa vyama ieleweke kwamba wakala hawatakiwi kuwaingilia watendaji wanapotekeleza wajibu wao," alisema Jaji Mbarouk.

Aliwataka kuzingatia sheria, kanuni na maelekezo na miongozo inayotolewa na Tume kwa ajili ya kuendesha zoezi hilo muhimu kwa uandikishaji.

Alifafanua kuwa Mkoa wa Dodoma imedhamiria kuhakikisha uandikishaji wapigakura unafanyika kwa ufanisi mkubwa, na kuwataka kuwajibika na kuwa makini wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Naye Mkurugenzi wa uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, aliwataka wananchi mkoani Dodoma kujitokeza na kujiandisha kwenye daftari la kudumu la wapigakura ili wapate fursa ya kuchagua viongozi wanaowataka katika uchaguzi mkuu 2020.

Dk. Charles alisema wameshaboresha daftari hilo katika mikoa 15.

" Hivi sasa tupo katika mkoa wa Dodoma kwenye wilaya za Dodoma Mjini, Bahi, Chamwino na Kongwa na turatarajia kufunga kesho na baada ya hapo tutahamia wilaya za Mpwapwa (Dodoma), Chunya, Mbalali, Rungwe na Iringa na baadaye Ruvuma na Songea," alisema.

Alisema ni matarajio ya Tume kuwa uboreshaji huo ukamilike Machi mwakani na majina kubandikwa katika maeneo mbalimbali.


**CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)**
(Tanzania Teachers' Union – TTU)

P.O. Box 3077 DODOMA — Fax: 255 262323452
Cable: WALIMU DODOMA — Telephone: 255 262323451
E-mail: info@ttu.or.tz

## INVITATION FOR PRE QUALIFICATION FOR PROPOSED CONSTRUCTION OF OFFICE BUILDING AT CHATO

8th December, 2019

1. Tanzania Teachers Union (TTU) has set aside funds towards the cost of the construction of its district office at Chato and it intends to apply part of the proceeds of this funds to cover eligible payments under the contract for office building construction. Tanzania Teachers Union now intends to pre-qualify Applicants for construction of office building at Chato, Geita. It is expected that invitations to tender will be made in January, 2020.

2. Pre-qualification will be conducted through Tanzania Teachers' Union (TTU) financial Regulation, 3rd edition approved by TTU National assembly in February 1st 2018, and will be opened and read to all applicants on the day of tender opening.

3. Tanzania Teachers Union intends to pre-qualify contractors registered in Class Five (5) and above in Building Category for the proposed construction of an office building at Chato.

4. Interested applicants may submit applications at the office of General Secretary, TANZANIA TEACHERS UNION, CWT Building Jamhuri Street, Dodoma municipal in Dodoma on or before 24th December, 2019.

5. All applications in one original plus two copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address below on or before 1400 hours 24th December, 2019. Applications will be opened promptly thereafter before the Tender board on the day of tender opening.

6. The outer cover containing the applications shall be properly marked **"GENERAL SECRETARY, TANZANIA TEACHERS UNION (TTU), P.O. BOX 3077 DODOMA**

7. Tender board team will evaluate using on but not limited to the following criteria's;
   i. Company Experience
   ii. Company Organization
   iii. Structure i.e management processes, operational procedures, & turnover.
   iv. Quality
   v. Safety
   vi. Senior Management
   vii. experience
   viii. Current Projects/Backlog
   ix. number, size, and location of projects i.e percent of capacity being utilized, status and expected completion period
   x. Financial Strength

8. Late applications, portion of applications, electronic applications, and applications not received, applications not opened and not read out in tender board at the tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

Mwl. Deus G Seif
GENERAL SECRETARY
TANZANIA TEACHERS UNION

GENERAL SECRETARY
TANZANIA TEACHERS' UNION (TTU)
DODOMA - HEADQUATERS

215549902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ukatili kijinsia upingwe

**MAADHIMISHO** ya Siku 16 za Kupinga Ukatili zilifika kilele chake jana, kwa maeneo mbalimbali kuadhimisha kwa kuwa na maandamano, visa mkasa vya wanawake na wanaume waliopitia ukatili huo katika safari za maisha.

Kauli mbiu ya mwaka huu ilikuwa 'Kizazi Chenye Usawa: Simama Dhidi ya Ubakaji', lengo ni kuongeza ushawishi, kubadilishana taarifa, uzoefu, kujenga uwezo wa pamoja kwa jamii kupambana na ukatili wowote unaotokea kwenye jamii.

Chimbuko la Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ni mauaji ya kinyama ya wadada wa Mirabelle yaliyofanyika nchini Dominika mwaka 1960, mnamo mwaka 1991, Umoja wa Mataifa tarehe hiyo ukaifanya kuwa Siku ya Kimataifa ya Kupinga Unyanyasaji dhidi ya Wanawake.

Kwa makusudi hayo Umoja wa Mataifa ulitenga siku 16 ikiwa ni Novemba 25 ambayo ni siku ya tamko kupinga unyanyasaji dhidi ya wanawake na Desemba 10 ambayo ni Siku ya Tamko Rasmi la Haki za Binadamu ikiwa ni ishara ya kuhusisha ukatili huo na uvunjaji wa haki za binadamu.

Kwa Tanzania, jitihada zimefanyika ikiwamo kuruhusu mashirika yasiyo ya kiserikali kama Chama cha Wanasheria Wanawake (Tawla), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (Tamwa), Mashirika ya Umoja wa Mataifa UNFPA na UN- Women Bara na Visiwani, ambao kwa pamoja wametoa elimu kwa jamii na uraghibishi kuhusu kupinga ukatili.

Aidha, jitihada nyingi kwa kushirikiana na wafadhili zimewezesha kuanzisha madawati ya jinsia kwenye vituo mbalimbali vya polisi ambayo yamewawezesha watu wote kutoa taarifa za ukatili wowote waliofanyiwa kwenye jamii.

Ukatili unaotendwa kwa jamii kwa kiasi kikubwa ni ndoa za utotoni ambazo ziliwafanya wasichana wengi wasiendelee na masomo. Mwingine ni wanawake kunyimwa umiliki wa ardhi licha ya mabadiliko ya sheria ya ardhi kuruhusu, lakini mila na tamaduni za baadhi ya maeneo zimetumika kumnyima haki hiyo na kuendeleza mfumo dume.

Pia wa majumbani kwa maana ya ubakaji, ulawiti, vipigo kwa wanawake na wakati mwingine wahusika kutokutoa taarifa kwa kuogopa kuharibu mahusiano na wengine kuondoa kesi kwenye vyombo vya sheria.

Katika maadhimisho hayo kilio kikubwa kilikuwa madawati vya jinsia ambayo baadhi yameshindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Kadhalika kwa vyombo vya sheria kwamba licha ya kuwapo ushahidi wote, lakini kesi zinachukua muda mrefu kiasi cha waloumizwa kukata tamaa na wengine kutofika mahakamani. Pia baadhi ya madaktari wametajwa kuharibu ushahidi kwa kuwa wanapewa rushwa ambayo huleta madhara kwenye kesi kama hizo hususan ikiwa aliyetenda jambo hilo ni mtu mwenye uwezo, na wakati mwingine jambo kumalizika au kuishia Polisi kwa madai ya kukosekana ushahidi.

Wakati wa maadhimisho hayo jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, alitoa takwimu za miezi kumi zilionyesha matukio ya ubakaji yameongezeka kutoka 608 hadi 719 kwa miaka miwili.

Takwimu hizi ni kiashiria bado kuna kazi kubwa ya kufanya kuanzia kwenye jamii, wadau na taifa kwa ujumla kwa kuwa idadi ya watoto wanaobakwa yanaongezeka kwa kasi na waathirika ni watoto ambao hawawezi kujitetea.

Kuwapo kwa matukio haya maana yake jamii haijatimiza wajibu wake ipasavyo, na inapaswa kuchukua hatua kuanzia sasa kwa kuwa madhara ya kisaikolojia, kimwili kwa maana ya kuambukizwa maradhi mbalimbali ukiwamo Ukimwi ni mkubwa sana.

Ni rai yetu kwa serikali kuendelea kuimarisha madawati ya jinsia na ushirikiano thabiti kwa mashirika ambayo yanatoa elimu, uraghibishi na jitihada mbalimbali za kuielimisha jamii kuondokana na fikra potofu ambazo zinazidi kumkandamiza mtoto wa kike na mwanamke kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# 'Umeteleza mkuu eti bendera ni uchafu?'

**KUWAPO** kwa vyama vingi vya siasa nchini, kunatokana na Bunge na Baraza la Wawakilishi kufanya kikao mwaka 1992 kilichojadili mabadiliko muhimu ya kikatiba na sheria.

Lengo lilikuwa kuruhusu mfumo wa vyama vingi na bunge lilipitisha muswada wa kuingia katika utaratibu huo na kufuta vifungu vyote vilivyokuwa vinatoa mamlaka kwa chama kimoja na cha pekee cha siasa.

Baadaye kikawekwa kifungu cha 3 (1), katika katiba kinachosomeka;"Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa".

Kifungu kingine ni cha 8 (1), kisemacho: "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inafuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii, kwa hiyo wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi, kwa mujibu wa katiba hii."

Kuwekwa kwa vifungu hivyo kulifuatiwa na kutungwa, kujadili na kupitisha sheria ya vyama vingi vya siasa, huku serikali ikiwasilisha muswada wa utaratibu wa kuendesha shughuli za siasa katika mfumo wa vyama vingi.

Sheria ya vyama vingi inaweka wazi kuwa chama chochote chenye usajili wa kudumu kitafanya mikutano yake ya kitaifa, kimkoa na kiwilaya na katika ngazi za chini kwa mujibu wa katiba.

Kwamba endapo chama kinakusudia kufanya mikutano au maandamano sehemu yoyote ya umma, kitatoa taarifa chini ya saa 48 kabla ya mkutano kwa ofisa wa polisi ambaye ni kiongozi wa eneo mkutano utakapofanyika.

Lakini pamoja na sheria kutambua uwepo wa vyama vingi, kuna baadhi ya viongozi ambao hawalikubali hilo.

Kiongozi wa serikali, anaripotiwa na vyombo vya habari kuwa anawakamata wanachama wa upinzani kwa sababu ya kupeperusha bendera za vyama vyao katika maeneo yao ya utawala.

Wengine wanadaiwa kuamrisha kushushwa bendera za vyama vya upinzani mara viongozi wa kitaifa wanapofanya ziara katika maeneo ya "wakubwa" hao, hadi waondoke ndipo wanaruhusiwa kuzipeperusha.

Tunajiuliza hivi kuna kiongozi asiyejua kwamba Tanzania inafuata mfumo wa vyama vingi hadi bendera za vyama vya upinzani zifichwe? Waamuru bendera zifichwe au zishushwe kwa lengo geni hasa?

Wakati hayo yakiendelea sehemu mbalimbali nchini, kuna kiongozi mwingine amekaririwa na vyombo vya habari akiwaagiza wenyeviti wa vitongoji kuondoa bendera zote za vyama vya upinzani na kubakiza za CCM.

Mkuu wa Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa, Dk. Halfan Haule, ndiye aliyetoa maagizo hayo wakati akiwaapisha wenyeviti hao na kudai eti bendera hizo zitawachanganya wananchi wasifahamu ni wapi wanapatikana.

"Sitaki kuona zinapepea kwenye nyumba ya mtu yeyote, na atakayebisha tutamkamata na kumfungulia mashtaka ya kusababisha uchafu, atakwenda jela mwezi mmoja au kulipa faini ya Sh. 50,000," anasema DC huyo.

Kauli kama hizi hazipendezi kutolewa na kiongozi wa serikali, hasa kwa kuzingatia kwamba anailinda na kuitetea katiba iliyoruhusu mfumo wa vyama vingi ambavyo vipo nchini kwa zaidi ya miaka 20 sasa.

Akumbuke kuwa hakuna sababu ya kuleta uhasama wa kisiasa kwa wana Sumbawanga. Mheshimiwa DC atakuwa ameteleza kwa kauli yake hiyo, ni vyema akarejea kwenye katiba na Sheria ya Vyama vya Siasa, ili kuepusha mkanganyiko zaidi.

Pengine si sahihi kuziita bendera za vyama vya upinzani uchafu wakati anajua ni mali za vyama hivyo na zimegharamiwa na walipa kodi wa Tanzania.

Katika mfumo wa vyama vingi, hakuna chenye haki kuliko vingine, hivyo ni vyema viongozi wakajaribu kuepuka kauli zinazolenga kuwagawa Watanzania kwa aina ya itikadi zikiwamo za kisiasa.

Ikumbukwe kuwa mtindo wa baadhi ya wakuu wa wilaya na mikoa kuweka watu rumande ulishakatazwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, George Mkuchika na kuwataka kuzingatia taratibu na sheria.

Kauli ya DC huyo inaonyesha huenda atawatupa wapinzani rumande iwapo bendera za vyama vyao zitaonekana juu ya milingoti kwani alishaziita kuwa ni uchafu na kama zitaendelea kupeperushwa, bila kujali kwamba vyama hivyo vina mchango katika ustawi wa demokrasia nchini.

HABARI KITAIFA




Mafundi wa kampuni ya Chico wakiendelea na kazi ya ujenzi wa daraja karibu na Shule ya Mama Salma Kikwete jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Taasisi macho kanda, wodi saratani kujengwa Bugando

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

HOSPITALI ya Rufani ya Kanda Bugando, inatarajia kuanzisha ujenzi wa taasisi ya magonjwa ya macho kanda na ujenzi wa wodi ya magonjwa ya saratani.

Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Bugando, Prof. Abel Makubi, alisema hayo juzi katika mkutano wa watumishi na wafanyakazi wa hospitali hiyo, kujadili uboreshaji zaidi wa huduma za afya katika hospitali ya Bugando mpya mwaka 2019.

"Hospitali yetu tunatarajia kuanzisha ujenzi wa taasisi ya macho kanda, utakaogharimu zaidi ya Sh. bilioni tatu na ujenzi wa wodi ya saratani utakaogharimu kiasi cha Sh. bilioni 1.7 kukamilika zilizotolewa na Serikali kupitia Wizara ya Afya," alisema Prof. Makubi.

Prof. Makubi alisema fedha za ujenzi wa taasisi ya macho, zimetokana na mapato ya ndani pamoja na wafadhili unaotarajia kukamilika ndani ya mwaka mmoja na nusu kuanzia sasa. "Lakini pia ujenzi wa wodi ya saratani, tayari Serikali kupitia Wizara ya Afya, imeshatoa hizo Sh. bilioni 1.7, kwa ajili ya ujenzi huo, kanisa katoriki, wadau na wafadhili nao wanashiriki kusaidia, alisema.

Aidha, alisema kuwa mapato yatokanayo na dawa pekee katika hospitali hiyo yamepanda kwa mwezi kutoka Sh. milioni 400 Desemba mwaka 2018 hadi Sh. bilioni 1.4 mwaka huu pamoja na bima ya afya kuongezeka wagonjwa wake kutoka 100 hadi 240 kwa siku.

Vile vile, alisema wagonjwa wameongezeka kwa siku mwaka 2017,kutoka 600 hadi 1,500 mwaka 2019 na mapato ya ndani yameongezeka kutoka Sh. bilioni 1.1 kwa mwezi hadi Sh. bilioni 4.

Alisema kuwa katika hospitali yake wizi wa dawa za wagonjwa umepungua kwa asilimia kubwa, baada ya kuwekwa mfumo maalumu wa kisasa wa kudhibiti wizi huo. Awali,watumishi na wafanyakazi walikuwa wanakamatwa getini wakiwa wameiba dawa na kuficha sehemu za siri, na wengine kuzikalia kwenye gari wakati wa kwenda nyumbani.

Prof. Makubi alisema hospitali ya Bugando inatarajia kufanya sherehe za Bugando Day Desemba 14, mwaka huu, ambapo watumishi na wafanyakazi kumi bora watazawadiwa Sh. 500,000 kila mmoja.

Aliwataka madaktari,wauguzi pamoja na wafanyakazi wengine kufanyakazi kwa bidii, kuwa na nidhamu kazini wakati wakitoa huduma za wagonjwa, kutoa majibu mapema ya mgonjwa bila kuchelewesha ili ajue anachoumwa pamoja na vipimo kufanyika kwa wakati.

Alisema kuwa hali hiyo itamuondolea yeye changamoto ya wananchi na wagonjwa kumpigia simu ofisini kwake, wakilalamikia kutopewa huduma bora wakati wa kuhudumiwa.

# Mvua yaua mifugo, kuharibu nyumba

**Na Jumbe Ismailly,** ITIGI

MVUA zinazoendelea kunyesha mkoani Singida, zimeanza kuleta madhara kwa kuua mifugo, kuharibu miundombinu ya barabara na kuangusha baadhi ya nyumba za wakazi wa Kijiji cha Munkawa, Kata ya Rungwa, wilayani Manyoni.

Mvua hizo zilizonyesha kwa takribani saa sita, zimeua ng'ombe wawili maksai wa mfugaji wa Kijiji cha Munkawa, Lata Hwima, baada ya kusombwa na maji kwenye mto Musa.

Akizungumzia tukio hilo, Hwima alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya mchana wakati ng'ombe hao wakitokea kulima shamba la mwananchi mmoja kwa malipo ya Sh. 30,000 kwa hekta moja.

Alieleza kwamba walikuta mto huo umejaa maji, lakini aliamua kuwavusha ng'ombe hao ili awapeleke nyumbani, huku wakiwa wamefungwa joki shingoni, na walipofika katikati ya mto huo walivutwa na maji na kutumbukia ndani ya mto huo na kufa.

Kwa mujibu wa Hwima, kufa kwa ng'ombe hao kumesababishia hasara ya Sh. 400,000, hivyo kuiomba serikali kuwatengenezea daraja la kijiji.

Mkazi mwingine wa Kijiji cha Munkawa, Madaha Kurwa, aliishauri serikali kuangalia uwezekano wa kuitengeneza barabara pamoja na daraja hla kijiji ili wananchi wawe na uhakika wa kuwa na mawasiliano na makao makuu ya Kata ya Rungwa.

Diwani Rungwa, Charles Machapaa, akieleza kusikitishwa na matengenezo yasiyokuwa na kiwango ya barabara hiyo na ujenzi wa daraja, na kwamba iwapo viwango vingezingatiwa, hali hiyo isingetokea. "Mfugaji asingeweza kupoteza mifugo yake kwa sababu alikuwa anakwenda kuzalisha kwani alikuwa ametoka kulima na pia kesho yake alikuwa na lengo la kurudi kulima tena... amekosa nyenzo za kulimia maana yake ni kumsababishia umaskini," alisema diwani Machapaa.

Wakati huo huo abiria zaidi ya 80 wamenusurika kufa, baada ya basi la Kampuni ya Singida Airline lenye namba za usajili T.306 AXT walilokuwa wakisafiria kutoka Rungwa kwenda Singida tairi kupasuka na kuacha njia karibu na Ofisi za Idara ya Maliasili Halmashauri ya Itigi, juzi jioni jioni.

**CHAP CHAP AUCTIONMART & REAL PROPERTY CO. LTD**
Head Office: Plot No. 125 Block "M" Mbizi "A" Street, Jangwani Area
P.O.Box 49 Sumbawanga-Rukwa, Mobile: 0755-812732,0621-061461
Email: **chapchapcompany@yahoo.com.**
***Dealers in: Debt collection, Auction mart, Civil and Building Engineering contractors, Court broker, general broker, Business consultancy***

**TANGAZO LA MNADA**
**(Sahihisho la Tangazo lililopita)**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA MTEJA WETU BENKI YA MAENDELEO, TUTAUZA KWA NJIA YA MNADA WA HADHARA MALI ZILIZOORODHESHWA HAPO CHINI AMBAZO ZILIWEKWA KAMA DHAMANA YA MKOPO, MNADA UTAFANYIKA MAHALI ZILIPO, SIKU NA SAA KAMA ILIVYOONYESHWA KATIKA JEDWALI LIFUATALO:-

| S/N | JINA LA MKOPAJI | MALI ITAKAYOUZWA | MKOPESHAJI | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA | MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | J F 05 SPARE PARTS ENTERPRISES. | NYUMBA YA BIASHARA KIWANJA NO. 1487 KITALU'TT' MAJUMBA SITA | BENKI YA MAENDELEO | SUMBAWANGA (MJINI) | 21.12.2019 | 4:00 ASUBUHI |
| 2 | J F O5 SPARE PARTS ENTERPRISES. | NYUMBA YA KUISHI KIWANJA NO.25,KITALU 'U' KATANDALA | BENKI YA MAENDELEO | SUMBAWANGA (MJINI) | 21.12.2019 | 5:00 ASUBUHI |
| 3 | J F O5 SPARE PARTS ENTERPRISES. | NYUMBA YA BIASHARA KIWANJA NO. 145, KITALU 'U' KATANDALA | BENKI YA MAENDELEO. | SUMBAWANGA (MJINI) | 21.12.2019 | 6:00 MCHANA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. NYUMBA ITAUZWA KAMA ILIVYO " AS WHERE IS BASIS"
2. MNUNUZI ATAKAYE SHINDA ATALIPA MALIPO YA AWALI ASILIMIA 25% YA BEI YA MNADA SIKU YA MNADA, NA 75% NDANI YA SIKU 14 BAADA YA MNADA.
3. MNUNUZI ATAKAYESHINDWA KUMALIZA SALIO LA ASILIMIA 75% KATIKA MUDA ULIOPANGWA HAPO JUU HATORUDISHIWA FEDHA ALIZOLIPA AWALI NA MNADA UTARUDIWA SIKU NYINGINE ITAKAYOPANGWA.
4. GHARAMA ZOTE ZA KUBADILISHA HATI MILIKI NI JUU YA MNUNUZI.
5. WATEJA WOTE MNAKARIBISHWA KUONA NA KUKAGUA NYUMBA HIZO MUDA WOTE ISIPOKUWA USIKU, WASILIANA NA KAMPUNI YA CHAP CHAP AUCTIONMART AND REAL PROPERTY NAMBA ZA SIMU: 0755-812732/0621 – 061461

***CHAP CHAP AUCTION MART NI KIBOKO YA MADENI SUGU***

2155S0302

# Mwanamke aelezea maisha yake akiwa gerezani na mwanawe

INATOKA UK. 2

ya biashara ya madini, lakini zilisimama kutokana na mimi kuwa gerezani kutumikia kifungo cha miaka 30 ambacho nashukuru sijakimaliza kutokana na kupata msamaha wa Rais," alisema na kuongeza kuwa maisha ya gerezani ni tofauti sana na uraiani.

"Wakati naingia gerezani niliwaacha watoto wangu wa kike wawili wakiwa wadogo sasa sijui wakoje na wanaendeleaje. Sina taarifa zozote kuhusu wanangu, najua wapo nikifika nitajua wanaendeleaje," alisema.

Ramadhani alimshukuru Rais Magufuli kwa msamaha alioutoa na kuahidi kuachana na vitendo vya uhalifu na kumwomba kuwakumbuka wafungwa wengine waliobaki katika magereza mbalimbali ili kupunguza msongamano uliopo.

"Tunamshuru Rais Magufuli, lakini tunaomba awaangalie na wengine wafungwa walioko magerezani. Kuna wazee wengi nimewaacha gerezani," alisema Ramadhan. Akisimulia maisha ya gerezani, alisema kwa upande wa chakula wanakula, lakini shida iko kwenye sehemu wanazolala.

Awali Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi (ACP) Kenneth Mwambije, alisema wafungwa 385 wa magereza mbalimbali ya mkoa huo wameachiwa huru kutokana na msamaha wa Rais alioutoa wakati wa maadhimisho ya sherehe za Uhuru.

**RC ALONGA**

Akikagua orodha ya wafungwa waliostahili kupata msamaha huo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, aliwataka wafungwa hao kwenda kuwa raia wema wanaozingatia kanuni, taratibu na Katiba ya nchi.

Alisema Rais ametoa msamaha huo kwao, hivyo hawana budi kwenda kuwa mfano wa kuigwa katika jamii kwa kujishughulisha na shughuli za uzalishaji kama walivyofundishwa wakati wakiwa gerezani.

# Mikopo elimu ya juu kaa la moto

INATOKA UK. 3

"TCU na Bodi ya Mikopo zote ni taasisi za serikali, suala la kupata uthibitisho kwamba mwanafunzi huyu alihama mafunzo ni suala la sekunde, tunasikitishwa na huu urasimu ambao mwisho wa siku unaosababisha maisha ya wanafunzi kuwa magumu."

Malekela aliitaka serikali iingilie suala hilo kwa sababu wanafunzi wengi hawajui nini hatima yao ya masomo. "Suala lingine linahusu, fedha za wanafunzi wanaostahili kupata mikopo, lakini zimekatwa, mapema mwezi huu Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia alizungumza kwamba kumekuwa na changamoto ndani ya bodi ya mikopo," alisema.

Alisema naibu huyo alieleza kuwa changamoto hiyo kimtandao ilisababisha kukatokea kutawanywa baadhi ya fedha za wanafunzi na wengine kupata kidogo.

"Tangu naibu waziri azungumze sasa ni mwezi na wanafunzi hawajui nini hatima yao, tunataka suala hili lifanyiwe kazi kwa haraka kwa sababu hizi ni stahiki za wanafunzi na hazijawekwa kama mapambo ni matumizi ya watu ambayo mwisho wa siku zinawasaidia kielimu," alisema. Alisema ipo haja ya kufanyika mapitio upya kwa sababu wanafunzi wengi wamekuwa wakiacha masomo kwa kukosa ada.

"Wanafunzi wakishindwa kulipa ada wanashindwa kufanya mitihani na kushindwa kuendelea na vyuo vikuu, serikali ione umuhimu wa kusaidia hili.

"Namna bora ya kukabiliana na changamoto hizi ni kugharamia mahitaji ya wanafunzi ambayo ni ada, fedha hizi ambazo zimetolewa kwa wachache, wakienda kwa mtindo wa kulipa ada kila mwanafunzi hataachwa nyuma."

"Mtandao unataka serikali iliangalia suala hili ili mwisho wa siku wanafunzi wote wanaostahili kupata mikopo wapate," alisema.




# Balozi Marekani amwaga chozi akimuaga Mufuruki

INATOKA UK. 2

kuhakikisha sekta ya viwanda na biashara inakua nchini.

Katika ibada ya kumuaga jana, Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Kairuki, alisema Mufuruki alikuwa mtu mwema, mchapakazi hodari, mzalendo na kiongozi mahiri.

"Alikuwa mstari wa mbele kushauri masuala mbalimbali ya biashara na uwekezaji na kutoa maoni yake na alishauri mambo gani ya kisera na kisheria yarekebishwe ili kuhakikisha tunaendelea kurahisisha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji Tanzania," alisema.

"Tutaendelea kutambua mchango wake alipokuwa mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Uhifadhi Mazingira, mwenyekiti na mjumbe wa bodi wa chama cha sekta binafsi cha watendaji wa kampuni na nafasi mbalimbali alizoshika ndani na nje ya nchi," alisema.

Kairuki alisema Mufuruki aliamua kuweka mawazo yake kwenye maandishi kupitia kitabu chake cha 'Tanzania Industrialization Journey, 2016-2056' ambacho kimeeleza kuhusu safari ya ujenzi wa viwanda Tanzania na kutoa mwelekeo.


"Serikali itaendelea kumuenzi kwa vitendo kuhakikisha tunaendelea kuwa wasikivu wa maoni na mapendekezo ya sekta binafsi ili kutetea maslahi ya biashara ya sekta binafsi," alisema. Akitoa salamu za Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, Balozi Martin Kimani, alisema Rais ametoa pole kwa familia ya marehemu.

Alisema Rais Kenyatta atamkumbuka Mufuruki kama kiongozi aliyeacha kumbukumbu iliyotukuka kwa kuwa mmoja wa waanzilishi wa Taasisi ya Kuwakuza Viongozi wa Afrika, iliyoanzishwa mwaka 2002.

Simbeye kwa upande wake, alisema Mufuruki hakumaliza kitu ambacho alitaka kukifanya kuhusu sekta binafsi nchini na kwamba walikuwa wakizungumza mengi na alidhani kazi ya kuendeleza sekta binafsi Tanzania ilikuwa bado haijakamilika.

Mdogo wa marehemu, Akili Mufuruki, alisema Ali alikuwa mtoto wa pili katika familia ya watoto tisa na alikuwa kiongozi bora kwa wana familia wote na walijifunza mengi kutoka kwake ikiwamo uvumilivu.

"Mufuruki enzi za uhai wake alituongoza katika misingi mizuri na alijitahidi kuipa familia heshima pamoja na taifa kwa ujumla," alisema.




# Ukosefu madarasa wachelewesha wanafunzi

INATOKA UK. 3

Alisema kutokana na ufaulu huo, Mkoa wa Lindi unakabiliwa na upungufu wa vyumba 44 ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa la saba.

Akichanganua mahitaji hayo, alisema waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza, Kilwa inaongoza kwa mahitaji ya vyumba 25, ikifuatiwa na Nachingwea (8), Ruangwa (7), Halmashauri ya Mtama (4), wakati Lindi Manispaa na Liwale hazina tatizo la vyumba.

Aliwataka wakurugenzi wote ambao halmashauri zao zimekumbwa na upungufu huo, kufanya jitihada kuhakikisha wanafunzi wote 1,695 wakiwamo wasichana 877 na wavulana 818 waliokosa nafasi, wanaanza masomo kabla Februari 15, mwakani.

"Hawa wanafunzi waliofaulu wametimiza wajibu wao, na hawapaswi kukoseshwa haki yao kuendelea na elimu ya sekondari kwa namna yoyote," alisema Madenge.

Alisema watoto wanane wenye mahitaji maalum, watano wavulana na watatu wasichana wamechaguliwa kujiunga na sekondari za bweni nje ya Mkoa wa Lindi, huku wanafunzi 52, wavulana 22 na waschana 30, waliofika ngazi ya taifa, mashindano ya UMITASHUMTA wamepangiwa kuendelea na masomo Mahiwa Sekondari kuanzisha kitalu cha michezo cha mkoa huo.

HABARI KITAIFA

# Kipindupindu mtihani kwa wenyeviti mitaa, vitongoji

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, Jacob Mtalitinya, amewataka wenyeviti wa mitaa na vitongoji kusimamia usafi ili kuzuia mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili sasa halmashauri hiyo haijakumbwa na mlipuko wa ugonjwa huo, na wameingia kazini, hivyo jukumu la kwanza ni kuhakikisha wanasimamia usafi kudhibiti ugonjwa huo.

"Nendeni mkasimamie usafi hasa katika kipindi hiki cha masika, wale mtakaowakamata kwa kushirikiana na maofisa afya ambao maeneo yao ni machafu muwatoze faini ya Sh. 50,000 kwa mujibu wa sheria, lengo ni kuhakikisha maeneo yao yanakuwa safi ili ugonjwa wa kipindupindu usije kutokea," alisema.

Mtalitinya aliwaasa wenyeviti hao kujiepusha na rushwa watakapokuwa wanawahudumia wananchi.

Mkurugenzi huyo aliwataka wenyeviti hao kwenda kuibua na kusimamia miradi ya maendeleo iliyopo, ikiwamo ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na vyumba vya madarasa ili wanafunzi waliofaulu wapate nafasi ya kuanza kidato cha kwanza mapema mwakani.

## Serikali: Cheti alama ubora kwa wauza chakula, vipodozi lazima

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewataka wafanyabiashara wa chakula na vipodozi kuhakikisha wanapata cheti cha alama ya ubora, kwani bidhaa hizo zinaangukia kwenye kundi la lazima.

Akizungumza wakati wa maonyesho ya nne ya viwanda jijini Dar es Salaam, Ofisa Udhibiti Ubora wa Viwango wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mary Kapwani, alisema wafanyabiashara wa bidhaa hizo wanalazimika kuwa na cheti cha ubora.

"Wafanyabiashara wote ambao wanauza au kuingiza chakula na dawa wanatakiwa kuhakikisha bidhaa zao zimehakikiwa ubora na shirika husika, kabla ya kuingia sokoni," alisema.

Awali bidhaa hizo zilikuwa chini ya usimamizi wa iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) kwa sasa zimehamishiwa TBS.

Alidokeza kuwa wafanyabiashara wa chakula na vipodozi ambao wana vyeti vya TFDA watambue kuwa muda wa matumizi unakwisha mwakani.

"Tunawataka wafanyabiashara kuja TBS au kutuma maombi ya kupata alama ya ubora kupitia mtandao," alisema.

Alisema maofisa wa shirika hilo watapokea maombi hayo na kutembelea jengo husika ili kuona kama mwombaji amekidhi viwango vya uzalishaji au la.

Akielezea kuhusu maonyesho, alisema yana umuhimu mkubwa hasa kwa wajasiriamali wakubwa na wadogo kupata fursa ya uelewa wa masuala mbalimbali kuhusu viwango.

"Tumekuwa tukishiriki maonyesho ya aina mbalimbali kwa ajili ya kujenga uelewa kwa wajasiriamali ili waweze kuhakikisha kuwa bidhaa zao zina viwango na kuweza kupenya masoko ndani na nje ya nchi," alisema.

Kapwani alisema alama ya ubora inawawezesha wafanyabiashara wadogo na kati kuuza bidhaa zao ndani ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki bila kikwazo.

Aliwataka wafanyabiashara wanaotaka kuuza bidhaa zao nje ya Afrika Mashariki kuwasiliana na shirika hilo ili wapatiwe maelekezo zaidi.

Aliwapongeza wajasirimali wawili waliopata soko la bidhaa zao nje ya Bara la Afrika ambao kwa sasa wameanza mchakato wa kupata alama ya ubora.



Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Edward Mpogolo, akipanda mti kwenye eneo la Halmashauri ya Ikungi mkoani Singida. Pia kiongozi huyo aliambatana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Justice Kijazi, na watumishi wengine kufanya usafi maeneo mbalimbali ikiwa ni maadhimisho ya Siku ya Uhuru, ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## 4,000 wafanyiwa ukatili kijinsia miezi 9 Kagera

**Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WANAWAKE na watoto 4,307 wamefanyiwa ukatili wa kijinsia mkoani Kagera katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ofisa Ustawi wa Jamii mkoani humo, Rebeca Gwambasa, alisema kwa upande wa wanawake waliofanyiwa ukatili huo ni 2,545 na watoto wenye umri wa kuanzia mwaka mmoja hadi 17 ni 1,762.

Gwambasa alisema pia wanaume 830 walifanyiwa ukatili huo katika kipindi hicho, na kufanya idadi ya watu waliofanyiwa ukatili wa kijinsia mkoani Kagera katika kipindi hicho kufikia 5,137.

"Takwimu hizi zinaonyesha watu 1,284 wamefanyiwa ukatili wa kimwili ikiwamo kipigo kwa wanawake, watu 2,412 wamefanyiwa ukatili wa kihisia au kisaikolojia, watu 286 wamefanyiwa ukatili wa kingono na watu 1,155 wamefanyiwa ukatili wa kiuchumi," alisema Gwambasa.

Alisema katika mkoa wa Kagera halmashauri ya wilaya inayoongoza kwa kuwa na vitendo vingi vya ukatili wa kijinsia ni Muleba na kuwa Wilaya ya Ngara ndiyo yenye kiwango cha chini cha idadi ya watu wanaofanyiwa vitendo hivyo.

"Sababu zinazochangia kufanyika kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia ni malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto yasiyozingatia maadili, matumizi ya pombe, dawa za kulevya na migogoro na mifarakano ya ndoa," alisema.

Aidha, alitaja sababu nyingine zinazochangia kuwapo kwa vitendo hivyo kuwa ni umaskini, utelekezaji wa familia na utamaduni na mila potofu kama vile ndoa za ututoni na vipigo kwa wanawake kwenye ndoa vinavyotumika kama njia mojawapo ya kuwapa adhabu.

Alisema serikali ya mkoa inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana na vitendo hivyo kwa kuhamasisha jamii kwa kutumia vyombo vya habari na mikusanyiko mbalimbali.

"Lakini tunatoa elimu kwa timu za kuzuia ukatili wa kijinsia wakiwamo watumishi wa vituo vya kutolea huduma za afya, viongozi wa dini na watumishi kwenye vyombo vya maamuzi inayohusu jinsi ya kumhudumia mwathirika wa ukatili wa kijinsia," alisema.

Aidha, alisema jamii imehamasishwa kutoa taarifa mara wafanyiwapo ukatili kwa kuwahi kwenye vituo vya afya au polisi, kwa ajili ya kupata msaada wa haraka. Kwa mujibu wa Gwambasa, jumla ya mashauri 308 yalipelekwa mahakamani na kati ya hayo mashauri 232 yalimalizika kwa kutolewa hukumu mbalimbali, na mashauri 76 bado yanaendelea kusikilizwa.

Kufuatia Mkoa wa Kagera kushika nafasi ya nne kwa kuwa na asilimia 67 za ukatili, Shirika la Muungano wa Utepe Mweupe wa Uzazi Salama limeanzisha mradi wa kuzuia ukatili kwa wanawake na wasichana, ili kukabiliana na vitendo hivyo.

Akizungumza wakati wa semina kwa waandishi wa habari inayolenga kuweka mikakati ya kudhibiti vitendo hivyo, Meneja wa mradi huo, Datus Ng'wanangwa, alitaja aina za ukatili unaofanyika mkoani Kagera kuwa ni wa kimwili, kisaikolojia, kingono na kiuchumi.

# Serikali yatoa 5 usajili wa kampuni kimtandao

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

SERIKALI imesema imeridhishwa na utendaji kazi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (Brela) hasa kwa kusimamia usajili wa makampuni na majina ya biashara kwa njia ya mtandao na kwamba kwa upande wake serikali nayo inaandaa sheria ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara.

Hayo yakisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwezekezaji) Bi.Agellah Kairuki, wakati anahutubia mkutano wa mashauriano ambao ulihudhuriwa na watendaji wa serikali, wawekezaji na wafanyabiashara wa Mkoa wa Morogoro.

Mkutano umebaini changamoto za uwekezaji na alipendekeza namna ya kuzipatia majibu ili kuboresha mazingira ya biashara nchini.

"Hatua kubwa iliyofikiwa na Brela kupitia mfumo wao ni kwamba sasa usajili wa jina la biashara pamoja na namba ya mlipa mkodi (TIN) vinapatikana sehemu moja. Jambo hili linazidi kuboresha mazingira ya biashara nchini," alisema Waziri Kairuki na kuongeza: "katika kuhakikisha mazingira ya biashara yanaboreshwa Ofisi ya Waziri Mkuu nayo inaanda muswada wa sheria mpya ya itakayoitwa Uwezeshaji wa Biashara (Business Facilitations Act) ambayo itafanya utekelezaji wa mapendekezo yaliyopo kuwa katika blueprint."

Alisema biashara yoyote ni lazima ianze na usajili wa jina au Kampuni, na kwamba ongezeko la viwanda katika Mkoa wa Morogoro na maeneo mengine nchini ni ishara tosha kuwa Brela imetekeleza majukumu yake katika usajili wa majina ya biashara na makampuni.

"Mfumo huu wa usajili kwa njia ya mtandao ni moja ya maelekezo ya serikali kwa Brela kuboresha mazingira ya kufanya nchini. Uboreshaji huu umekuwa nyenzo ya kuwavutia wawekezaji na kuifanya azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati kutekelezeka kwa vitendo."

Aliongeza kwamba kuongezeka kwa idadi ya wawekezaji ni ushahidi kuwa Brela inafanya kazi yake kwa ufanisi.

Amesema wawekezaji wanatumia muda mfupi kupata usajili tofauti na hapo nyuma ambapo ilimlazimu mfanyabiashara kusafiri hadi Dar es Salaam akitafuta usajili.

Aliitaka Brela na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuendelea kuboresha mifumo yao ili wafanyabiashara kupata huduma ya majeresho ya mwaka (annual return) kwa njia ya mtandao.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Brela, Roy Mhando, kuna ushahidi kwamba mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao umerahisisha uanzishwaji wa biashara nchini kwa sababu mwananchi anaona mwenyewe kwamba gharama za usajili zimepungua.

"Mfumo wa BRELA umeunganishwa na mifumo ya taasisi nyingine za Serikali kama TRA, Wizara ya Ardhi ili kurahisisha utambuzi wa mlipa kodi na maeneo ya viwanda anapotaka kuwekeza hivyo umesaidia kuondoa usumbufu kwa mwekezaji kutoka taasisi moja kwenda nyingine kufata nyaraka au vibali," alisema Bi.Mhando

# Miradi ya Jumeme yaziondoa gizani kaya 5,000 Ukerewe

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya kaya 5,000 katika kisiwa cha Ukara wilayani Ukerewe mkoani Mwanza, zimenufaika na umeme jua unaozalishwa na kusambazwa na kampuni ya usambazaji umeme vijijini (JUMEME).

Hayo yamebainishwa hivi karibuni na mmoja wa wakurugenzi wa kampuni hiyo, Prof. Costa Mahalu, katika hotuba yake kwa maofisa kutoka Umoja wa Ulaya (EU) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), waliotembelea miradi ya umeme jua iliyopo wilayani hapo. Prof. Mahalu alisema kaya hizo zimenufaika kutokana na awamu ya kwanza ya mradi wa usambazaji umeme katika kisiwa hicho cha Ukara.

"Awamu ya kwanza iliyopewa jina la 'Uzalishaji umeme katika kukuza uchumi wa Tanzania' imeonesha utofauti kutokana na faida za kiuchumi na kijamii zilizopatikana.

"Kwa sababu mbali na kaya 5,000 kunufaika pia, wafanyabiashara wadogo na viwandani wameunganishwa. Lakini taasisi mbalimbali zinazotoa huduma za kijamii kama vile maji vijijini na hospitali zimeunganishwa," alisema.

Alisema huduma za Jumeme zimevifikia vijiji 20 kwenye visiwa 10 tofauti, na kuchochea uchumi wa eneo hilo jambo lililosaidia kuibua fursa nyingi za ajira.

"Malengo ya muda mrefu kwa Jumeme ni kuendelea kushirikiana na wazalishaji wadogo ikiwa ni pamoja na kuwekeza kwa waajiriwa wa eneo husika," alisema Prof. Mahalu ambaye ni Makamu wa Chuo Kikuu cha Mt. Agustino (SAUT). Aidha, alisema kampuni hiyo imekuwa ikizingatia utoaji wa fursa za ajira kwa Watanzania ili kuisaidia serikali kukabiliana na uhaba wa ajira kwa vijana nchini.

"Kila mmoja wa wafanyakazi wanaofanya kazi ya uhandisi katika miradi 12 ya Jumeme, ni Mtanzania. Kati ya watu 25 wanaounda timu ya kudumu ya Jumeme wenyeji ni 22, ambao hupewa upendeleo wa wazi linapokuja suala la kufanya kazi. "Kwa kuzingatia mafanikio ya awamu hii ya kwanza, tunatumaini kuwa na uwezo wa kutoa fursa zaidi za kazi kwa vijana wetu kwa kuendelea nao katika awamu ya pili, ya tatu na kuendelea zaidi katika miradi ya Jumeme." alisema.

Alisema ili kuongeza uweledi na ufanisi wa waajiriwa wazalendo, kampuni hiyo inaendelea kutoa mafunzo yanayowajengea uwezo wahandisi wa ndani na vijana wataalamu kwa madhumuni ya kuendesha gridi ndogo ndogo zinazoendelea kujengwa hapa nchini.

Pia alisema lengo la Jumeme ni kutoa umeme wa uhakika na wa bei nafuu kwa wakazi husika hususani maeneo ambayo umeme gridi ya Taifa hauwezi kufika.

"Lengo letu ni kufunga mifumo 300 ya uzalishaji umeme utakaoweza kuingizwa kwenye ya gridi ya Taifa na kusaidia watu zaidi ya 1,000,000 ifikapo mwaka 2023 katika vijiji mbalimbali nchini Tanzania."

Aliongeza kampuni hiyo ya Jumeme ilioundwa mwaka 2014 chini ya mradi wa "Micropower Economy roll out in Tanzania" na kufadhiliwa na EU, inalenga kukuza, kujenga, na kuendesha gridi ndogo za umeme jua katika vijiji mbalimbali nchini.



Baadhi ya mafundi mitambo wa kampuni ya uzalishaji na usambazaji umeme jua (Jumeme), wakifunga mitambo ya kuzalisha nishati hiyo katika moja ya miradi yake kisiwa cha Ukara wilayani Ukerewe, mkoani Mwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waomba sheria kudhibiti mifugo kuzurura

**Na Gurian Adolf,** NKASI

WAKAZI wilayani Nkasi mkoani Rukwa, wameziomba serikali za vijiji kutumia sheria zilizopo kudhibiti mifugo inayozurura ovyo kwani imekuwa ikikwamisha jitihada za uhifadhi wa mazingira kutokana na kula miti wanayoipanda.

Ombi hilo walilitoa jana katika mji wa Namanyere wakati Mkuu wa Wilaya hiyo, Said Mtanda, akihitimisha zoezi la siku saba la upandaji miti katika wilaya hiyo ambalo lilihitimishwa katika maeneo ya Ikulu ndogo wilayani humo.

Mmoja wa wakazi hao, Said Pembe, alisema baadhi ya wafugaji wamekuwa na tabia ya kuacha mifugo yao ikizurura ovyo na matokeo yake imekuwa ikila miti wanayopanda.

Alisema wapo baadhi ya wanyama kama mbuzi ambao mate yao yana sumu kwa mimea, wanapokula miti hiyo inakauka na kukwamisha jitihada za kuhifadhi mazingira.

Naye Maria Kalela, alisema katika kukabiliana na changamoto ya kuzurura mifugo ni vizuri serikali za vijiji zikawa zinawatoza faini wafugaji hao ili kudhibiti tabia ya kuiachia mifugo yao kuzurura ovyo.

Alisema pia viongozi hao wa serikali wawe wanawachukulia hatua watu wasiopanda miti kwani baadhi yao wamekuwa wakipuuzia na matokeo yake wamekuwa wakipatwa na majanga kama ya kuezuliwa nyumba zao wakati wa masika.

Naye DC Mtanda alisema kuwa Wilaya ya Nkasi imedhamiria kupanda miti milioni mbili kwa lengo la kuhifadhi mazingira.

Alisema wilaya imekuwa ikikabiliwa na uhaba wa vyanzo vya maji kutokana na kutokuwa na misitu ya kutosha, hata miti michache imekuwa ikikatwa ovyo kutokana na matumizi ya binadamu.

# Vijana kunufaika mtandao uvuvi, mifugo

**Na Mwandishi Wetu**

VIJANA kutoka mikoa 13 ya Tanzania Bara na visiwani wanatarajiwa kunufaika na mtandao wa vijana unaojihusisha na shughuli za uvuvi na mifugo.

Kuanzishwa kwa mtandao huo, kutawasaidia vijana nchini kujiajiri moja kwa moja kupitia kwenye sekta ya uvuvi na mifugo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mtandao huo, uliofanyika jijini hapa, Rais wa mtandao huo, Laban Boaz, alisema vijana chini ya miaka 35, kutoka mikoa mbalimbali watanufaika na mtandao huo kwa kufundishwa mbinu bora za kisasa za ufugaji.

Alisema lengo la kuanzishwa kwa mtandao huo, ni kuhamasisha vijana kujiajiri katika sekta ya mifugo na uvuvi kwa kutumia njia za kisasa ambazo zitasaidia kuongeza uzalishaji mali na ajira kwa vijana.

Laban alisema kilichofanya kuanzisha mtandao huo, ni baada ya kuangalia mwanya uliopo kati ya wazee na vijana.

"Mtandao huu utasaidia kuwapa ujuzi na maarifa namna ya kufuga kisasa na vijana waliopo vijijini ambao walikuwa hawafikiwi na maarifa hayo na lengo ni mtandao huo kuwanufaisha vijana," alisema Laban.

Alisema mtandao huo ulianzishwa jijini Dar es Salaam mwaka 2017, lengo likiwa kupanua wigo wa vijana nchini.

Mkurugenzi wa Uzalishaji na Masoko Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Felix Nandonde, alisema mtandao huo ni juhudi za muda mrefu ambazo zimefanywa na Umoja wa Afrika kupitia mradi wa kuendeleza rasilimali za wanyama (AU-IBAR).

Alisema hilo limewashirikisha vijana wanaojihusisha na kazi tofauti katika mnyororo wa thamani ya mifugo, samaki, kuku na nguruwe na kupitia mtandao huo watawekwa kufanya kazi ya mnyororo wa thamani.

Nandonde alisema serikali itaendelea kushirikiana na mtandao huo, kuwafikia vijana ili waitumie fursa hiyo ipasavyo.

Makamu wa Rais wa mtandao huo, Veronica Lyambiko, alisema wamefikia hatua ya kuanzisha mtandao huo, kwa kuwa vijana wengi nchini wanakabiliwa na tatizo la ajira.

Alisema, kupitia mtandao huo, idadi ya vijana wataingia na kuwafikia vijana vijijini.

# Wazazi wafundwa kupenda walimu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZAZI na walezi wa wanafunzi nchini, wametakiwa kuepuka uadui kwa walimu na kujenga urafiki ili wafundishe vizuri watoto wao.

Askari Polisi mstaafu wa mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Shem Kayobyo, aliyasema hayo juzi, wakati akizungumza na wazazi, walezi, wanafunzi na walimu wa shule ya awali na msingi ya New Light iliyopo wilayani humo.

Kayobyo alisema walimu ni watu muhimu kwa kukuza taaluma ya wanafunzi shuleni, hivyo wanapaswa kukumbatiwa ili wapate moyo na siyo wazazi kuwakwaza. "Walimu ni watu muhimu mno kwa kuwa wanatengeneza maisha yajayo ya wanafunzi wetu, ambao ni watoto wetu hivyo tuchukue jukumu la kuwajali na siyo kuanzisha nao ligi kama mtoto akikosea aadhibiwe," alisema.

Alipongeza uongozi wa shule, walimu na wanafunzi kwa kutoingia kwenye mchezo mchafu wa kununua mitihani, kama baadhi ya shule zinavyofanya na kutangazwa kwenye vyombo vya habari. Hata hivyo, aliwataka walimu na wanafunzi wa shule hiyo kujitahidi kitaaluma ili wapige hatua zaidi kwa kuwa nafasi waliyopo kiwilaya na kimkoa ni nzuri, lakini wanapaswa watoke hapo walipo.

"Hivi sasa mmeshika nafasi ya nne kiwilaya na wa saba kimkoa kwenye matokeo ya kuhitimu darasa la saba, mnapaswa kuwa wa kwanza wilayani Simanjiro na wa kwanza mkoani Manyara," alisema Kayobyo. Mwalimu mkuu wa shule hiyo, Tumaini Mbise, alisema wanajitahidi kupiga hatua kwa upande wa taaluma na kuwaomba wazazi na walezi wapeleke watoto wao.

Mbise alisema wanafunzi wanaopitia mikononi mwa shule hiyo, wanakua kwenye wakati mzuri katika suala la taaluma kwa sababu ya kuwa na walimu wazuri waliobobea.

Mmoja kati ya wazazi wenye wanafunzi shuleni hapo, Regina Anney, aliwapongeza walimu na uongozi wa shule hiyo kwa namna inavyowajali wanafunzi wake.



Mfanyabiashara wa nguo maarufu kwa jina la Rasi akiwa anatengeneza koti la jeans kwa kuweka staili za creizi katika kijiwe chake kilichopo katika njia ya Shivas mjini Arusha jana. **PICHA WOINDE SHIZZA**

# Balozi ahamasisha Sayansi kwa wasichana

**Na Cynthia Mwilolezi**, ARUSHA

BALOZI wa Taasisi ya Next Forum (NEF), Dk. Lwidiko Edward, amewataka wanafunzi wa kike, kutumia fursa zilizopo kusoma masomo ya mchepuo wa Sayansi, licha ya changamoto za kijamii zinazowakabili.

Alitoa rai hiyo jana wakati wa Wiki ya Sayansi iliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Nelson Mandela (NM-AIST), ambayo pamoja na mambo mengine, wanasayansi wanaochipukia saba walipewa tuzo za kutambuliwa mchango wao.

"Tumetoa tuzo kwa watafiti wanawake wanaochipukia katika Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati ambao walitambuliwa na wenzao katika maeneo mbalimbali na kupitia mchujo wa wataalamu, ili kuendeleza utafiti wao na kuhamasisha wasichana walio katika shule za msingi na sekondari, wapende masomo ya Sayansi," alisema Dk. Lwidiko.

Waliopewa tuzo ni Nancy Iraba, anayefanya utafiti wa Sayansi ya baharini, Diana Machuve, ambaye ni Mhadhiri Msaidizi Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, Ofisa Kilimo Jiji la Dodoma, Agnes Woisso, Mhadhiri Msaidizi Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Theofrida Maginga, Mtafiti katika Chuo Kikuu cha Nelson Mandela, Risala Mureth.

Dk. Lwidiko aliwataja wengine kuwa ni Neema Mduma, mwanafunzi anayesoma Shahada ya Uzamivu wa Sayansi ya Mawasiliano na Profesa Verdiana Masanja, alipewa tuzo ya kuwa mbobezi katika somo la Hisabati ambaye alikuwa mkuu wa idara wa kwanza mwanamke katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Naye Makamu Mkuu wa NM-AIST, Prof. Emmanuel Luoga, alisema masomo ya Sayansi ni eneo muhimu la kuwajenga vijana kuwa wabunifu, katika maeneo mengi ya kisayansi kwa kutatua changamoto zinazoikabili jamii.

"Hatuna budi kujielekeza katika Sayansi, maana sasa taifa linapozungumzia uchumi wa viwanda ni muhimu tukawekeza kwa vijana wa kike na kiume kupenda na kusoma masomo hayo kwa wingi zaidi bila kufanya hivyo tutajikuta nchi yetu inakua na wahitimu wa fani ya wanasheria, maofisa rasilimali watu na wahasibu, ambao kama viwanda havifunguliwi watakosa mahali pa kufanya kazi," alisema Prof. Luoga.

Neema Mduma ambaye ni mmoja wa waliotunukiwa, alisema kupitia tuzo hiyo anawahamasisha vijana wa kike kuwa masomo ya Sayansi sio magumu kama watu wengi wanavyodhani, kwa kuwa wanawake waliopo kwenye Sayansi wamefanya mambo makubwa katika jamii.





# Shirika laruhusiwa miradi ya kijamii

**Na Na Mwandishi Wetu,** SAME

SERIKALI imekubali Shirika la World Expedition Exchange kuanza utekelezaji wa miradi yake ya kijamii katika Wilaya ya Same kuanzia mwanzoni mwa mwaka ujao.

Shirika hilo lenye maskani yake nchini Uingereza ni kama linakwenda kufufua matumaini ya serikali ya Wilaya ya Same ya kukuza na kuvitangaza vivutio vyake vya utalii, baada ya kukubali kuja kuwekeza katika sekta hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema shirika hilo linaruhusiwa sasa kuanza uwekezaji.

Alisema kabla ya kuja rasmi, shirika hilo kwa sasa limeanza kugawa vitabu vya masomo ya Sayansi kwa Shule za Msingi na Sekondari za Kata ya Mshewa ili kuunga mkono juhudi za serikali katika utaoji wa elimu bora na yenye ushindani kimataifa.

"Hivyo vitabu vilivyoletwa na Shirika la World Expedition Exchange, ndivyo ambavyo vimewezesha kuanzishwa kwa maktaba hiyo katika kijiji hicho cha Goma. Wametoa maelekezo kwamba vitumiwe na wanafunzi wa Kata ya Mshewa ili kuongeza maarifa.

"Utalii wa asili, ndio ambao umelivuta hilo shirika na kuamua kuja kuwekeza hapa kwetu siku za usoni, lakini kimsingi tayari wamekubali pia kufadhili ujenzi wa maktaba ya kwanza ya utalii, hasa ukizingatia kuwa suala la kukuza utalii wa asili ni moja ya malengo yaliyopo kwenye mpango mkakati wa kukuza utalii wilayani Same."

Mkakati huo, unaelezwa kwamba umeanza kuvutia watalii wengi kutoka mataifa ya kigeni kutembelea vivutio vya asili, maporomoko ya maji, mapango, mashamba, mabwawa, misitu, milima na vingine.

Senyamule alitoa wito kwa wananchi kujifunza na kushiriki shughuli za utalii akisema, katika mpango mkakati wa utalii, Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na Msitu wa Chome wenye kilele cha Shengena, wilaya imepanga kuunganisha vivutio hivyo pamoja na vivutio vya utamaduni ili serikali na wananchi wote wafaidike na kukuza uchumi wa wilaya.

Awali, mmoja wa wafanyabiashara aliyewaleta maofisa hao wa shirika hilo la Uingereza, Elly Kimbwereza, ameeleza mtazamo wake wa namna utalii wa asili unavyoweza kuunganishwa na shughuli za jamii na kuleta maendeleo ya haraka, kwani watalii wengine wameshashiriki kutengeneza barabara katika kijiji hicho.

# Mwenyekiti CCM awashangaa wanaodai hakuna demokrasia

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) mkoa wa Kilimanjaro, Ivan Moshi, amesema dunia inawashangaa wanasiasa ambao wanadai hakuna demokrasia nchini.

Badala yake, amewashauri wanasiasa wa vyama vya upinzani wanaoichafua Tanzania katika sura ya kimataifa kuacha mara moja na kulipigania taifa kufikia ndoto zake za uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

Alikuwa akizungumza jana wilayani hapa, baada ya kumalizika zoezi la upandaji wa miti na kuwajulia hali wagonjwa katika Hospitali ya Wilaya ya Siha.

"Watu wanaodai hakuna demokrasia nchini wapuuzwe na mimi nataka niwape ushauri hata kama kiumri mimi ni mdogo, acheni ushamba wa kuichafua nchi na njooni muunge mkono Rais Dk. John Magufuli anayepambana kila uchao kuiondoa nchi katika umaskini na kuwaletea maendeleo wananchi wake, " alisema Moshi.

Moshi alisema baadhi ya watu wanadai kuwa hakuna mahusiano ya moja kwa moja ya uhuru wa mawazo na uminywaji wa demokrasia katika nchi, naomba niseme hili jambo halina ukweli na limejaa upotoshwaji mkubwa.

Alisema Watanzania wanao uhuru wa kuzungumza na vyama vya siasa vimepewa fursa ya kukosoa na tunaona serikali inawajibika.

Zaidi Moshi aliongeza: "Watu hao ni wa kuwapuuza na kuendelea kuunga mkono juhudi za Rais Dk. John Magufuli ya kuwaletea maendeleo wananchi, hatutaki demokrasia ya kuturudisha nyuma kimaendeleo."

Kwa upande wake, Katibu wa UVCCM wa Wilaya ya Siha, Bulugu Magige, alieleza kufurahishwa kwake na jitihada zinazofanywa na Rais Magufuli katika kuwaletea wananchi maendeleo katika nyanja mbalimbali ikiwamo kufufua treni ya abiria na mizigo katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini hasa mkoa wa Kilimanjaro.

Naye Frank Rwechuchugura ambaye ni Ofisa Afya wa Wilaya ya Siha, aliwashukuru vijana hao kwa kutembelea wagonjwa na kuwapa zawadi, kufanya usafi na pia kupanda miti zaidi ya 200 katika hospitali hiyo.



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Babati, mkoani Manyara, Sajenti Joachim Katindasa, akitoa elimu ya kutumia kizima moto cha awali kinachobebeka kwa askari wa jeshi la akiba wa Kijiji cha Kiongozi, Kata ya Maisaka. **PICHA: GIFT THADEY**

# Shule Same yapata ufadhili miundombinu

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

HALI mbaya ya miundombinu ya Shule ya Msingi Ishinde iliyopo Wilaya ya Same, ambayo ilikuwa hatarini kufungwa kutokana na uchakavu wa madarasa, imepata wafadhili waliokubali kurejesha hadhi ya majengo yake.

Wafadhili hao ambao ni wanafunzi waliowahi kusoma shuleni hapo, wamejitolea kukarabati madarasa saba na ofisi mbili za walimu kwa gharama ya Sh. milioni 18.

Akitoa taarifa kuhusu ufadhili huo, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Gilbert Semgonja, alisema awali hali ya madarasa katika shule hiyo ilikuwa mbaya kiasi cha kuonekana kama magofu.

Alisema kabla ya kupatikana kwa wafadhili hao na kuanza kazi ya ukarabati, kuta za madarasa zilikuwa zimepasuka nyufa na kusababisha idadi kubwa ya wanafunzi kuacha shule.

"Kwa sasa baada ya vijana hao kukarabati na kutunza mazingira ya shule hii kwa kupanda miti ya matunda na kivuli, uwezekano wa idadi ya wanafunzi kuongezeka ni mkubwa na tutaongeza kiwango cha ufaulu kutokana na mazingira ya shule kuwa rafiki kwa wanafunzi na walimu," alisema Semgonja.

Alipotafutwa msimamizi wa mradi huo wa ukarabati wa shule, Mkurugenzi wa Taasisi ya Vijana Ishinde, Noel Kipesha, alisema baada ya kuona hali ya shule hiyo inazidi kuwa mbaya na kuhatarisha usalama wa wanafunzi, yeye na wenzake walilazimika kuanza kutafuta fedha na wafadhili ili kunusuru wanafunzi hao.

"Tulihofia kwamba wanafunzi wanaosoma katika madarasa hayo wanaweza kuangukiwa na kuta za madarasa, ndio maana tukatafutana na kuchangishana fedha mpaka tukapata Sh. milioni 18 na tukafanya kazi hiyo na sasa tumekabidhi majengo yakiwa nadhifu," alisema Kipesha.

Kaimu Ofisa Elimu Msingi wa Wilaya ya Same, Niwaeli Kajia, akizungumzia ukarabati huo aliwapongeza vijana hao kwa jitihada walizozifanya kunusuru majengo ya shule hiyo kuendelea kuharibika zaidi kutokana na kukosa ukarabati kwa muda mrefu.

# Ushirikiano wa kisiasa mlango wa maridhiano

**Na Sabato Kasika**

NOVEMBA mwaka 2015, Rais John Magufuli, alilihutubia taifa wakati akifungua rasmi Bunge la 11, ikiwa wiki chache baada ya kuapishwa kuiongoza serikali . Ni baada ya kushinda uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 uliokuwa na wagombea wengi na ushindani mkali kutoka ndani ya CCM na pia kwa wapinzani.

Waliochuana naye walikuwa Anna Mghwira wa ACT Wazalendo, Edward Lowassa-Chadema, Hashimu Rungwe- Chauma na Maximilian Lyimo wa TLP.

Hata hivyo, wakati Rais Magufuli, akilihutubia bunge, wapinzani walianza chokochoko na kuanza kufanya vurugu, kupiga kelele na kuzomea hali iliyomlazimu Spika Job Ndugai kuwatoa ndani ya ukumbi huo.

Rais alihutubia bunge ili kutimiza matakwa ya ibara ya 91 ibara ndogo ya kwanza ya katiba inayomtaka kulihutubia na kulifungua rasmi bunge hilo.

katika salamu zake aliwapongeza wabunge wote kwa kuchaguliwa kuwa wabunge na kuwapongeza pia wale wote waliochaguliwa katika nafasi za udiwani kwenye kata mbalimbali kote nchini.

Katika hotuba yake, Rais aliwaeleza wabunge kuwa kulikuwa na ushindani katika uchaguzi wa mwaka huo kuanzia ndani ya vyama na baadaye kwenye uchaguzi mkuu uliohusisha na kushindanisha wagombea toka vyama tofauti.

Miongoni mwa mambo aliyozungumzia, katika hotuba yake ni kwamba CCM, imejengwa, katika misingi ya kukataa rushwa na ufisadi, kuwa ni moja ya imani kuu za CCM ni ile isemayo: "Rushwa ni adui wa haki, sitatoa wala kupokea rushwa"



Viongozi wa upinzani Mwenyekiti wa Chadema Mbowe (wa pili kushoto), James Mbatia wa NCCR-Mageuzi na Seif Shariff Hamad kutoka ACT Wazalendo (kulia). **PICHA: MTANDAO.**

Kwamba kwa Mtanzania mwaminifu kwa imani yake hatakuwa na kigugumizi, bali atakuwa mstari wa mbele kwenye mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi.

Aliahidi kuchukua hatua hiyo, kwa vile mmoja wa waasisi wa taifa hili Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliwahi kuifananisha rushwa na ufisadi 'kama adui mkubwa wa watu'.

"Rushwa na ufisadi havina budi kushughulikiwa bila huruma kwa sababu naamini wakati wa amani rushwa na ufisadi ni adui mkubwa kwa ustawi wa watu kuliko vita," Rais Magufuli akasema.

Tangu atoe hotuba hiyo iliyosusiwa na baadhi ya vyama vya upinzani, Watanzania wanashuhudia jinsi ambavyo anapambana na rushwa na kila aina ya ufisadi kwenye sekta ya umma na binafsi ili kila Mtanzania afaidi keki ya taifa.

Ni muhimu kukifahamu kilichofanyika bungeni, lengo likiwa ni kutaka kutizama Zaidi kususia mambo ya kitaifa yaliyofanywa na baadhi ya vyama vya upinzani uliofanywa kuanzia kuapishwa kwake hadi wakati anahutubia bunge.

### KUSAKA MARIDHIANO

Kilichoonekana Mwanza juzi wakati wa maadhimisho ya miaka 58 ya Uhuru kinaonyesha kuwa vyama vya siasa vinasaka maridhiano ya kisiasa ikiwa ni takribani miaka mine tangu kutokea kwa tukio hilo la kususia, ambalo kimsingi halina afya kwa maslahi ya taifa.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kilikuwa hakijashiriki katika sherehe za uhuru tangu Rais Magufuli alipoapishwa mwezi Oktoba mwaka 2015.

Lakini kwa mara ya kwanza, katika sherehe za miaka 58 ya uhuru, zilizofanyika kitaifa, jijini Mwanza, chama hicho kilishiriki huku mwenyekiti Freeman Mbowe akiongoza ujumbe wa viongozi waandamizi.

Hatua ya chama hicho kushiriki sherehe hizo, ilitokana na mashauriano ya muda mrefu ya ndani na nje ya chama, na hatimaye kufikia uamuzi huo, ambao kimsingi ni wa kiungwana.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano Chadema, Tumaini Makene, anasema, Kamati Kuu iliazimia chama kushiriki kwenye maadhimisho ya kumbukumbu ya Uhuru wa Tanganyika.

Kwamba iliazimia kwa kauli moja kuwa Mbowe, aongoze ujumbe wa baadhi ya viongozi wakuu na waandamizi kuwakilisha chama katika maadhimisho hayo na kuhamasisha wanachama kujitokeza kwa wingi.

Chama hicho hakikuishia kwa wanachama tu bali kilihimiza pia Watanzania wengine wa maeneo ya jirani na Mwanza, washiriki kwenye maadhimisho hayo, ambayo hufanyika Desemba 9 ya kila mwaka.

### UMUHIMU WA KUSHIRIKI

Hatua hiyo inaonyesha ukomavu wa kisiasa na kama itaendelea inaweza kusaidia kumaliza sintofahamu, ambayo imekuwapo ikianzia kususia sherehe za kuapishwa kwa Rais John Magufuli.

Kimsingi nchi ni muhimu kuliko vyama vya siasa, hivyo umoja wa kitaifa inapaswa kuwekwa mbele badala ya kutenganishwa na itikadi za kisiasa za kusababisha kususia mambo ya muhimu yanayounganisha Watanzania.

Ni muhimu kutambua kuwa maridhiano ndiyo njia pekee ya kuweka kumaliza mkwamo wowote, ambao unaweza kujitokeza badala ya kususa mambo muhimu ya historia ya nchi kama sherehe za uhuru.

Wanasiasa watambue kuwa malumbano hayajengi, hivyo tofauti za kisiasa ziachwe na zisiwagawe Watanzania, kwani vyama vya siasa huja na kupita, lakini nchi itaendelea kuwapo.

Kitendo cha Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe kwenda kwenye sherehe hizo na kumuomba maridhiano kwa Rais Magufuli ni cha kiungwana kuliko kukaa pembeni au kususa na kulalamika.

"Nimekuja kushiriki sherehe za miaka 58 ya Uhuru kama uthibitisho wa ulazima wa kuwepo maridhiano, kuwepo upendo, na kuwapo mshikamano katika Taifa letu," ndivyo anavyosema Mbowe.

Ukweli ni kwamba mara nyingi meza ya mazungumzo huwa inasaidia kupata maridhiano kuliko kukaa pembeni na kulalamika au kususa kama, ambavyo kwa muda mrefu Chadema ilisusa sherehe hizo.

Kitendo cha viongozi wa upinzani kutoa wito wa kuwapo maridhiano ya kisiasa mbele ya Rais John Magufuli, ninaweza kusema kuwa ni dalili ya kufunguliwa kwa ukurasa mpya wa siasa za maridhiano.

Siasa hizo ndizo ambazo zinaweza kujenga umoja wa kitaifa, kwa kutanguliza maslahi ya nchi kwanza badala ya vyama, hasa kwa kutambua kuwa vyama vya siasa vinapita, lakini Tanzania itaendelea kuwapo hadi ukamilifu wa dahari.

Hatua ya viongozi wa vyama vya siasa kuomba maridhiano ya kisiasa, kama nilivyosema ni dalili tosha kuwa sasa siasa za kususa au kulumbana zinaelekea kuzikwa na kufungua ukarasa mpya wenye demokrasia.

> "Nimekuja kushiriki sherehe za miaka 58 ya Uhuru kama uthibitisho wa ulazima wa kuwepo maridhiano, upendo, na mshikamano katika taifa letu,"



Mbowe akitoa salamu kwa wananchi wakati wa maadhimisho ya miaka 58 ya Uhuru jijini Mwanza Jumatatu wiki hii. **PICHA: MTANDAO.**

## MIAKA 58 YA UHURU WA NCHI

# Kuadhimisha kuna maana gani leo?



Mwenyekiti wa ACT- Wazalendo, Zitto Kabwe. **PICHA: MTANDAO**

**Na Zitto Kabwe**

DESEMBA 9, 1961 Tanganyika iliingia katika jumuiya ya mataifa huru duniani baada ya kupata uhuru wake kutoka mkoloni wa Uingereza.

Muda mfupi baadaye Tanganyika ikawa mwanachama wa Umoja wa Mataifa. Safari ya kwanza ya nje ya nchi ya Mwalimu Julius Nyerere kama Mkuu wa Serikali ilikuwa tarehe 14 Desemba 1961 kwenda New York kwa ajili ya kupokea uanachama wa Tanganyika katika Umoja wa Mataifa (UN).

Siku ya Uhuru Mwalimu Nyerere alitoa hotuba fupi sana ya kupokea 'instruments of independence' kutoka kwa mwakilishi wa Malkia wa Uingereza.

Kabla ya hapo, akiwa Rais wa TANU, alitoa salamu za Uhuru, pamoja na mambo mengine alieleza maana ya Uhuru ambao Watanganyika waliupigania.

Aliwakumbusha wanachama wa TANU kuwa " muda wote ambao tumekuwa tukipambana kupata Uhuru wa nchi yetu, tuliweka msingi kuwa imani yetu ni usawa na heshima ya utu kwa watu wote na kuheshimu tangazo la haki za binaadamu".

Alisisitiza kwa wana TANU kuwa, "hakuna rangi, dini, kabila, au kingine chochote kile kinachoweza kumwondolea mtu haki yake ya kuwa sawa mbele ya jamii yake".

Aliwaambia wana TANU kuwa ni lazima kuendelea kupambana na " umaskini, ujinga na maradhi" ili kujenga jamii ya watu waliosawa na huru.

Katika mazingira ya sasa unaweza kusema kuwa hata kuwa mwanachama wa chama cha siasa tofauti na kilichopo madarakani hakuwezi kukuondolea haki yako kama Mtanzania mwingine yeyote.

Hii ndiyo maana ya Uhuru ambao waasisi wa nchi hii waliuamini.

**MAANA HALISI**

Hata hivyo, utapata maana ya Uhuru kwa wazee wetu kwa mapana zaidi katika Hotuba ya Mwalimu Nyerere ya Desemba 10, 1962 wakati anahutubia taifa kama Rais wa Jamhuri ya Tanganyika.

Ikumbukwe Mwalimu alijiuzulu Uwaziri Mkuu na kutumia mwaka mzima kujenga TANU kabla ya kuchaguliwa kuwa Rais wa Tanganyika. Katika hotuba hiyo ambayo pengine inapaswa kusomwa na kila Mtanzania kuanzia viongozi wakuu mpaka mwananchi wa kawaida, Mwalimu Nyerere anaeleza maana ya Uhuru ambao waliupigania yeye pamoja na wenzake .

Wapigania uhuru hao akiwamo Hamza Mwapachu, AbdulWahid Sykes na wadogo zake, Denis Phombeah, Oscar Kambona, Rashidi Kawawa, Dossa Aziz, John Rupia, Titi Mohammed, Andrew Tibandebage, Vedastus Kyaruzi, Steven Mhando na wengine wengi ambao kwa hakika hatuwathamini wala kuwaenzi kama taifa.

Sina hakika kama kuna mtaa au barabara iliyopewa jina la kama Hamza Mwapachu au Vedastus Kyaruzi kuenzi uasisi wao wa taifa letu.

Katika Hotuba hii ya 10/12/1962 Mwalimu Nyerere alisema "Uhuru tulioupigania sio tu uhuru dhidi ya mkoloni, tulitaka uhuru wa watu wetu binafsi kufanya mambo yao na kujitafutia kipato chao kwa ajili ya maisha yao yenye utu". Aliendelea kusema "tunataka kila raia awe sawa na mwingine na hakuna ubaguzi wowote". Maneno haya ya Mwalimu yanaweza kutafsiri maana ya Uhuru kwa uendelevu kwani ni rahisi kupima kama kila mwananchi ana haki sawa mbele ya jamii, hasa bila kujali itikadi za kisiasa.

> "Katika Hotuba hii ya 10/12/1962 Mwalimu Nyerere alisema "Uhuru tulioupigania sio tu uhuru dhidi ya mkoloni, tulitaka uhuru wa watu wetu binafsi kufanya mambo yao na kujitafutia kipato chao kwa ajili ya maisha yao yenye utu". Aliendelea kusema



Mwalimu Nyerere akiwa na viongozi wa kikoloni wakishuhudia kushushwa bendera ya Mwingireza na kupandishwa ya Tanganyika. **PICHA: MTANDAO.**

Lakini leo, tafsiri hii ya Uhuru ina maana gani sasa? Watanzania wa leo, ( baada ya nchi mbili zenye hadhi sawa mbele ya sheria ya kimataifa kuungana ambazo ni Tanganyika na Zanzibar, wana tafsiri Uhuru sawa na Watanzania wa miaka ya 1960?)

Takwimu rasmi za serikali zinaonyesha kuwa ni asilimia tatu ya Watanzania wanaoishi walikuwepo mwaka 1961 wakati Tanganyika inapata Uhuru.

Watanzania wengi, asilimia 71 hawakuwa wamezaliwa mwaka 1995 wakati wa uchaguzi wa kwanza chini ya Demokrasia ya Vyama vingi.

Asilimia 65 ya Watanzania wanaoishi sasa wala hawakuwahi kumwona Mwalimu Nyerere , kwa Watanzania hawa, Uhuru wa Tanganyika una maana gani kwao?

Ni uhuru wa kumtoa mkoloni na kupandisha bendera ya Tanganyika tu au ni uhuru wa kuondokana na umasikini, ujinga na maradhi?

Kuna baadhi ya watu wanajenga hoja kuwa uhuru wetu ni kujenga nchi na kujiletea maendeleo kama kujenga miundombinu ya barabara, reli, madaraja na shule.

Lakini mkoloni alifanya haya Mjerumani alijenga reli ya kati kutoka Pwani mpaka bara (Dar es Salaam - Kigoma na kutoka Tanga mpaka Dar es Salaam.

Mwingereza akamalizia mpaka Mwanza na kuifikisha Moshi na Arusha. Wakoloni walijenga shule barabara mbalimbali na hospitali. Lakini haya 'maendeleo' aliyoleta mkoloni hayakuwafanya wazee wetu waseme "sasa Uhuru wa nini wakati barabara zimejengwa, shule zipo na hata reli zimejengwa".

Wazee wetu walitaka uhuru wa wananchi kujiamulia wenyewe mambo yao. Uhuru wa maoni na wa kuendesha maisha yao. Kina Nyerere na Hamza Mwapachu hawakujali miundombinu inayojengwa kwani wao walitaka kujenga taifa ndiyo Tanzania iliyoungana na Zanzibar.

Mwalimu Nyerere alisema hili vizuri wakati wa hotuba ile ya 10 Desemba, 1962. Aliwaambia Watanganyika "kujenga nchi sio kujenga barabara za lami, majengo makubwa na hoteli za kifahari. Nchi inaweza kuwa na hayo yote lakini isiheshimike. Kujenga taifa ni kujenga watu".

Wazee wetu hawa walijaribu kweli kujenga taifa kwa kujenga watu. Tanganyika na baadaye Tanzania ilikuwa inaheshimika duniani si kwa sababu ya utajiri wake wa madini bali kwa utu wa watu wake, tabia za watu wake na misingi imara ya kutetea haki za watu waliokuwa wanaonewa.

Uhuru waweza kuwa na maana tofauti kabisa kwa asilimia 71 ya Watanzania ambao wamezaliwa baada ya mwaka 1995. Uhuru kwao ni dhidi ya umasikini, kulisha familia zao na kuepukana na njaa.

Kwa mujibu wa Benki ya Dunia, asilimia 49 ya Watanzania wanaishi kwenye dimbwi la umaskini kwani hawana uwezo wa kutumia Sh. 5,000 kwa siku (Dola mbili).

Iwapo kuna miaka 58 ya Uhuru lakini nusu ya wananchi wanakabiliwa na tatizo la kula mlo mmoja kwa siku Uhuru una maana gani? Zinahitajika juhudi zaidi ili uhuru uwe na maana zaidi kwao.

Wenzetu ambao tulipata Uhuru wakati mmoja, kama Malaysia, ni asilimia tatu ya watu wao wanaitwa masikini.

Uhuru kwa asilimia 71 ya Watanzania ni Uhuru wa usalama wao. Kwamba waweze kuishi bila kuogopa kuwa na amani na kufanyakazi zao.

Utafiti uliofanywa Twaweza unaonyesha kuwa asilimia 54 ya wananchi, pamoja na mambo mengine, wanaumizwa sana na ukosefu wa ajira. Hii ina maana kuwa kwa Watanzania wa sasa Uhuru kwao maana yake ni kuwa na ajira, kuwa na haki ya uhuru wa mawazo na kuwa na haki ya uhuru wa usalama.

Ni dhahiri kuwa maana ya Uhuru kwa Watanganyika wa miaka ya 1960 ni tofauti na ile ya Watanzania wa kizazi cha demokrasia ambao wanachotaka ni kujipatia ajira watakayo, kupata na kutoa habari na uhuru dhidi ya umaskini na changamoto za kijamii na kiuchumi.

# Miaka 10 nchi kujitawala, Nyerere aliwarejeshea majibu waliodhihaki

**INATOKA UK.13**



Kutoka kushoto, Aboud Jumbe Mwinyi, Rashid Mfaume Kawawa na Chifu Adam Sapi Mkwawa, walipokuwa katika mafunzo ya JKT, mwaka 1968.

ya taifa huru, ndipo alipotoa hotuba ndefu yenye kuainisha simulizi za mavuno kutoka Tanzania huru.

Alienda mbali katika sherehe hiyo akiwataka wote walioubeza uhuru wakitamka 'hawatajiweza' sasa aliwataka waje kushuhudia kilichojengwa.

Bendi za muziki zilizoshamiri nchini wakati huo ikiwa burudani kubwa ya Watanzania, baadhi kama Morogoro Jazz na Nuta Jazz hazikuwa nyuma kuziundia tungo kufikisha ujumbe.

Mikakati ya maendeleo nchini chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere alitimiza kupitia mtazamo mkuu, ambayo ni kuwa na jamiii huru inayojikwamua kiuchumi, kifikra, kimazingira, kimkakati na kitalaamu ndani ya siasa huru.

Mwanzo wa safari ya Tanzania huru, ilianza na kuwapo siasa zinazofunikwa na falsafa za Ujamaa wa Kitanzania chini ya kaulimbiu iliyobuniwa baadaye "Ujamaa na Kujitegemea ndio njia sahihi ya kujenga jamii iliyo sawa na huru."

Waziri Mkuu Julius Nyerere, akiegemea dhana siasa ndio inayohodhi mwelekeo wa serikali, muda mfupi baadaye alijiengua serkalini na akarudi kwa muda katika chama tawala TANU. Alimuachia majukumu 'pacha' aliyedumu naye kiutendaji, Rashid Kawawa.

Mwisho wa mwaka 1962, Nyerere alirudia nafasi yake serikalini ikiwa na mabadiliko ya kikatiba kutoka Waziri Mkuu hadi Rais. Cheo cha awali kikawa na jukumu jipya la mtendaji mkuu wa shughuli za kiserikali, chini ya Rais. Taifa nalo lilivuka kuwa Jamhuri ya Tanganyika.

Kuanzia mara tu ulipopatikana uhuru hadi mwaka 1964, serikali iliunda Mpango wa Maendeleo wa muda mfupi wa kuhuisha nchi na watu wake kimaendeleo, pia ikatengeneza mwelekeo wa taifa jipya kuleta mageuzi ya haraka katika mfumo wa kumiliki rasilimali zake.

Mfano mmojawapo ni jijini Dar es Salaam, shule nyingi za matabaka ya Kihindi na Kizungu, sasa ziligeuzwa kuwa za umma. Hapo zinatajwa shule kama Kibasila ambayo ilikuwa wahindi Wagoha kwa jina la St. Xavier na sekondari za wasichana; Zanaki na Kisutu, katikati ya jiji la Dar es Salaam, huduma hiyo ikipatikana bila ya malipo, kama ilivyo leo katika ngazi ya msingi, hadi kidato cha nne.

Ikumbukwe katika zama za ukoloni, mfumo wa kielimu uligawanywa katika makundi makuu matatu; Wazungu walipewa fursa zaidi, wakifuatiwa na Wahindi, kisha Waafrika waliokuwa na nafasi kidogo na za chini.

**MAZITO YA 1964**

Ni mwaka uliobeba historia kubwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Tanganyika na Zanzibar kuungana, kisha rasmi Tanzania kuwa na siasa ya mfumo wa chama kimoja na kuzaliwa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

Kikubwa katika mwaka huo kiuchumi, ni mpango wa kwanza mkuu wa maendeleo ya nchi, 1964 hadi 1969, uliounda mwelekeo wa maendeleo ya kuondoka na uchumi na nyendo za maendeleo tegemezi.

Ni mpango, ambao hadi sasa nyendo na falsafa zake ndizo zinazotawala mwelekeo wa kulijenga taifa katika uchumi na maendeleo mengi ndani ya mazingira ya leo.

Wakati huo kuanzia mwaka 1964, Tanzania iliazimia kujiengua kupitia mpango huo wa miaka mitano, kutoka dira ya uchumi wa kikoloni ya "tunazalisha tusichokitumia na kutumia tusichokizalisha." Hiyo maana yake ni nini?

> Wazalishaji pamba walivaa nguo za kigeni, vivyo hivyo wa wafugaji walivaa viatu vya ngozi vya kigeni. Mpango wa Maendeleo uliweka mkakati kufuta hilo la "kutumia tusichokizalisha na kuzalisha tusichokitumia

Sekta kama kilimo iliyoajiri zaidi ya asilimia 90 ya Watanzania na ikawa mzizi wa uchumi nchini, ilikuwa wakala wa kuzalisha malighafi kwa viwanda vya nje na ndio ulikuwa msingi mmojawapo wa kuwapo ukoloni.

Wazalishaji pamba walivaa nguo za kigeni, vivyo hivyo wa wafugaji walivaa viatu vya ngozi vya kigeni. Mpango wa Maendeleo uliweka mkakati kufuta hilo la "kutumia tusichokizalisha na kuzalisha tusichokitumia."

Mambo yaliposhamiri katika mikoa kama Morogoro, Mara, Mwanza, Shinyanga na Tabora, kulishuhudiwa ujenzi wa viwanda vingi ambavyo ni wateja wakuu wa malighafi hayo kutoka shambani.

Hapo vinatajwa viwanda vya nguo kama Mutex (Musoma), Tabotex (Tabora), Mwatex (Mwanza). Dar es Salaam zikawepo Urafiki na Kiltex, huku mkoa wa Tanga ukijidai na bidhaa ya katani na viwanda vyake.

Mpango uliweka mkakati katika mfumo wa uzalishaji uwe ambao unaegemea zaidi nguvukazi ya watu (labour production) kuliko mashine zaidi (capital intensive) na ndivyo viwanda vingi vilivyojengwa, kufuata utaratibu huo.

Ndani ya mwaka 1967, mageuzi makubwa yalishashuhudiwa katika mfumuko wa viwanda, ikiwamo kiwanda cha Urafiki (Friendship Textile Mills) kwa ufadhili wa China, ambacho kilikuwa na wafanyakazi waliotapakaa jiji zima.

Hata hivyo, kabla mwaka 1966 kuna mageuzi, ilizaliwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), baada ya kujiengua kutoka chombo cha Afrika Mashariki na kuanza kufanya kazi kisheria.

Mwaka huo huo, ndio ambao una chimbuko la mzizi wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na utaratibu wa kuchukua vijana wanaomaliza masomo kujiunga nalo kwa mujibu wa sheria.

Ni utaratibu uliodumu uliowahusu wahitimu wa kidato cha nne waliopitia mafunzo yasiyopungua mwaka mmoja, mathalan kidato cha tano na sita vyuo. Ni utaratibu uliodumu hadi mwaka 1992, ndipo ukaanza kulega.

Pia, wapo waliohudhuria mafunzo hayo kwa misingi ya kujitolea. Mwaka 1968, baadhi ya viongozi walihudhuria mafunzo ya JKT, akiwamo Waziri Mkuu, Rashid Kawawa, Spika wa Bunge Adam Sapi Mkwawa na aliyewahi kuwa Rais wa Zanzibar, Aboud Jumbe Mwinyi.

Ni chombo ambacho kilileta mageuzi ya ukomavu kifikra, umoja na uzalendo unaoenziwa hadi leo, mfano hai ni vijana waliopitia JKT kambi ya Mgambo Tanga, wameunda umoja wao kuenzi na hata kumna wakati walipotembelea baada ya wastani wa miaka 30 waliokuwapo huko.

Mifumo wa huduma wezeshi nayo katika kipindi cha mipango ya miaka hiyo mitano, iliimarishwa kuwaweka sawa wananchi wasiyumbe katika harakati za maendeleo.

Hadi katikati miaka ya 1960, ziljengwa zahanati nne jijini, Dar es Salaam, Temeke, Mnazi Mmoja, Amana na Mwananyamala, ambazo ni huduma wezeshi kwa maendeleo ya umma. Kwa sasa zote ni hospitali za Rufani, isipokuwa Mnazi Mmoja.



Mzee Rashid Kawawa, alipoenda ziarani ugaibuni.

Ni njia zilezile ambazo leo zinapitiwa katika ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali chini ya uangalizi wa Ofisi ya Rais (Tamisemi) na mwongozo wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) wa mwaka 2007 na ukaanza kufanya kazi 2008.

Katika elimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kilichoanza sambamba na uhuru mwaka 1961, kwa kitivo cha sheria katika Mtaa wa Lumumba, Mnazi Mmoja, Dar es Salaam, mwaka 1964, ilikuwa na upanuzi mkubwa kuhamia , iliko sasa eneo la Mlimani, ikiongeza vitivo viwili; Sanaa na Sayansi.

Masuala ya uongozi na biashara ilichukuliwa hatua zake, kupitia mfumo wa elimu. Mwaka 1965, kilianzishwa Chuo cha Uongozi wa Maendeleo (IDM), Mzumbe na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), lengo ni kupanua wigo wa taaluma na wataalamu wa serikali katika kipindi hicho, ambacho walikuwa wachache sana.

Ni zama athari za ukoloni bado zilikuwapo, kwa upungufu wa wataalamu serikalini hata kulazimika kupeleka baadhi ya vijana wake nje ya nchi kupata taaluma, ikiwamo katika fani za uhasibu, kozi za cheti cha juu ACCA na ACA(kama CPA nchini).

Vivyo vivyo, kukawapo kasi kubwa ya ongeza la shule za msingi na elimu ya watu wazima, ambayo rasmi ilirithi jengo ilkoanzia UDSM Mtaa wa Lumumba.

Sekta kilimo ilitanuliwa kwa kuwapo vyuo vingi vya kunoa wataalamu 'mbawana shamba' kuwahudumia wakulima shambani. Yote yalilenga namna ya kuwajengea uwezo Watanzania, katika harakati za kulijenga taifa lao.

**MAGEUZI YA 1967**

Ni mwaka ambao katika nafasi ya kipekee unakumbukwa kupitia Azimio la Arusha, ambalo ni la kisiasa likiwa tafsiri "tamko rasmi la namna nchi itakavyoendeshwa kupitia siasa ya Ujamaa na Kujitegemea."

Vivyo hivyo 'Ujamaa na Kujitegemea' ikabebeshwa tafsiri kwamba 'ni tamko rasmi la kujenga jamii ya watu walio sawa na huru' wakati Ujamaa ni mfumo wa "Watu kuishi pamoja kufanya kazi kwa pamoja kwa faida ya wote."

Msingi wa Azimio la Arusha unaanzia katika mwongozo wa kisiasa unaopigilia msumari uamuzi wa mwaka 1961, namna ya kuiendesha nchi kiserikali.

Hatua mojawapo ilikuwa kutaifishwa miradi binafsi, ukawa mwanzo wa kuzaliwa mashirika kama Msajili wa Majumba, lililotokana na majengo mengi yaliyotaifishwa kupitia azimio hilo.

Wakati wa kuzaliwa shirika hilo, kulikuwapo Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) lilikuwa la kwanza la umma kuundwa mwaka 1962.Lilijenga makazi mengi hasa mijini nchi nzima. Kwa sasa mashirika hayo yameunganishwa, imebaki NHC.

Inakumbukwa miradi mikubwa ya ujenzi wa makazi nchini kuanzia mwaka 1966, mathalan mamia ya nyumba za makazi jijini Dar es Salaam kwa mikopo ya bei nafuu ya miaka 20, katika maeneo ya Kinondoni, Ubungo, Mwananyamala, Temeke na Magomeni.

Mashirika yaliyotaifishwa yalibadilishwa kuwa ya umma, mfano, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), iliyozaliwa wakati huo. Mashirika hayo ya umma yaliundiwa sheria mpya inayozitafsiri kuwa asasi zote ambao serikali ina asilimia 51 au zaidi.

Pia, kisheria ikaundwa chombo kilichovuma sana, Tume ya Utumishi wa Mashirika ya Umma (SCOPO), hata viwango vyake maarufu 'mishahara ya Scopo.' Watumishi walikuwa na viwango, ikiakisi Azimio la Arusha 'jamii ya watu walio sawa.'

Ni wakati ulipoanza mkakati wa kuundwa mashirika tanzu, kusimamia sekta, mathalan baadaye kukawapo TKAI (Tanzania Karatasi Associated Industries) kusimamia sekta yote ya bidhaa za karatasi.

Wakulima wa bidhaa za nafaka sasa, ziliangukia mikononi mwa Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC), iliyokuwa na vinu na maghala yake kuongezea thamani za bidhaa hizo.

Hadi inatimu mwaka 1969 mwisho wa mpango wa miaka mitano ya maendeleo, mageuzi makubwa yalishashuhudiwa kwa na mfumo wa kujitegemea ukichukua kwa 'kuzalisha tunachokitumia.'

Mwaka 1970, Tanzania ikiwa imeanza kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo (1969 - 1974), liliundwa Shirika la Maendeleo ya Taifa (NDC), iliyobuni kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo kitaifa.

Kimsingi, mpango huo ulifuata zaidi kuboresha kilichopatikana katika awamu iliyopita na kuangalia mipango na miradi inayopiga hatua zaidi.

Mwaka 1970 kupita mwongozo wa TANU kukaagizwa kuanzishwa mabaraza ya wafanyakazi katika sehemu za kazi, ambayo hivi sasa yako kisheria.



Mwalimu Nyerere akimkaribisha jirani yake Mzee Jomo Kenyatta, katika siku ya uhuru. . **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Ushindi wote huo, Mwalimu Nyerere, aliiweka katika sherehe kubwa ya kujivunia, ambayo alifafanua kilichofanikishwa katika sura pana ya maendeleo ya ushindi.

**BAADA MIAKA 10**

Baada ya miaka 10 ya uhuru wa nchi, mipango ya maendeleo iliendelea kushika kasi. Sekta ya Viwanda, ikaboreshwa kuwafika wananchi waoliko katika uzalishaji wa kiwango chao.

Huo ndio ukawa mwanzo wa kuzaliwa Shirika la Maendeeo ya Viwanda Vidogo (Sido) mwaka 1973 na mwaka mmoja kukawepo Azimio la Iringa la mwaka 1972, ambao kimsingi ni namna fulani ya kuendeleza Azimio la Arusha, katika maeneo maalum.

Ni azimio liilokipa kilimo hadhi yake, katika kupanua mashamba na bora, huku Mwalimu Nyerere akihimza na hata mifano ya hotuba zake 'mpunga tunapanda nchi moja moja.'

Mwaka 1974, ilipitishwa kinachojulikana 'oparesheni vijiji' ambavyo vililenga kuwakusanya watu na kuwaletea maendeleo ya pamoja, ambako kulikuwapo miradi mingi ya kuendeleza na kupanua kilimo; watu wanalima katika mashamba aina mbili, ushirika na binafsi.

Vijiji vipya katika mipango kuzungusha Dar es Salama, ni pamoja na Tegetam, Gezaulole na Mwanadilatu, ambako ni mjini.

Kilimo kilisonga kwa kuongozwa na vituo vya ushauri kitalaamu kama Tengeru (Arusha), Maruku (Bukoba) Mlingano (Tanga) na Naliendele - Mtwara

Mwaka 1974, nako kulipitishwa Azimio la Musoma, kiuendeleza dira ya Azimio la Arusha, katika nyanja ya elimu, ambako kuna tafsiri nyingi, ikiwamo elimu ya msingi kwa wote kuendeleza mwongozo wa Umoja wa Mataifa, kuhusu elimu- UPE (Universal Primary Education).

Kuziba pengo hilo, kulikuwapo walimu wahitimu wa elimu ya msingi waliopigwa 'brashi' kupitia vyuo vya walimu.

Jumuiya ya Wazazi ya TANU (Tapa) nayo ilichukua hatua kuanzisha shule nyingi za sekondari binfasi kuchangia kupunguza pengo hilo mwaka1976, nyingi mkondo wake zikifuata sera za nchi, sekondari za ufundi na kilimo.

Hapo unataja shule kama Vituka (Dar e s Salaam), Ovada (Singida), Boza (Pangani), Bagamoyo Tech (Bagamoyo) na Lupata, iliyopo Tukuyu.

Hatua kama hiyo ya ilishafanywa na Baraza Kuu la Waislamu Tanazania, katika kipindi kabla ya tapa, ilioanzisha shule za sekondari kama Kinondoni ya Dar es Salaam, Kibohehe (Moshi) na jumuiya (Tanga)

Elimu kwa wasiobahatika kupata fursa ilisambazwa, kukaanzishwa madarasa ya elimu ya watu wazima, kupitia kaulimbiu 'kisomo chenye manufaa.'

Shule nyingi zilitumika jioni kama madarasa ya elimu kwa watu wazima na walimu wa kujitolea vijijini na mijini, huku watu wakihimizwa watoto waliofikia umri, kupelekwa masomoni.

Kwa waiotaka kujiendeleza zaidi, Taasisi ya Elimu tya Watu Wazima ilikuwa na huduma hiyo hadi elimu ya sekondari.

Haikushangaza Tanzania iling'ara kinara barani Afrika nyuma ya Nigeria katika kuboresha elimu ya msingi na kisomo chenye manufaa.

> 'Ujamaa na Kujitegemea' ikabebeshwa tafsiri kwamba 'ni tamko rasmi la kujenga jamii ya watu walio sawa na huru' wakati Ujamaa ni mfumo wa "Watu kuishi pamoja kufanya kazi kwa pamoja kwa faida ya wote

Ni zama iliyoanzishwa Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), ukiwa mwendelezo wa kutekeleza Azimio Musoma na mwaka huohuo 1975, pia Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu (NBAA), katika zama tayari kuna wataalamu wake walioshaanza kujitokeza.

Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) nacho kilishaanza kazi mwaka 1972 na wataalamu walioenda kutafuta CPA ughaibuni nao walisharudi.

Katika hifadhi ya chakula, mwaka 1974 kuilitokea njaa kubwa nchini kutokana na hali ya hewa, wengi wakikumbuka, serikali ilivyohami wananchi wake.

Hilo lilifanyika kwa kuletwa nchini mahindi ya njano nchini maarufu 'mahindi ya Yanga' yaliyohifadhiwa ambako sasa ni Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam.

Mwaka 1976, ulipitishwa Mpango Maendeleo ya Viwanda wa miaka 20, iliyolenga kujengwa viwanda vya aina zote; viwanda vidogo, vya kati kuzalisha bidhaa za kawaida na viwanda mama vinavyolenga kuzalisha bidhaa za uzalishaji, mfano mashine.

Hata hivyo, ndani ya miaka tisa mpango huo mpya ulikwama, baada ya mabadiliko makubwa ya kisera, kisheria na kisiasa, taifa likiingia katika mfumo huria.

Mashirika ya Umma mengi yalibinafsishwa kwa matarajio ya kuleta tija zaidi yalikwama.

Mfumo wa ubinafsishaji ulioendeshwa kupitia iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC), ulifanyika kwa njia kuu nne; Mosi, ni kuuza hisa zote kwa mashirika yaliyoonekana yana hali mbaya.

Pili, kuuza hisa zinazogawanywa katika sura tatu; mwekezaji, serkali na umma; mwisho ni ubinafsishaji wa watumishi kumiliki mali zao, maarufu kama Mebo (Management by Ownership) kama ilivyo kwa Kiwanda cha Uchapishaji cha Taifa (Kiuta).

Nyingine ilikuwa ukodishaji taasisi kama ilivyokuwa kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC), ambako mwekezaji alionekana 'mbabaishaji' akanyang'anywa mradi, ukarejeshwa serikalini hadi sasa.

# Mzizi wa Nyerere na harakati za uhuru hizi

SIMULIZI ya uhuru wa nchi, ina chimbuko refu lenye mzizi wa kisiasa kuanzia mwaka 1929, wakati mshika usukani mkuu wa baadaye, Mwalimu Julius Nyerere, alikuwa na umri wa miaka saba tu.

Hapo inaanzia mwaka iliopundwa chama Tanzania African Association( TAA), safu ya waasisi ikiwa na majina maarufu nchini: Kleist Sykes, Mzee bin Sudi; Ibrahim Hamis, Zibe Kidasi, Ali Said Mpima, Suleiman Majisu, Raikes Kusi, Rawson Watts, ba Cecil Matola

Ingawa kilikuwa chama cha jamii ya Kiafrika ndani ya ukoloni, lakini utashi wake ulikuwapo katika sura ya kupigania uhuru.

Mwaka 1950, TAA ilimtuma kiongozi wake Abdulwahid Sykes kwenda Nairobi, Kenya kuwasiliana na kiongozi wa chama cha siasa cha Kenya African Union (KAU), Jomo Kenyatta, ili kujenga mawasiliano na chama cha chao.

Mwaka 1951, baada ya mawasiliano hayo, kukaundwa tawi la siasa la TAA, likiwa na wajumbe: Abdulwahid Sykes (Katibu), Sheikh Hassan bin Amir, Hamza Kibwana Mwapachu, Said Chaurembo, Dk. Kyaruzi, John Rupia na Stephen Mhando

Ni katika mweaka huo, Mzee Kenyatta akutana tena na viongozi wa TAA, katika mkutano uliofanyika mjini Arusha, wajumbe wa TAA wakiwa Abdulwahid Kleist Sykes, Dossa Aziz na Stephen Mhando .

Baadaye mwaka uliofuata, 1952, Abdulwahid alichaguliwa kuwa Rais wa TAA na ndipo wakaanzisha mchakato wa kumkaribishaji kijana 'jembe' Mwalimu wa Shule ya Sekondari Pugu, kujiunga na harakati zao na alikubali na akatambulishwa rasmi kwa Abdulwahid na Kasela Bantu.

Hapo ndipo Nyerere, akanzisha utaratibu wa Jumamosi kukutana na akina Dossa Azizi, Ally Sykes, Abdulwahid Sykes, Dustan Omar na Mhando kujadili mustakbali wa nchi ya Tanganyika.

Ni safari aliyoifanya kwa kutumia baiskeli yake, akija kwa siri bila ya mwajiri kujua. Mikutano hiyo ilikuwa ikifanyika ama nyumbani kwa Dossa Azizi Mtaa wa Congo au Mtaa wa Stanley nyumbani kwa Abdulwahid, katikati ya jiji la Dar es Salaam. Hivi sasa Congo ni mtaa maarufu kibiashara.

Alikuwa ni Dossa Azizi, ambaye mara nyingi alikuwa alimrudisha Mwalimu Nyerere kwa gari lake Pugu, wakati huo shule hiyo iliitwa St. Francis College.

Mwaka1953, Mwalimu Nyerere alichaguliwa kuwa Rais wa TAA, wazee wakimpa nguvu kubwa ya kisiasa. Hapo aliacha kazi ya ualimu, kwani ilikuwa sharti la ajira yake, kutojihusisha na siasa.

Wazee waliokuwa nyuma yake ni pamoja na Sheikh Hassan bin Amir, Sheikh Suleiman Takadir, Mzee Mohammed Jumbe Tambaza, Mshume Kiyate na Mwinjuma Mwinyikambi.

Wengine walikuwa Rajab Diwani, Makisi Mbwana, Sheikh Haidar Mwinyimvua na Idd Faiz Mafongo. Aidha walikuwapo Idd Tosiri, Sheikh Mohamed Ramia na Mashado Ramadhani Plantan.

Mnamo Oktoba 10, 1953 Mwalimu Nyerere, Abdulwahid Sykes, Ally Sykes, Dossa Aziz na John Rupia walikutana kujadili namna ya kuibadili TAA kuwa chama kamili cha kisiasa.

Ilipofika mwaka1954, TANU ilianzishwa ikiwa na wajumbe wa mkutano uliojadili kuibadili katiba ya TAA kuwa TANU. Hao ni Abdulwahid Sykes, Julius Nyerere, Tewa Said Tewa, Dossa Aziz, Ally Sykes, Kasela Bantu, , Abubakar Ilanga na Saadan Abdu Kandoro.

Wengine ni Mzee Kitwana, Oscsar Milinga, Patrick Kunambi, Gerimano Pacha, Japhet Kirilo, Makaranga. Joseph Kimalando na John Rupia.

Mkutano wa kuizindua rasmi TANU ulihudhuriwa na wajumbe Nyerere mwenyewe, Abdulwahid Sykes, Ally Sykes, Dossa, Rupia na Kiyate, Mbwana, Tambaza, Juma Waziri, Clement Mtamila, Rajab Diwani, Plantan na Marsha Bilali, Rashid Ally Meli, Frederick Njiliwa, Idd Mafongo, Idd Tulio na Denis Phombeah.

Julius Nyerere alipewa kadi ya TANU namba moja na kadi namba mbili ikaenda kwa Ally Sykes na Abdulwahid akachukua kadi namba tatu, Dossa Azizi namba nne, ya tano Phombeah, Dome Okochi alipata kadi namba sita, Rupia ya saba na Bibi Titi Mohamed kadi namba 16 na Tosiri namba 25.

- ***Makala hii imeandaliwa na Peter Orwa, kwa mujibu wa taarifa za kihistoria.***




Kutoka kushoto, John Rupia, Julius Nyerere, Zuberi Mtemvu. Waliosimama nyuma yao ni BANTU Group, vijana walinzi wa viongozi wa TANU. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> Mwaka1953, Mwalimu Nyerere alichaguliwa kuwa Rais wa TAA, wazee wakimpa nguvu kubwa ya kisiasa. Hapo aliacha kazi ya ualimu, kwani ilikuwa sharti la ajira yake, kutojihusisha na siasa.



# Kwanini Mafia isherehekee miaka 58 ya Uhuru kitofauti?

Na Gaudensia Mngumi



Mkuu wa Wilaya ya Mafia Shaib Nnunduma, akifurahia mafanikio ya makubwa yaliyopatikana Mafia. **PICHA: BEATRICE PHILEMON**

HUWEZI kudhania kuwa watu wengi hasa watumishi wa umma waliofanyakazi Mafia kuanzia Uhuru mwaka 1961 hadi miaka ya hivi karibuni walihofia kufa wakiwa kwenye vituo vya kazi kisiwani humo.

Inawezekana ikiwa ni jambo la ajabu lakini kilichowahofisha ni pale walipofikiria itakuwaje iwapo imetokea wamefia Mafia wanapelekwaje nyumbani kwa mazishi? Aidha, ni kisiwa ambacho kwa miaka takribani 55 ya Uhuru hakikuwahi kuwa na chumba cha kuhifadhi miili. Wala hospitali ya wilaya haikuwahi kutoa huduma ya kuhifadhi miili isiharibike.

Hivyo, inapotokea umefariki ni vigumu kukuhifadhi wala kukusafirisha nyumbani kwako kwa mazishi kwa wakati, kwa sababu hakuna miundombinu wala vyombo vya usafiri vya uhakika kama ndege, anasema Mkuu wa Wilaya Shaib Nnunduma.

Mkuu wa Wilaya aliyekuwa anazungumza na Nipashe kuhusu miaka 58 na Uhuru na hali ya Mafia leo, anaongeza kuwa Mafia kwa miongo zaidi ya mitano ya uhuru, haijawahi kuwa na usafiri wa uhakika kwa na rahisi kwa wananchi si meli , ndege nje ya eneo hili ilikuwa shida sana pale mtu anapokumbuka kuwa ikitokea akafariki dunia ghafla au akipata ajali ama maradhi yanayohitaji huduma za dharura za rufani ilikuwa si rahisi kunusurika.

Nnunduma anasema, hiyo ni hofu ambayo watu wengi walikuwa nayo hasa wanaotoka mikoa ya mbali au maeneo ambayo ilikuwa mwili urudishwe nyumbani kwa mazishi.

### MAFANIKIO MIAKA 58

"Kwangu miaka 58 ya Uhuru siwezi kuizungumza bila kutaja kazi za awamu ya tano ambayo imefungua milango ya Mafia ambayo ilikuwa haijawahi kufunguliwa tangu kisiwa kuumbwa au taifa hili lilipopata uhuru mwaka 1961."

" Nasema haya kwa sababu kwa muda wote hatukuwa na 'mochari' lakini leo ipo. Tofauti na zamani hatuogopi kufa. Tunafanyakazi na tuna Amani."

Mkuu wa Wilaya anasema miaka 58 ya Uhuru kwa Mafia ni ukurasa mpya wa maisha ya wananchi ambao siku zote walikuwa wakisikia kuwa sehemu mbalimbali za Tanzania zina zahanati kila kijiji na kituo cha afya kila kata hilo halikuwepo kwao.

"Mimi nimekuja hapa 2016 wakati maeneo mengi wanazungumzia kituo cha afya cha kata. Hakuna hata kata moja katika nane tulizonazo iliyokuwa na huduma hiyo. Leo tunapoadhimisha miaka 58 tunacho kipo kata ya Kirongwe."

### MAABARA KISASA

"Maabara ya Mafia ilikuwa ni kichekesho niseme haikuwepo. Mwaka wa 58 wa Uhuru tumejengewa maabara ya kisasa kwa gharama ya Sh. milioni 400."

Ni maabara ya kisasa inapima sampuli za magonjwa yote pia wananchi walikabiliwa na tatizo la tiba hasa vipimo vya ultra sound. Kina mama walilazimika kwenda kutafuta huduma hiyo hasa wajawazito lakini leo zipo kwenye hospitali ya wilaya.

> "Kuanzia mwaka 2016 uzalishaji wa korosho umeongezeka kutoka tani nne na sasa tumefikia tani 214 zilizopatikana mwaka 2018."

### PANTONI MAFIA

Mkuu wa Wilaya anasema Mafia itaanza kujidai kwa kuwa na pantoni yake yenye uwezo wa kubeba abiria 200, tani 100 za shehena, magari kadhaa na inatarajiwa kuanza kazi Februari mwakani.

Nnunduma anasema hayo akimnukuu Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, aliyezuru Mafia mapema Novemba mwaka huu na kwamba ujenzi wa kivuko hicho kitakachofanya safari kati ya Nyamisati na Mafia kila siku upo kwenye hatua za ukamilishaji. Anaongeza kuwa wataondokana na matatizo ya usafiri yaliyodumu kwa miaka yote tangu uhuru na kwamba safari itaanzia Dar hadi Nyamkisati kwa barabara na kutoka Nyamisati hadi Mafia kwa pantone, anasema hayo na kumpongeza Rais John Magufuli, kuwa ndiye inayestahili kupokea shukrani hizo za kuifanya Mafia kuwa mahali salama pa kuishi.

### KIDATO CHA 5

"Tangu uhuru Mafia hakujawa na sekondari ya kidato cha tano na sita sasa ipo moja tumeanzisha ni Sekondari ya Kitomondo yenye miaka mitatu tangu kuanzishwa. Si hivyo tu hata ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2016 na leo tunafaulisha kwa asilimia 82," anasema Nnunduma.

Vilevile, anazungumzia ufaulu , akisema kitaifa wamepanda mwanzoni mwa 2016 Mafia ilishika nafasi ya 107 kitaifa leo imependa na kushika nafasi ya 54 kitaifa katika matokeo ya darasa la saba.

### UMEME WA KUTOSHA

Aidha, Nnunduma anasema licha ya kuwa ni kisiwa katikati ya bahari umeme si tatizo, vijiji 20 vya kisiwa kikuu cha Kilindoni vimepata umeme unaosambazwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na vimebakia vichache vilivyo katika visiwa vya Jibondo, Bwejuu, Chole na Juwani ambavyo vitapata umeme wa jua na tayari zabuni ya kumpata mkandarasi ameshatangazwa.

### KILIMO JUU

Aidha, Mkuu wa Wilaya anasema kisiwa hicho chenye watu takribani 51,000 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, kimejizatiti katika kilimo na kufanya mambo makubwa.

"Kuanzia mwaka 2016 uzalishaji wa korosho umeongezeka kutoka tani nne na sasa tumefikia tani 214 zilizopatikana mwaka 2018. Mafanikio haya ni kuzingatia maelekezo ya wataalamu, kutumia pembejeo hasa kunyunyuzia dawa na wananchi kuwa na bidii na juhudi za kufanyakazi." Anasema Mkuu wa Wilaya.

### HUDUMA ZA AFYA.

Mganga Mkuu wa Wilaya Dk. Zuberi Mzige, anasema licha ya kuwa na hospitali ya kisasa wilaya ina zahanati nne ziko katika visiwa vya Jibondo, Chole, Juwani na Bwejuu.

Anazungumzia pia chumba cha kuhifadhi miili akisema kina uwezo wa kuhifadhi miili sita na kwamba kimekamilika na kwa mara ya kwanza Mafia inakuwa na huduma hiyo.

### BOTI YA AMBULENSI

Dokta Mzige anasema , Mafia ina visiwa vingi na usafiri unategemea mitumbwi, boti, majahazi na mashua na hilo linaathiri huduma za afya hasa za dharura.

Anaeleza kuwa ili kuondoa changamoto hiyo serikali imetenga Sh. milioni 200 kwa ajili ya kununua boti ya wagonjwa au ambulensi boti.

Anaeleza kuwa zabuni imeshaandaliwa kwa ajili ya kununua boti hiyo na wakati wowote wanaamini kuwa itapatikana.

### CHANGAMOTO

Mzige anataja usafiri usio na uhakika kwa sababu mara nyingi vyombo vya majini vinatatizwa na upepo mkali na dhoruba ambayo hukwamisha watu kwenda huku na huko kutoa huduma.

Wakati mwingine wanatumia majahazi kusafirisha dawa na wagonjwa lakini licha ya upungufu huo hawajaacha kutoa huduma kwa wananchi. Anasema pia kuwa usafiri wa ndege si rafiki ni ghali na pia kuwa wagonjwa ambao hawawezi kupanda ndege.

### MATUMAINI MAPYA

Mganga Mkuu wa Wilaya anasema wana matumaini ya kumaliza changamoto hizo kwa sababu serikali imeahidi kupanua uwanja wa ndege wa Mafia ili ndege kubwa zitue na kutoa huduma kama ilivyo mikoa mingine.

"Hili ni ombi letu ATC, kwa kuwa Rais ametoa ndege mbili za serikali zitumike kwenye usafirishaji tunaomba Mafia ipewe kipaumbele kwenye ndege hizo kuwapa watu unafuu badala ya kutegemea mashua na majahazi." Anaomba.

Baadhi ya kina mama wanachama wa Sauti ya Wanawake Mafia (Sawama) wakizungumzia huduma za afya wanafurahia kuwapo kwa xray ya ultra sound ambayo kwa miaka mingi waliikosa.

Hata hivyo wanalalamikia ukosefu wa viwanda vya kusindika mazao kama samaki, nazi na korosho na kuiomba serikali kusaidia upatikanaji wa viwanda ili uhuru uwe na maana ya kubadili maisha kijamii na kiuchumi.

# Trump atamwachia Makamu Pence ofisi?



Makamu wa Rais wa Marekani, Mike Pence, ndiye anayekuwa kiongozi iwapo Bunge la Seneti litampata Rais Trump na hatia. **PICHA: MTANDAO**

> Ushahidi si wa kuzozaniwa. Rais alikiuka mamlaka yake kwa ajili ya faida zake za kisiasa kwa kutumia usalama wa taifa letu , kwa kuzuia msaada wa kijeshi na mikutano muhimu ya kitaifa ili kushinikiza uchunguzi ufanyike dhidi ya hasimu wake.

**Na Mwandishi Wetu**

SPIKA wa Bunge la Wawakilishi nchini Marekani, Nancy Pelosi, anasema chombo hicho kitawasilisha mashtaka ya uchunguzi dhidi ya Rais Donald Trump, kwa madai ya matumizi mabaya ya mamlaka yake. Au kutumia vibaya ofisi ya umma.

"Demokrasia yetu iko mashakani, Rais anatuacha bila chaguo la kufanya," anasema kiongozi huyo wa ngazi ya juu wa wapinzania wa Trump, chama Democrat.

Anayasema hayo siku moja baada ya kamati ya masuala ya sheria ya bunge kuanza kuangalia mashitaka yanayoweza kuwasilishwa dhidi ya rais huyo kutoka chama cha Republican.

Rais Trump aliwaambia wanachama wa Demokrats kama watataka kumshitaki basi waharakishe anawaeleza hayo kwa kuwatumia ujumbe wa Twitter muda mfupi kabla ya kauli za Spika Pelosi. Anasema: "Kama mtanichunguza, mfanye sasa hivi, haraka, ili tuwe na kesi ya haki katika Seneti, ili nchi iweze kuendelea na shughuli za kawaida"

Mbunge wa Bunge la Congress kutoka jimbo la California, anauambia mkutano wa waandishi wa habari Alhamisi iliyopita kuwa "ushahidi si wa kuzozaniwa. Rais alikiuka mamlaka yake kwa ajili ya faida zake za kisiasa kwa kutumia usalama wa taifa letu , kwa kuzuia msaada wa kijeshi na mikutano muhimu ya kitaifa ili kushinikiza uchunguzi ufanyike dhidi ya hasimu wake."

Anaongeza kuwa: "Tunatarajia kuwa na kesi ya usawa katika Seneti."

Wiki iliyopita mshauri wa ngazi ya juu ya Trump Kellyanne Conway, aliwaambia waandishi wa habari : "Tuko tayari kwa kesi."

"Hapo ndipo upande wa utetezi utakapotumia sheria," anasema, na kuongeza kuwa Republican wanatarajia kuwaita mashahidi wao wenyewe.

Hivi karibuni Spika Pelosi anafanya mkutano wa faragha kuhusu uchunguzi pamoja na wanachama wa Demokrat wenzake na akawauliza : "Je mko tayari?"

Wabunge hao wakajibu kwa sauti ya juu "ndiyo", kwa mujibu wa shirika la habari la Associated Press na Jumatano iliyopita wataalamu wa sheria ya katiba walitoa ushahidi mbele ya Kamati ya Mahakama Bunge kwamba vitendo vya Rais Trump kutaka msaada kutoka kwa taifa la kigeni ni makosa yanayostahili kuchunguzwa.

Wanasema kuwa vitendo vya kiongozi huyo wa Marekani vilikuwa ni kosa, lakini si la kiwango cha kuchunguzwa.

Katika mawasiliano ya simu, Trump alimtaka Rais wa Ukraine Zelensky amchunguze Joe Biden, ambaye kwa sasa ndiye mgombea aliye mstari wa mbele kuwania kiti cha urais kwa tiketi ya chama cha Democratic katika uchaguzi wa urais mwaka ujao, na mtoto wake wa kiume Hunter Biden, ambaye awali alifanyia kazi kampuni ya nishati ya Ukraine ya Burisma.

Uchunguzi unataka kubaini ikiwa Trump alitumia kitisho kuzuia msaada wa jeshi la Marekani kwa Ukraine ili kuifanya imchunguze Biden na mwanae. Rais Trump amekana kufanya kosa lolote na ameutaja uchunguzi kuwa ni "hila".

Wiki iliyopita, Kamati ya Masuala ya Ujasusi ilikamilisha wiki mbili za kusikiliza kesi hiyo , kufuatia wiki kadhaa za vikao vya faragha ambapo waliwahoji mashahidi kadhaa.

Adam Schiff, Mwenyekiti wa Kamati ya Ujasusi, anayeongoza uchunguzi huo alisema kamati za masuala ya kigeni na intelijensia ilitoa ripoti hiyo wiki iliyopita 3 Desemba 3.

**MCHAKATO UCHUNGUZI**

Kwa wale wanaofuatilia mwenendo mzima wa kumchunguza Truimp hiki ndicho kitakachofuata katika hatua za kumchunguza Rais Trump kwenye kesi hiyo ya matumizi mabaya ya ofisi.

Jukumu la kumchunguza Rais Trump linaanzia kwenye kamati sita za bunge ambazo ndizo zinazomchunguza zitafanyakazi na zitawasilisha mapendekezo yake katika Kamati ya Sheria ya Bunge ambayo huangalia uwezekano wa kufanya uchunguzi.

Mambo ambayo yanatarajiwa kuwekwa hadharani na kamati hizo ni iwapo kuna ushahidi wa kutosha wa makosa yanayotolewa uliobainika kwenye kuandaa taratibu za uchunguzi.

Aidha ni jukumu la kamati hiyo kuona na kuchambua iwapo upo ushahidi wa kutosha uliobainika unaowezesha kufanya uchunguzi dhidi ya Rais.

**KUAMUA HATMA**

Katika mchakato huo kuna suala la Trump kubakia madarakani au kuondolewa, kinachoamua hatma hiyo ni bunge kupigia kura vipengele vya uchunguzi .

Matokeo yanategemea wingi wa wapiga kura. Iwapo kutakuwa na idadi ndogo ya wabunge wanaounga mkono Trump kuchunguzwa ni wazi kuwa ataendelea kubaki ofisini kwa sababu wachache wameunga mkono uchunguzi dhidi yake. Lakini, kama walio wengi zaidi ya asilimia 51 wakaunga mkono uchunguzi ufanyike hapo ni lazima Rais Trump atachunguzwa na kazi hiyo itaanzishwa na Seneti au Bunge la Juu.

Baada ya Seneti kufanyakazi yake suala linarudi tena kwenye kupiga kura iwapo impempata na hatia au lah. Kama idadi ndogo au chini ya theluthi mbili ya wabunge wa Seneti watapiga kura ya kumtia hatiani moja kwa moja Trump atabaki madarakani.

Na ikitokea theluthi mbili asilimia 67 ya wajumbe wa Seneti wakipiga kura kuwa ana hatia Rais Tump ataondoka madarakani na Makamu wa Rais Mike Pence, atachukua mamlaka ya ungozi wa nchi.

**BBC**



# Teku: Kifungo cha TCU kimetupa fundisho

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

UONGOZI wa Chuo Kikuu cha Teofilo Kisanji (Teku) cha jijini Mbeya, umesema kitendo cha chuo hicho kufungiwa kudahili wanafunzi na Tume ya Vyuo Vikuu nchini (TCU) kutokana na upungufu uliyokuwapo, imekuwa fundisho kwao na kwa taasisi zingine.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mwenyekiti wa Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini Magharibi, Mchungaji Zacharia Sichone, wakati uongozi wa chuo hicho ulipokuwa unazungumza na wanahabari.

Mchungaji Sichone alisema, kanisa wanatambua changamoto zilizokuwa zimeibuka wakati chuo hicho kilipokuwa kimefungiwa na kwamba serikali ilifanya hivyo kwa ajili ya kuboresha sekta ya elimu nchini. Baada ya Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Herman Mwasonko, kueleza katika taarifa yake kuwa ukusanyaji wa mapato umeshuka kutokana na kusitishwa kwa udahili kwa mwaka 2017/18 na hivyo kusababisha kushindwa kulipa mishahara kwa watumishi wake.

"Tuna kila sababu kuishukuru serikali kwani licha ya kusitisha kwa muda huo, lakini tulikaa na kuzungumza na kufuata maelekezo ya Tume na kwa mwaka 2019/20 tunaendelea kuzalisha wasomi wa fani mbalimbali ili kwenda na kasi ya serikali ya awamu ya tano," alisema Mchungaji Sichone.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Herman Mwasonko, alisema kuwa chuo hicho kwa sasa mapato yake yameshuka kutokana na chuo hicho kufungiwa na kwamba wakati huo baadhi ya gharama zilikuwa bado zinaendelea kufanyika.

Alisema chuo hicho kilikuwa na watumishi ambao walikuwa wanahitaji kulipwa mishahara na posho zao kwa ajili ya uendeshaji wa maisha yao kama ilivyo kwa watumishi wengine walioajiriwa.

"Kilikuwa kipindi kigumu sana kwani miaka miwili kutokuwa na wanafunzi ni changamoto kubwa, huku kukiwa na watumishi, ambao wanahitaji kulipwa mishahara," alisema Prof. Mwasonko.

Hata hivyo Prof. Mwasonko alisema jana katika mahafali ya 12 ya chuo hicho yaliyofanyika mwaka huu, wanafunzi wa fani mbalimbali 1,245 walihitimu na kati yao wavulana 657 na wasichana 588.

Makamu Askofu wa Kanisa la Moravian Jimbo la Kusini Magharibi, Kenady Panja, alisema kanisa hilo linakusudia kuweka mipango ambayo itasaidia kukiwezesha chuo hicho kisikumbwe na janga la kufungiwa tena.

Mhitimu wa fani ya uandishi wa habari ngazi ya diploma, Ainess Thobbia, alisema kuwa wanamshukuru Mungu kwa kuhitimu mafunzo hayo na kwamba amejiandaa kuitumikia jamii na kuwa chachu hususan katika suala zima la kujiajiri.



Wafanyakazi wa moja ya kampuni ya ujenzi ya jijini Mbeya, wakipakia tangi la mafuta kwenye gari wakati wa marekebisho ya kituo cha mafuta kilichopo eneo la Posta jijini humo, juzi, huku wakiwa wamezungushia utepe eneo hilo kwa ajili ya tahadhari kwa watumiaji wengine wa barabara. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Viongozi mila wajitosa misitu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa mila wa Kata za Njelenje na Mshewe katika Halmshauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuwashirikisha katika utunzaji wa misitu kwa kuzuia ukataji ovyo wa miti kwa ajili ya kuni na uchomaji wa mkaa.

Walitoa kauli hiyo juzi walipokuwa wanazungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti katika maeneo hayo ambapo walisema wao ndio wanaishi karibu na misitu hiyo, kuliko watendaji wa serikali ukiwamo Wakala wa Misitu nchini (TFS).

Kiongozi wa mila wa Kata ya Njelenje, Joseph Manjonje, alisema katika eneo hilo kuna baadhi ya watu wanaingia kinyemela misituni na kuanza kuvuna miti kwa ajili ya shughuli hizo na kwamba huwa shughuli hizo zinafanyika zaidi usiku.

Alisema muda huo ni vigumu kwa watendaji wa serikali kufanya doria katika maeneo hayo hali ambayo inasababisha uharibifu kuongezeka na kuhatarisha vyanzo vya maji.

"Wengi wanasafirisha mkaa na kuni hizo kwa kutumia pikipiki nyakati za usiku, lakini tukishirikishwa na tukapewa mamlaka ya kuwadhibiti wahalifu hao naamini tutafanikiwa katika vita hii ya kuokoa mazingira yetu," alisema Mwanjoje.

Alisema wengi wa waharibifu hao huwa wanatoka nje ya maeneo hayo na kwamba wakati mwingine wanapewa vibali na serikali, lakini wanavuna kuliko eneo halisi walilopewa.

Naye Chifu wa Kata ya Mshewe, Raison Ngole, alisema kwa sasa serikali imeweka kizuizi katika Kijiji cha Itimba kwa ajili ya ukaguzi wa mazao ya misitu, lakini wanakaguliwa wenye magari ambao kwa sasa hawasafirishi sana mazao hayo.

Alisema katika eneo lake wamefanikiwa kudhibiti vitendo hivyo kwa asilimia ndogo kutokana na chanzo cha maji kinachotegemewa na wananchi wa kata hiyo kwa ajili ya kilimo na matumizi ya nyumbani kwenye misitu hiyo.

Alisema changamoto kubwa iliyopo ni wananchi wa Idugumbi ambako ndiko uchomaji wa mkaa upo kwa kiwango kikubwa kwa madai wakati mwingine wanaachia moto kwenye misitu hiyo.

# Madeni machafu tishio kwa mfuko

**Na Innocent Ng'oko, MBEYA**

MENEJA wa Mfuko wa huduma za mikopo kwa ajili ya wajasiriamali SELF Micro Finance (SELF MF), Musa Rajabu, ameweka wazi kuwa vyama vingi vya ushirika wa akiba na mikopo (Saccos) katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini havikopesheki kutokana na kukabiliwa na madeni makubwa kutoka taasisi zingine za fedha.

Alisema jana kuwa SELF FM ni mfuko unaojitegemea ulio chini ya udhamini wa serikali, unaotekeleza dhana ya serikali ya kupunguza umaskini wa kipato.

Rajabu alisema kumekuwa na changamoto kwa Saccos nyingi kushindwa kukopesheka kutokana na mzigo wa madeni unaosababishwa na viongozi wa vyama hivyo vya akiba na mikopo kushindwa kusimamia vyema mikopo wanayopewa na kutokukaguliwa na Shirika la Umma la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) kulingana na sheria na 15 ya mwaka 1982.

"Vyama vingi vya akiba na mikopo vina mzigo wa madeni na kutokukaguliwa kulingana na sheria ya ushirika na hivyo kupelekea vyama hivyo kushindwa kukopesheka kwa lengo la kuwawezesha wanachama kunufaika na mikopo kutoka SELF FM," alisema Rajabu.

Alisema SELF inatoa mikopo ya jumla kwa asasi ndogo na za kati za fedha kama vile mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO's), Saccos, kampuni za fedha zinazotoa huduma za mikopo na benki za wananchi ili asasi hizi ziweze kutoa mikopo kwa jamii ambayo haijafikiwa na huduma rasmi za kifedha.

Pia alisema pamoja na kutoa mikopo, pia mfuko huo huzijengea uwezo asasi na wajasiriamali wadogo ambao wanakusudiwa kunufaika na huduma hiyo ili kuweza kutoa huduma endelevu za fedha kwa jamii ambayo haijafikiwa na huduma rasmi za fedha hususan kwa jamii zilizopo vijijini.

Meneja huyo alisema kuelekea uchumi wa kati unaoendeshwa na viwanda nchini, serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango inatoa mikopo kwa wajasiriamali na Watanzania wote ili kuwawezesha kukua kiuchumi kupitia mfuko huu wa 'Self Micro Finance'.

Alisema kuwa kutokana na mabadiliko ya kisera kwa sasa mfuko wa Self Micro Finance umeunganishwa na mfuko wa UTT ambapo utawezasha kuwakopesha wafanyakazi wa serikali, mikopo ya miradi maalum ya shule na hospitali.

"Unajua riba zetu ni ndogo sana, kwa mfano wafanyakazi wa serikali wanatozwa riba ya asilimia 16 na mjasiriamali mdogo anatozwa riba ya asilimia 14 ya mkopo wake na kuwa mikopo hiyo huwa tayari ndani ya siku 21 baada ya kuhakikiwa kwa nyaraka za mwombaji," alisema Rajabu.

Mfuko huo wa serikali ulianzishwa mwaka 2000 na tayari umehudumia nchi nzima na una ofisi saba katika mikoa ya Mbeya Zanzibar, Dodoma, Mwanza, Kahama, Arusha na Dar es Salaam ambazo zinatoa huduma kikanda.





# Mahenge aonya uharibifu mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** KONGWA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amewataka wakazi wa Kongwa kuacha uharibifu wa mazingira kwa kuwa unachangia kuathiri miundombinu ya barabara.

Kauli hiyo aliitoa jana alipotembelea daraja la Mto Ibwaga lililopo Tarafa ya Mlali, wilayani Kongwa, ambalo kipindi cha mvua wananchi walikuwa wakikosa huduma muhimu kutokana na eneo hilo kutopitika.

Akizungumza na wananchi, Dk. Mahenge alisema kuwapo kwa uharibifu huo kunachangia mabadiliko ya tabia nchi na kuathiri miundombinu ya barabara.

Aliagiza kila mwananchi wa wilaya hiyo kuwa mlinzi wa mwenzake na kuhakikisha hakuna uharibifu wa mazingira kwenye eneo hilo.

"Mkikata miti ovyo kazi ya maji yatakayokuwa yakija kwenye mto huu nje ya mkondo yataathiri miundombinu ya daraja na barabara kwa ujumla kwa kuleta mmomonyoko," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, alisema wakati wa mvua mto huo ulikuwa ukikata mawasiliano na maeneo mengine na kuathiri shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

"Tunashukuru serikali kwa kufanikisha kujenga daraja la kudumu maana kipindi cha mvua eneo hili lilikuwa linageuka kisiwa," alisema.

Alitoa rai kwa wananchi kutunza miundombinu ya daraja ili lidumu kwa muda mrefu.

Awali, baadhi ya wananchi walishukuru serikali kwa kujenga daraja hilo ambalo ni muhimu kwenye eneo hilo.

Mkazi wa Ibwaga, Edson Lemuka, alisema daraja hilo ni kiunganishi cha tarafa hiyo na maeneo mengine ya Mkoa wa Dodoma na hivyo wakati wa mvua huduma za kwenda hospitali ya wilaya kwao ilikuwa ndoto kutokana na eneo hilo kutopitika.

"Hapa ukitaka kuvuka kwenda ng'ambo ya pili ni ngumu, sasa ukute mtu anaumwa anatakiwa kwenda hospitali ya wilaya hawezi kwenda njia haipitiki," alisema.

Naye Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (Tanroads) Mkoa wa Dodoma, Mhandisi Leonard Chimagu, alisema daraja hilo lina urefu wa mita 52 na upana wa mita 13 na limegharimu Sh. bilioni 2.1.



Mhandisi Nassiri Nassoro wa kampuni ya ujenzi ya Mohammed Builders Ltd, akionyesha hatua ya ujenzi wa mradi wa Soko Kuu la Dodoma ilipofikia jana, mradi huo upo eneo la Nzuguni jijini humo na unatarajiwa kukamilika Februari 2020. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Ujenzi soko jipya wakifikia asilimia 80

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

UJENZI wa soko kuu jipya la Jiji la Dodoma umefikia asilimia 80, huku mkandarasi akiihakikishia serikali kuwa atakamilisha kwa muda uliopangwa.

Awali, ujenzi huo ulitarajiwa kukamilika Desemba, mwaka huu lakini mkandarasi kutoka kampuni ya ujenzi ya Mohammed Builders Ltd, aliongezewa mkataba hadi Februari 2020 ili akamilishe.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mhandisi wa kampuni hiyo, Nassiri Nassor, alisema ujenzi huo kwa sasa upo zaidi ya asilimia 80, hivyo watahakikisha wanakamilisha kwa kipindi hicho. "Huu mradi ni mkubwa utakuwa na uwezo wa kuingia malori makubwa 30 kushusha na kupakia mizigo kwa wakati mmoja pamoja maegesho ya magari 300," alisema.

Nassoro alisema malori hayo yatakuwa na sehemu yao maalumu ya kuingia kwa ajili ya kushusha au kupakia mzigo ndani ya soko ambayo haitaingiliana na magari mengine ya kawaida.

Alisema mradi huo ni wa kisasa kutokana na uwapo wa miundombinu bora ya barabara za kuingia na kutoka ndani ya soko ili kuepuka msongamano wa magari na watu ndani ya soko.

Alitaja baadhi ya huduma zitakazokuwapo ndani ni pamoja na hoteli kubwa ambazo zitakuwa zikitoa huduma ya chakula kwa watumiaji wa soko na wageni wengine. "Kutakuwapo na sehemu ya wajasiriamali wa biashara ndogo ndogo ndani ya soko zilijengwa kutokana na mahitaji ya kila sekta ya biashara hizo," alisema.

Vile vile, alisema lengo la kampuni ni kuhakikisha wanakamilisha ujenzi wa mradi huo ifikapo Februari 2020 ili wananchi wapate huduma.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Mohammed Jafrej, alisema mradi huo hadi kukamilika utagharimu Sh. bilioni 14.1.

Alisema mradi huo wa soko umetoa ajira za watu zaidi ya 200 kwa fani za ufundi, vibarua na madereva na wahandisi wa fani mbalimbali.

# Bucha zashtukiwa kuuza nyama zisizopimwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Nyama nchini imebaini baadhi ya bucha za nyama Jiji la Dodoma kuuza bidhaa hiyo bila kupimwa na daktari wa mifugo na hivyo kuhatarisha afya za walaji.

Kufuatia hali hiyo, Bodi imefanikiwa kuteketeza kilogramu 97 za nyama ya ng'ombe iliyokamatwa baada ya kubainika haijapimwa.

Akizungumza na Nipashe kuhusu operesheni inayoendeshwa na bodi hiyo kwenye bucha za nyama, ofisa usajili wa bodi hiyo, Godfrey Sosthenes, alisema nyama hiyo ilikamatwa kwenye bucha mbili eneo la Ipagala na Mipango, jijini humo.

"Wafanyabiashara wa mabucha haya kwenye operesheni yetu tumewakuta wakiuza nyama ya ng'ombe kwa wateja bila kupimwa," alisema.

Pia alisema wafanyabiashara hao wamepigwa faini ya Sh. milioni moja kila mmoja huku wakitakiwa kutekeleza agizo la kuuza nyama ambayo imepimwa na daktari.

"Tunaendelea na operesheni ya kukagua bucha ambazo hazina mashine za kukatia nyama ambao wanakata kwenye magogo," alisema.

Alisema mpaka sasa wamekagua bucha 79 na kati ya hizo 20 zimekutwa hazina mashine za kukatia.

"Tumewapa mwezi mmoja kuhakikisha wanakuwa na mashine hizi la sivyo hawataruhusiwa kuendelea kuuza nyama," alisema.

Sosthnes aliagiza wauzaji kupima afya kila baada ya miezi sita na kila bucha kuwa na mzani wa dijitali, nondo za aluminium, madirisha na milango ya vioo.

"Vitu vingine ni sinki la kunawia mikono, kuvaa sare wakati wote na mabucha yote kusajiliwa na bodi kwa mujibu wa sheria ya tasnia ya nyama namba 10 ya mwaka 2006," alisema.

Alisema wauzaji wa bucha wanapaswa kutekeleza agizo lililotolewa na Bodi ya Nyama wakati wa mchakato wa ukaguzi unaoendelea jijini hapa.

Hata hivyo, alisema lengo lao ni kuona kila bucha lina vifaa vyote vinavyotakiwa kuwapo ili kuuza nyama ambazo ziko salama kwa jamii.

"Hivi sasa tunaendelea kutoa elimu kwa wauzaji nyama ili kuuza nyama ambayo ipo bora kwa jamii, lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kutaka kuepusha magonjwa yanayotokana na nyama kutopimwa," alisema.





## Rais Shein kuzindua kongamano la Diaspora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, anatarajiwa kuzindua kongamano la siku mbili la Diaspora linalotazamiwa kufanyika tarehe 14 hadi 15 katika hoteli ya kitalii ya Verde iliopo Maruhubi mjini Unguja.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Ussi, akizungumza na waandishi wa habari, alisema kongamano hilo limebeba ujumbe wa kaulimbiu "Mtu kwao ndiyo ngao".

Alisema hilo ni kongamano la sita ambalo limetayarishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuwakutanisha Watanzania wanaoishi nje ya nchi.

Ussi alisema jumla ya washiriki 300 wanatarajiwa kuhudhuria kongamano hilo wakiwamo wawekezaji 150 kutoka nchi mbalimbali.

Alisema katika kongamano hilo watendaji wa taasisi za fedha na benki na mashirika ya umma yaliopo nchini watahudhuria na kupata nafasi ya kusikiliza changamoto zinazowakabili wana Diaspora.

"Kongamano hilo lengo lake kubwa ni kuwakutanisha wana Diaspora pamoja na watendaji wa mashirika mbalimbali pamoja na taasisi za fedha kwa ajili ya kubadilisha mawazo na kujadili mustakabali wao katika kujenga uchumi imara,"

# 'Adhabu ya viboko isiwe kukomoa wanafunzi'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Muhamed Said, amesema kuna wakati walimu hulazimika kuwapa adhabu ya viboko wanafunzi kwa nia njema ya kuwajengea nidhamu nzuri, lakini hiyo isitumiwe kama fursa ya kuwakomoa kwa kuwapiga vibaya.

Akizungumza wakati wa hafla ya kuwaaga wanafunzi wa darasa la sita na kidato cha nne wa shule ya Feza, mjini hapa, alisema katika kumchapa mwanafunzi lazima mwalimu afuate matakwa yaliyowekwa kisheria ambayo miongozo yake inafahamika vizuri.

Aliwataka kufuata utaratibu mzuri iwapo kunatokea haja ya kuwapa wanafunzi adhabu ya kinidhamu badala ya kuwachapa kwa hasira hali inayoweza kuwasababishia madhara ya kimwili.

Alieleza kuwa suala la ufundishaji linahitaji walimu wenye saikolojia ya kutosha ya kumjua mtoto na kufahamu namna ya kuishi naye.

"Mwanafunzi ni mtoto hivyo bado anahitaji kulelewa na mwalimu wakati akiwa shule, ni vyema walimu watumie busara kubwa katika ulezi huo na sio kuwapa adhabu iliyopindukia mpaka mtoto anaiogopa shule," alisema.

Alitoa wito kwa wamiliki wa shule binafsi kuajiri walimu waliopata mafunzo ya kazi hiyo na wenye weledi wa kutosha na kuacha mara moja kuchukua ambao hawajasomea kwa lengo la kusaidia.

Alisema kufanya hivyo ni kinyume na Sheria ya Elimu ya Mwaka 1982 kifungu cha 36 (2).

Kwa upande mwingine, alikemea tabia ya madereva wa mabasi ya wanafunzi kujaza watoto kupita kiasi na kuvitaka vyombo vya usalama kuwafuatilia na kuhakikisha wanachukuliwa hatua za kisheria.

"Kuna gari za baadhi ya shule zinajaza wanafunzi kinyume na uwezo wao, hii ni hatari kwa usalama wao na pia wanafunzi hawashushwi katika vituo husika, hivyo wamiliki wa shule acheni mtindo huu kwa kuwa usalama wa mwanafunzi ni kitu cha kwanza," alisema.

Aliwakumbusha walimu, wazazi na jamii kuimarisha uangalizi wa watoto ili kuwaepusha na vitendo viovu vikiwamo vya udhalilishaji wa kijinsia vilivyoshamiri nchini.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Fedha, Ali Nungu, aliishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa namna inavyothamini mchango wa shule binafsi, jambo alilosema linaongeza ari ya kuongeza bidii na kupata matokeo mazuri kitaifa.

Alitoa pongezi kwa walimu wa shule hiyo, ambao wamekuwa chachu ya mafanikio wanayopata, ikiwamo mwaka 2018 kushika nafasi ya kwanza kwa matokeo ya darasa la nne kitaifa, darasa la sita na kidato cha nne wa pili, mwaka 2019 nafasi ya kwanza kidato cha sita.

Katika risala yao, wanafunzi walibainisha kuwa umoja na ushirikiano ndiyo silaha pekee inayowaletea ufanisi na kung'ara katika mitihani ya taifa Tanzania.

Walisema, kwao suala la elimu ndio kipaumbele na wamekuwa wakipuuza vishawishi ikiwamo matumizi mabaya ya simu za mkononi na mitandao ya kijamii.

Hata hivyo, waliwashukuru walimu na wazazi wao kwa kuwapa kila msaada unaohitajika kwa lengo la kuwajenga kitaaluma ili wawe wajenzi wazuri wa taifa na familia hapo baadaye.



Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohamed Said (kushoto), akitoa salamu za rambirambi kwa baba mzazi wa marehemu Zainab Vuai Dude (16). **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Wanafunzi wafariki dunia wakitoka kufanya mitihani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SIKU chache baada ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kusikitishwa na ongezeko la ajali za barabarani Zanzibar, wanafunzi wawili wa Shule ya Sekondari ya Chaani, Mkoa wa Kaskazini Unguja, wamefariki dunia juzi baada ya kugongwa na gari.

Wanafunzi hao waligongwa wakati wakitoka shule kufanya mitihani yao ya taifa ya kidato cha pili ambayo imeanza Desemba 5, mwaka huu. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ali Haji Ali, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kuwataja waliofariki kuwa ni Zainab Vuai Dude (16) na Dhulfa Miraji Ali (16).

"Wanafunzi hao waliopata ajali walikuwa wakitoka shule na kuelekea nyumbani baada ya kufanya mitihani yao ya taifa ya kidato cha pili," alisema.

Alisema waligongwa na gari iliyokuwa ikiendeshwa na Abeid Khamis (36) na chanzo cha ajali ni mwendo kasi.

"Ajali hii kwa mujibu wa uchunguzi wa awali inaonyesha kwamba imesababishwa na mwendo kasi na kusababisha vifo vya wanafunzi wetu wawili kupoteza maisha," alisema.

Takwimu za hivi karibuni visiwani Zanzibar, zimebainisha kwamba watu 145 wamepoteza maisha kutokana na ajali za barabarani kuanzia mwezi Januari hadi Oktoba, mwaka huu.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi ,alisema ni jambo la kuhuzunisha kuona kwamba tafiti hizo zinaonyesha kuwa watu 12 hufariki kila mwezi kutokana na ajali za barabarani.

Alisema ajali hizo zimekuwa zikiripotiwa kila siku na hatima yake kuacha majonzi na simanzi kwa wananchi.

Balozi Iddi, alisema hiyo ni hali ya kutisha na wakati wa kuchukuliwa hatua madhubuti za kudhibiti ajali barabarani ikiwamo kuhakikisha mtu asiye na leseni ya udereva haendeshi chombo cha moto.

Aliliagiza Jeshi la Polisi kupitia askari wake wa usalama barabarani kuwadhibiti watu wanaoendesha vyombo vya moto wakiwa tayari wameshalewa.

HABARI KITAIFA

# Sekta binafsi yaombwa ufadhili wa mashauriano

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

BARAZA la Taifa la Biashara Tanzania (TNBC) limewashauri wawekezaji na wafanyabiashara nchini kuwa sehemu ya wafadhili ili mikutano ya mashauriano katika ngazi ya mkoa na wilaya ambayo kwa sasa haifanyiki kwa sababu ya ukosefu wa fedha ifanyike kama inavyotarajiwa.

Akizungumza kwenye mkutano wa mashauriano hapa hivi karibuni, Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza hilo, Oliva Vegula, aliwaambia wajumbe wa mkutano huo mikutano ya mikoa na wilaya ni muhimu katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini. Mkutano huo ulihudhuriwa na watendaji wa serikali, wawekezaji na wafanyabiashara wa Mkoa wa Morogoro ili kujadili changamoto zinazowakabili na kuzipatia ufumbuzi. "Tumekuwa na changamoto ya kuratibu na kuhakikisha mikutano hii katika ngazi ya mkoa na wilaya inafanyika. Haifanyiki kwa sababu ya kukosekana kwa rasilimali fedha. Kwa hiyo tunawaomba wawekezaji na wafanyabiashara katika ngazi hizo wajitoe na kushirikiana na serikali ili kuhakikisha mikutano hii inafanyika walau mara moja kwa mwaka," amesema Vegulla.

Alieleza kuwa mabaraza ya mikoa na wilaya ndio sehemu ya maboresho ya mazingira ya uwekezaji na biashara nchini kwani utatuzi wa changamoto zote unaanzia huko, na kuongeza kwamba kuna kila sababu ya wafanyabiashara na wawekezaji kuchangia gharama za mikutano hiyo ili ifanyike.

"Tija ya majadiliano itaonekana endapo mikutano itakuwa inafanyika mara kwa mara. Mikutano hii itasaidia kujua hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kutatua changamoto zinazohusu serikali kwa ngazi ya mkoa na taifa kwa ujumla," alisema Vegulla.

Ameongezea kuwa maboresho ya mazingira ya biashara yanategemea zaidi majadilianao kati ya sekta ya umma na binafsi na kwamba serikali inatambua umuhimu wa mikutano hiyo katika mikoa na wilaya.

"Baraza lina jukumu la kuhakikisha uwekezaji katika viwanda unakua na kwamba jambo la muhimu ni sekta za umma na binafsi kushirikiana katika utekelezaji ili azma ya serikali ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifanikiwe," amesema Vegulla.

Akitoa mfano wa umuhimu wa mikutano hiyo, alisema changamoto za tozo na migogoro ya ardhi zimeibuliwa katika mikutano hiyo na kueleza kwamba sasa serikali itafuatilia ili kupata majibu ya changamoto hizo ili kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Akifunga mkutano huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji),

Angela Kairuki, alisifu matokeo ya mkutano huo kwa kusema kwamba majadiliano yalikuwa ya wazi, kila mjumbe ametoa maoni na mapendekezo yake kwa nia ya kuboresha uwekezaji na biashara nchini. "Jambo muhimu ni TNBC kuhakikisha mikutano ya mabaraza ya mikoa na wilaya inafanyika kila mwaka ili kutoa nafasi kwa sekta binafsi kueleza changamoto zao na serikali kuzitolea majibu," alisema Waziri Kairuki.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Amina Khamis Shaabani, akimkabidhi Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Benki ya CRDB, Godfrey Sigalla, Tuzo ya Benki Bora katika utayarishaji wa ripoti za kifedha kwa mwaka 2018, iliyotolewa na Bodi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu (NBAA). Hafla ya kukabidhiwa tuzo ilifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Meneja Mwandamizi Idara ya Fedha, Hemed Mkuu na Mkuu wa Idara ya Fedha na Utawala Kampuni Tanzu ya Bima, Abdallah Mrisho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yabana bodi, watendaji Saccos

**Na Mathias Canal,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mhandisi Mathew Mtigumwe, ameiagiza bodi na watendaji wa Saccos kuwasilisha Rasimu za Taarifa za Fedha kwa Wakaguzi wa Nje (COASCO) kabla au ifikapo Januari 31, mwakani. Mhandisi Mtigumwe alitoa agizo hilo jijini Dodoma, ambapo alisema ni lazima kuwasilisha mapema taarifa hizo ili ukaguzi uweze kufanyika kwa wakati na taarifa za ukaguzi ziwasilishwe kwa mamlaka husika ndani ya muda uliopangwa kisheria. Aliwataka wanachama wote wa Saccos hususani bodi na watendaji wa Saccos nchini kuwa matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 (The Microfinance Act 2018), kuhusu ukaguzi wa nje hivyo ni lazima kutekeleza agizo hilo kwa wakati. "Saccos zote zinatakiwa kuhakikisha kuwa taarifa za fedha za mwaka 2019 ziwe zimekaguliwa na kuwasilishwa Benki Kuu au kwa mamlaka iliyokasimiwa ambayo ni Mrajis wa Vyama vya Ushirika ifikapo tarehe 30 Aprili, 2020," alisema.

# Mbeya kutumia tani 72,969 mbolea

**Na Innocent Ng'oko**, MBEYA

MKOA wa Mbeya unatarajia kutumia tani 72,969 za mbolea katika msimu wa kilimo wa mwaka 2019/20 ukiwa unalenga kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa tija zaidi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Kilimo Mkoa wa Mbeya, Wilfred Kayombo, wakati akizungumza na gazeti hili juu ya mikakati ya ofisi ya kilimo katika kuhakikisha wakulima wanazalisha kwa tija katika mazao mbalimbali.

Alibainisha kuwa mkoa una kusudia kulima jumla ya hekta 559,589 za mazao ya chakula na biashara ambazo zinatarajiwa kuzalisha tani 3,939,949 za mazao kwa mwaka 2019/2020.

Alisema mkakati wa mkoa katika msimu wa 2019/20 unalenga kujenga uelewa zaidi wa viongozi na wagani kutumia teknolojia kwa kushirikiana na taasisi za utafiti na mafunzo, sekta binafsi na wadau wa maendeleo ya kilimo.

Alisema mbali na kiasi hicho cha mbolea, mkoa unatarajia kutumia lita 192,943 za viuatilifu vya kimiminika na mbegu bora kiasi cha kilogramu 100,427 za maharage, alizeti, mpunga, korosho na mazao mengine. .

Alisema bei elekezi gharama za mbolea kwa wakulima inazingatia gharama za ununuzi, usafirishaji na faida ya mfanyabiashara katika mchakato huo hadi kumfikia mkulima wa kawaida.

Kayombo alisema katika msimu wa 2019 na 2020 Mkoa wa Mbeya unaendelea kutekeleza mpango wa ununuzi na usambazaji wa mbolea kwa pamoja kwa kuzingatia bei elekezi ya mbolea ambayo inatolewa kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA).

Alisema kupitia mfumo wa ununuzi na usambazaji wa mbolea kwa pamoja (BPS), umekuwa na mafanikio makubwa kutokana na kuzingatia taratibu zilizowekwa katika soko na kuwa wadau wote wa sekta ya kilimo wanatakiwa kuendelea kuwahamasisha wakulima kuzalisha kwa tija zaidi.

Katika Mkoa wa Mbeya, mbolea zinazotumia mfumo wa BPS ni minjingu, TSP, DAP, UREA, NPK, CAN na SA, huku mbolea zingine zikiendelea kuuzwa na kununuliwa kwa kufuata soko lililopo.

## HABARI KIMATAIFA

# Azimio la UN kuilaani Urusi

**NEW YORK,** Marekani

BARAZA Kuu la Umoja wa Mataifa limepitisha azimio la kulaani hatua ya Urusi kuukalia mkoa wa Crimea na mji wa Sebastapol nchini Ukraine na kuitolea wito kuondoka mara moja.

Azimio hilo lilipitishwa jana, katika siku ambayo Rais Vladimir Putin na mwenzake wa Ukraine, Volodomyr Zelensky, walikuwa wakikutana mjini Paris, kwa ajili ya mzozo wa mashariki mwa Ukraine.

Kati ya wajumbe 193 wa baraza hilo, waliopiga kura ni 82 ambapo 63 waliunga mkono na 19 kupinga.

Mataifa 66 yalijizuia kupiga kura zao, huku 45 yakikataa kabisa kushiriki upigaji kura huo.

Mwaka 2014, Urusi ilipeleka wanajeshi wake ndani ya mkoa wa Crimea na pia inashutumiwa kuwaunga mkono waasi wanaotaka kujitenga mashariki mwa Ukraine, kwenye mzozo ambao hadi sasa umesha-poteza maisha ya watu 14,000.

DW

# Uingereza wapiga kura bila kitambulisho

**LONDON,** Uingereza

BUNGE la Uingereza siyo tu moja ya mabunge ambayo yanafahamika kwa demokrasia pia mfumo wake ni wa kustaajabisha.

Mfumo wake wa kupiga kura umekuwa ukibadilika kwa miaka kadhaa kadiri miaka inavyokwenda, umekuwa na mambo mengi ya kustaajabisha ambayo yatajitokeza wakati watu wanakwenda kupiga kura katika uchaguzi mkuu utakaofanyika kesho.

Zifuatazo ni miongoni mwa mbinu za kustaajabisha kuhusu vile raia wa Uingereza wanavyopiga kura kumchagua Waziri Mkuu, ambaye atachukua uongozi wa nchi hiyo ambayo uchumi wake ni watano kwa ukubwa duniani.

Nchi hiyo inatengeneza silaha za nyuklia na pia inashiriki katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Siku ya kupiga kura, inafanyika kwa njia rahisi ambapo kinachohitajika kufanywa ni kujitokeza katika kituo cha kupiga kura na kawaida huwa ni sehemu iliyokaribu na nyumba ya mpigakura. BBC




Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, ametunukiwa tuzo ya amani ya Nobel mjini Oslo, Norway, alitoa wito wa kuwapo umoja, huku machafuko ya kikabila yakiitikisa nchi yake na juhudi za suluhu pamoja na Eritrea zikionyesha kukwama. **PICHA: ALLIANCE.**

# Waathirika bomu ubalozi Marekani kulipwa fidia

**KHARTOM,** Sudan

WAZIRI Mkuu mpya wa Sudan, Abdallah Hamdok, ameahidi kuwa hivi karibuni taifa hilo litawafidia takriban dola bilioni sita waathiriwa wa mkasa wa bomu nchini Kenya na Tanzania.

Mkasa huo wa bomu ni ule uliotokea katika balozi za Marekani za 1998 mjini Nairobi na Dar es Salaam.

Akinukuliwa na gazeti moja nchini Marekani Hamdok alisema, "Tulichukua jukumu la kuangazia madai hayo na kuafikia makubaliano."

Hata hivyo, mawikili wa waathiriwa hao wanatilia shaka ahadi hiyo wakisema kwamba huenda isilipwe.

Akiwa ziarani nchini humo ikiwa ni ya mara ya kwanza, Hamdok alitaka Sudan kuondolewa katika idadi ya mataifa yaliyoorodheshwa na Marekani kwamba yanaficha magaidi.

Takriban familia 570 za wafanyakazi wa balozi za Marekani na wakandarasi waliouawa katika mashambilio pacha yaliotekelezwa na kundi la Al Qaeda mjini Nairobi na Dar es Salaam, wanatarajiwa kufidiwa.

Fidia hiyo iliyoagizwa na mahakama ya Marekani haitawafidia maelfu ya Wakenya na Watanzania ambao waliathiriwa na mashambulio hayo moja kwa moja au kwa njia nyingine.

Takriban watu 224 walifariki katika mashambulio hayo pacha ambapo 214 walikufa mjini Nairobi na watu 10 jijini Dar es Salaam.

Idadi hiyo inashirikisha Waafrika 212 na raia wa Marekani 12.

Mahakama za Marekani zimeiwajibisha Sudan kulipa fidia ya dola za Marekani bilioni 5.9 kwa watu hao kwa kuwa ilihusika kumficha kiongozi wa kundi la Al-Qaeda, Osama bin Laden wakati alipokuwa akipanga njama za kutekeleza mashambulio hayo.

Manusura hao wanaweza kupokea nyongeza ya Dola za Marekani bilioni 4.3 iwapo mahakama ya juu ya Marekani itabadilisha uamuzi wa mahakama ya chini wa kutowalipa fedha za muda waliotumia kuwasilisha kesi hiyo.

"Fidia hiyo inatilia maanani hali ya kiuchumi ya Sudan pamoja na hali ya kiuchumi ya waathiriwa ambao maisha yao yameharibiwa na wengine wengi ambao wamekuwa maskini kwa takriban miaka 20 kutokana na kufariki kwa baba, mama, mume au mke," aliandika wakili wa waathiriwa mwenye makao yake nchini Marekani, Gavriel Mairone.

**BBC**

# Muuguzi aiba kichanga, amficha kwa shangazi

**ISLAMABAD,** Pakistan

MUUGUZI wa dharura nchini Pakistan, amekamatwa baada ya kudaiwa kumuiba mtoto mchanga ili ampelekee shangazi yake ambaye hakuwahi kuwa na mtoto.

Mtoto huyo mchanga wa kike aliibiwa muda mfupi baada ya kuzaliwa katika Hospitali ya Mji wa Balochistan, uliopo Kusini-Magharibi mwa nchi hiyo.

Awali, familia haikuwa inafahamu kuwa mtoto wao alitoweka kwa sababu hakuna yeyote aliyemfichulia mama yake kuwa alikuwa amejifungua mapacha.

Ilijulikana kwa mara ya kwanza pale mama alipopata fahamu tena na kuuliza wapi aliko "msichana wake mwingine," shemeji yake ameiambia BBC.

Abdul Hamid alikuwa amempeleka mama huyo mtarajiwa, Jamila Bibi, katika hospitali ya mji wa Loralai, yapata kilomita 60 (maili 37) Kusini-Magharibi mwa kijiji chao, Jumatano, polisi walisema.

Aliiambia polisi kuwa baada ya kujifungua, familia ya Jamila Bibi ilikabidhiwa mtoto mmoja na kuambiwa impeleke mgonjwa nyumbani kwa sababu alikuwa na hali nzuri.

Hata hivyo, Jamila Bibi aliendelea kuwa katika hali ya kutojitambua kwa siku kadhaa zilizofuata na ni katika kipindi hicho ambapo mtoto aliyekwenda naye nyumbani alifariki.

Alipopata fahamu mama huyo alifichua kile kilichoiacha familia vinywa wazi kwa mshangao.

"Ijumaa, wakati Bibi aliporejesha fahamu, aliuliza ni wapi alipo mtoto wake mwingine msichana. Tulishangaa." Abdul Hamid aliiambia BBC.

"Baada ya Hamid kuwasilisha malalamiko polisi, tulimkamata muuguzi wa dharura ambaye alikuwa zamu katika chumba cha uzazi usiku ule na akatuongoza moja kwa moja kule alikokuwa mtoto mchanga," Jahangir Shah, Ofisa katika kituo cha polisi cha Loralai alisema.

"Alikuwa amesaidiwa na manesi wenzake wawili kumtorosha mtoto mchanga nje ya hospitali na kumpatia shangazi yake ambaye alikuwa ameolewa kwa miaka 17 lakini alikuwa bado hajapata mtoto. Muuguzi alituambia kuwa shangazi yake alikuwa ametaka sana kuasili mtoto mchanga."

Polisi imewakamata wanawake wote wanne, huku familia ikiunganana na mtoto wao mchanga ambaye bado hajapewa jina.

Maofisa wanasema kuwa tukio hilo limetokana na ukosefu wa taratibu, kama vile kuweka majina kwenye mikono ya watoto wachanga wanaozaliwa na uzembe wa maofisa usalama katika milango ya kutoka kwenye hospitali hiyo.

Daktari Bingwa wa Uzazi wa Wanawake katika Hospitali ya Bolan Medical mjini Quetta, mji mkuu wa Jimbo la Balochistan, aliambia BBC kuwa tukio hilo halikutarajiwa.

"Hakuna hospitali yoyote ya serikali katika jimbo yenye taratibu za usalama kama vile kuweka majina ya watoto wanaozaliwa au usajili wao ambao unaweza kuthibitishwa wanapoondoka katika milango ya kutoka hospitalini," alisema akiomba jina lake lisitajwe.

**BBC**

# Kila siku watoto wawili wapewa mimba Lindi

**Na Mwandishi Wetu**

MAADHIMISHO ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yalihitimishwa rasmi jana, huku ikielezwa kuwa watoto 565 wamepata ujauzito mkoani Lindi katika miezi minane ya mwanzo ya mwaka huu.

Takwimu hizo zinatoa taswira kwamba, kwa wastani kila siku, watoto wawili wanapata mimba mkoani humo.

Katibu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (Bakwata) Mkoa wa Lindi, Abdillahi Mfaume, aliyasema hayo wakati wa kongamano la viongozi wa dini kuadhimisha Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia lililofanyika jijini Dar es Salam jana.

Akinukuu takwimu za Idara ya Ustawi wa Jamii Mkoa wa Lindi, Mfaume alibainisha kuwa katika orodha hiyo ya watoto 565, watoto 43 ni wa shule za msingi, 108 ni wa sekondari na 414 ni wa nje ya shule.

"Sasa, angalia katika kipindi hicho kifupi cha miezi minane, watoto wote hao wamepata mimba za utotoni. Wako kwenye umri wa miaka 18, lakini wanaingizwa kwenye majukumu magumu ya kulea.

"Hapo tayari tunazalisha tatizo lingine la kupata watoto wenye udumavu maana mama zao hao bado hawajafikia umri sahihi wa kubeba ujauzito na hawajaandaliwa kubeba mimba ya mtoto mwenye afya ya akili. Hili ni tatizo kubwa mkoani kwetu Lindi," alilalamika.

Kongamano hilo lililohudhuriwa na viongozi wa dini kutoka madhehebu mbalimbali nchini, lilifadhiliwa na Norwegian Church Aid kwa kushirikiana na Church of Sweden.

Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia yalianza rasmi Novemba 25, mwaka huu.



Meneja wa Benki ya NMB Tawi la Mazengo jijini Dodoma, Victor Dilunga, akitoa elimu kwenye kongamano la mafundi wa fani mbalimbali Mkoa wa Dodoma lililofanyika jijini humo, Benki ya NMB ilidhamini kongamano hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yawahakikishia wakulima masoko

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imewahakikishia wakulima na wafugaji kuwa inafanya kila njia kuwapatia masoko ya uhakika ya mazao kwa kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda vya kuchakata nchini.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga aliyasema hayo mjini hapa wakati wa uzinduzi wa kongamano la maonyesho ya kilimo yaliyofanyika Kampasi kuu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Waziri Husunga alisema serikali imeanza kuchukua hatua mbalimbali kwa kutoa nafasi kwa wadau hasa wa sekta binafsi zikiwamo kampuni za kibiashara na mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) kushiriki kikamilifu kwa kuhakikisha masoko ya uhakika yanapatikana ili kuchangia maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwamo kilimo na mifugo.

Alisema Wizara ya Kilimo imeanza kuwekeza rasilimali za kutosha ikiwamo nguvu kazi na fedha ili kuhakikisha kilimo kinaendelea kukua na kuwa na ufanisi zaidi ikiwamo kuwaunganisha wakulima na masoko ya uhakika.

Kuhusu kongamano la maonyesho ya kilimo la mwaka huu, Waziri Hasunga alisema la msingi kwa kuzingatia upana wa sekta na ufugaji kwa kuwa hayawezi kuletwa na taasisi moja pekee bali ni lazima nyingine zishiriki kila mmoja kwa nafasi yake.

"Mkulima na mfugaji ndio msingi kwa kuwa mtekelezaji mkuu katika uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo na ili apate mafanikio inabidi taasisi na kada nyingine zihusike ikiwamo watafiti, wagani, wauza pembejeo, wanunuzi na wachakataji," alisema.

Naye, Mratibu wa kongamano na maonyesho ya kilimo ya SUA, Profesa Sebastian Chenyambuga, alisema kongamano hilo ni la tatu hufanyika kila mwaka chuoni.

Alisema kupitia kongamano hilo wadau hao kwa pamoja wameweka mikakati ya kuboresha sekta zao ili kuongeza mchango katika kukuza pato lao na la taifa ili kufikia lengo la serikali la kuwa na uchumi wa viwanda.

INATOKA UK 2

# Mfungwa agoma kutoka gerezani

Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa magereza walikuwa wameshaondoka eneo la tukio kuelekea gereza lingine na waliobaki gerezani hapo walikuwa askari magereza.

Abraham ni miongoni mwa wafungwa 259 waliopata msamaha wa Rais katika Mkoa wa Mbeya kutoka katika magereza mawili ya Ruanda na Kilimo la Songwe.

**Wahakikiwa alama vidole**

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amewataka wafungwa waliopewa msamaha wa rais mkoani humo, wakajishughulishe na kilimo, mifugo, na biashara, ili wapate vipato vya kuendesha maisha yao na kuachana vitendo vya uhalifu.

Amesema wafungwa wote walioachiwa kwa masamaha, wameandikwa majina yao, kupigwa picha, pamoja na kuweka alama ya kidole ili atakayekwenda kufanya uhalifu na kupelekwa kwenye magereza hayo hataachiwa bali maisha yake yote yatakuwa humo.

Telack alitoa tahadhari hiyo jana, wakati alipokwenda kujiridhisha majina ya wafungwa 74 mkoani humo ambao wamepewa msamaha na Rais juzi jijini Mwanza, kwenye maadhimisho ya miaka 58 ya Uhuru na miaka 57 ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, kati ya wafungwa 5,533 nchini.

Alisema kwa kuwa kipindi hiki ni cha msimu wa mvua, wafungwa hao 74 wakajikite kwenye shughuli za kilimo ili waweze kupata mavuno, kufuga mifugo, na kufanya biashara za kuwaingizia kipato halali na siyo kurudi kuiba.

"Natoa tahadhari kwenu nyie wafungwa ambao mmeachiwa huru kwa msamaha wa Rais John Magufuli, msirudi uraiani kwenda kufanya matukio ya uhalifu tena, na bahati nzuri mmeachiwa kwenye kipindi kizuri cha msimu wa mvua, hivyo muende mkajishughulishe na kilimo ili mpate mavuno na kuinuka kiuchumi,"alisema Telack.

"Wafungwa ambao mmeachiwa mkoani Shinyanga, majina yenu tunayo, picha zenu pamoja na alama za vidole, hivyo mkirudi kwenda kufanya uhalifu tena tutawatambua na hatutaachia tena, bali mkafanye shughuli ambazo zitawaingia kipato halali," aliongeza.

Naye Mkuu wa Magereza mkoani Shinyanga Kamishna msaidizi wa Magereza, Dk. Wilison Rugamba, alisema wafungwa walioachiwa huru mkoani humo ni waliobakiza vifungo vyao kuanzia siku moja, miezi sita, hadi mwaka mmoja na mkoani humo wameachiwa wafungwa 74, wakiume 62 na wanawake 12.

Nao baadhi ya wafungwa akiwamo Bakari Juma, mkazi wa Shinyanga, wamemshukuru Rais Magufuli kwa kutoa msamaha huo, huku wamkimuahidi Mkuu wa mkoa kutokwenda kufanya uhalifu tena kwa kuwa wameshajifunza kilimo bora wakiwa magereza na wataenda kuendelea ujuzi huo.

**Lindi nayo yatekeleza agizo**

Serikali mkoani Lindi, imetekeleza agizo la rais la kuwaachia huru wafungwa 129 kati ya 305 waliokuwa wakikabiliwa na makosa mbalimbali yakiwamo ya kukutwa na silaha kinyume cha sheria.

Kwa mujibu wa taarifa iliyowasilishwa kwa Mkuu wa Mkoa huo, Godfrey Zambi na Mkuu wa gereza mkoani humo, ACP Josephine Semwenda, wafungwa hao wakiwamo wanne raia wa Ethiopia, walikuwa wamefungwa katika magereza sita Mkoa wa Lindi.

Taarifa ya Mkuu wa Magereza mkoani Lindi, Semwenda na kusomwa na Mwanasheria Mkaguzi Msaidizi, Edgar Mombo, ilisema wafungwa walioachiwa, wanne ni raia wa Ethiopia.

Semwenda alisema gereza kuu la mkoa limewaachia wafungwa 34, Ruangwa (29), Kilwa (24), Nachingwea (20), Kingurungundwa (13) na Liwale (9).

"Wafungwa wanaoachiwa leo wote ni wanaume," alisema ACP Semwenda.

Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Zambi akizungumza na baadhi ya wafungwa walioachiwa huru, aliwataka wawe raia wema na kujiepusha kufanya mambo maovu yaliyowafanya wafikishwe gerezani.

Pia aliwataka waliopata ujuzi kuutumia kujitafutia riziki halali, kwa kushirikiana na jamii pamoja na familia zao, kwa kuwa Rais amefanya jambo kubwa la kuwaachia huru kwa sababu anachukia kuongoza taifa lenye wafungwa wengi.

Aliuagiza uongozi wa Idara ya Uhamiaji kuharakisha taratibu kwa wafungwa wanne waliotoka Ethiopia kurejeshwa nchini kwao.

Wakizungumza kwa niaba ya wafungwa wenzao, Juma Lauko kutoka Mkoa wa Kigoma na Mohamedi Ndalimu kutokea Kata ya Kitunda, Manispaa ya Lindi, wamemshukuru Rais kwa uamuzi wa kuwaachia huru baadhi ya wafungwa na kuahidi kuwa raia wema wanaporejea nyumbani kwao.

**Wafungwa 79 Mwanza huru**

Wafungwa 79 waliokuwa katika Gereza Kuu la Butimba mkoani Mwanza wameachiwa huru wakiwa miongoni mwa wafungwa 190 wa magereza yote ya mkoa huo watakaonufaika na msamaha huo.

Wakitoka ndani ya gereza hilo asubuhi ya jana, wafungwa pamoja na mahabusu walioachiwa huru akiwamo Timotheo Kaume, William Ngoso na Michael Elias, wamemshukuru rais huku wakiwaomba wananchi wenzao kuwapokea vyema kwani wamerekebika.

Akizungumza kutoka katika gereza hilo Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, alisema jambo lililofanywa na rais la kuwaachia huru ni sehemu ya ahadi yake ya kuwagusa wananchi wanyonge na maskini huku akiwasisitiza wakawe raia wema ikiwa ni pamoja na kuchapa kazi ili kujiletea maendeleo yao binafsi na taifa kwa ujumla.

Kwa upande wake Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza nchini, Faustine Kasike, aliwataka wafungwa hao wakatumie vizuri ujuzi walioupata gerezani ili kujipatia riziki zao kihalali

***Imeandikwa na Nebart Msokwa (Mbeya), Marco Maduhu (Shinyanga), Said Hamdani (Lindi) na Neema Emmanuel, Mwanza**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**


NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0782253676


## PASSPORT IMEPOTEA



**DEUSDEDIT LUCAS MCHOMBA** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba TAE167458 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu Dar es salaam 2019.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi:
**KW/K/B.I/I/VOL.VIII/148.**


## KUPOTEA KWA CHETI



**EDNA ANTHONY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0152/0005 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia SHINYANGA SEKONDARI mwaka 2006.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi:
**KBA/CPS/A.24/29/VOL.XV/196.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**IVAN ANDSON** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne kilichotolewa mwaka 2007, Isuto Secondary School Chenye Index No.S 1467/0021/2007.Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu au apige simu namba 0755555534.

**Taarifa ya polisi MB/RB/9082/2012.**

215550102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;238/2019
Ombi la THERESIA REVOCATUS MGAWE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu REVOCATUS NICHOLAUS MGAWE.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/12/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 22/11/2019.

115550902


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo: **DODOMA MJINI**

Usimamizi wa Mirathi No. 88/2019
Ombi la **ATHUMAN HUSSEIN** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya Marehemu **HUSSEIN HASAN MLELWA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 19/12/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa.

Tarehe 02/12/2019

115545901

## EMMANUEL KOYANO BUNZALI

**Wanyasubi Kahama,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.778 CFL aina ya CHEVROLET.

Yeyote atakaiona atoe taarifa katika kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

Taarifa ya Polisi.

**KAH/RB/TR/866/20**

215550002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA: 309....2019**
**Mdai: OSWARD MOSES ICHWEKELEZA**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: VENANT BAKENYA (2) ALMACHUS MWEMEZA**

Kwa:
ALMACHUS MWEMEZA
WA BUKOBA

Ombi la Mdai:
OSWARD MOSES ICHWEKELEZA
Madai ya: PESA ZA UKARABATI WA HOSPITAL TSH. 14,970,000/=

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 18 mwezi 12 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 06 mwezi 12 mwaka 2019.

115551002

## KUPOTEA KWA KADI

**GRACE CATHERINE RUTAHAKANA** anatangaza kupotea kwa kadi yenye namba ya usajili T137 BCM aina ya TOYOTA RAV4 iliyotolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
DB/RB/10226/019

115550702


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# FIFA yaifuata WADA kufungiwa kwa Urusi

**GENEVA,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (Fifa), limefanya mawasiliano na Wakala wa Kupambana na Dawa za Kusisimua Misuli michezoni (WADA), kupata meelezo zaidi juu ya kufungiwa kwa Urusi kwenye michezo mikubwa ya kimataifa.

Jumatatu Kamati ya Utendaji ya WADA ilitoa adhabu kwa Urusi kufungiwa kwa miaka minne.

Kufungiwa huko kuna maana kwamba, Urusi haitapeperusha bendera wala wimbo wao wa taifa kwenye michuano ya Olimpiki ya mwaka 2020 na michuano ya soka ya Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar.

Ingawa WADA haliitambui Shirikisho la Soka la Ulaya (Uefa), kama msimamizi wa mashindano makubwa, hivyo Urusi itaweza kushiriki kwenye michuano ya Euro 2020.

Hata hivyo, Shrikisho la Soka la Urusi, limesema kwamba lina matumaini adhabu hiyo haitahusu kwa upande wa soka na hivyo wanasubiri kauli ya Fifa.

Fifa bado haijatoa tamko lake kuhusu kufunguwa huko, lakini imethibitisha kwamba imefanya mawasiliano na WADA.

"Fifa imechukua uamuzi wa kuwasiliana na Kamati ya Utendaji ya WADA," alisema msemaji wa Fifa.



# Haaland: Sibabaishwi na uvumi wa usajili

**VIENNA,** Austria

ERLING Haaland hana tatizo na uvumi unaoenea juu yake ambao umekuwa wa kasi hasa baada ya kuonyesha kiwango kizuri cha kufunga mabao.

Mshambuliaji huyo kijana wa Salzburg anafurahia kipindi chake kizuri na klabu hiyo kwa kufunga mabao nane katika mechi tano alizocheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku akifunga mabao 16 kweye mechi 14 za Ligi Kuu ya Austria, Bundesliga.

Kama Haaland jana usiku alifunga dhidi ya Liverpool kwenye mchezo wa mwisho wa Kundi E, utamfanya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga katika mechi zote sita za makundi za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Manchester United, inayonolewa na kocha wa zamani wa Haaland wakiwa pale Molde, Ole Gunnar Solskjaer – imekuwa ikihusishwa zaidi na kuwania saini ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, wakati Borussia Dortmund, Juventus, Real Madrid, Barcelona na Liverpool pia zimekuwa zikihusishwa na kuwania saini yake.

Hata hivyo, Haaland amesema hasumbuliwi na uvumi huo.

"Mimi akili yangu ipo kwenye kazi yangu ya kucheza soka na kufurahia kile ninachokifanya kila siku, sifikirii kitu kingine chochote zaidi ya kufurahia kucheza soka kwa sasa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Hayo ndio malengo yangu kwa sasa, kuhakikisa naisaidia klabu yangu ya Salzburg kufantya vizuri na kufurahia soka."



# Solskjaer atolewa hofu kwa Pochettino United

**MANCHESTER,** England

MABOSI wa Manchester United wamemhakikishia Ole Gunnar Solskjaer kibarua chake kipo salama na hawana mpango wa kumchukua Mauricio Pochettino.

Kauli hiyo ya Manchester United inatokana na kikao baina ya Joel Glazer na kocha Solskjaer huku akihakikishiwa kupewa fedha za usajili wa kiungo wa Atletico, Saul Niguez.

Manchester United imechukua uamuzi huo baada ya ushindi dhidi ya Tottenham na Manchester City na kuwapandisha hadi nafasi ya tano katika msimamo wa Ligi Kuu England na kufufua matumaini yao ya kupata nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa.

Jina la Pochettino lilikuwa likitajwa karibu kila dakika na kuhusishwa moja kwa moja na kibarua cha kwenda kuinoa Man United.

Lakini sasa kocha huyo wa zamani wa Tottenham itabidi atafute kazi tu kwingineko, Old Trafford hakuna nafasi kabisa kwa siku za karibuni.

Katika mechi tatu baada ya Pochettino kufutwa kazi huko Spurs, Man United walikuwa kwenye hali mbaya, hawakuwa wameshinda yoyote, tena wakicheza na timu mbili zilizopanda daraja kwenye Ligi Kuu England pamoja na klabu ndogo ya huko Kazhakhstan, Astana.



# Ancelotti: Sihofii kutimuliwa Napoli

**MILAN,** Italia

CARLO Ancelotti amesema yeye "hahofii" kufukuzwa kama kocha wa Napoli wakati uvumi ukidai kwamba Gennaro Gattuso anahusishwa na mpango wa kuchukua nafasi hiyo.

Napoli ipo kwenye wakati mgumu baada ya kucheza mechi tisa bila ushindi tangu ilipomfunga Salzburg Oktoba 23, huku akitoka sare mechi zake saba.

Ripoti nchini Italia zinaeleza kwamba, kocha wa zamani wa AC Milan, Gattuso – ambaye alicheza chini ya Ancelotti pale Rossoneri, anaweza kuteuliwa mapema wiki hii, huku mabosi wa Napoli wakiwa wanaonyesha kuishiwa uvumilivu wa kutopata matokeo mazuri.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 60, alikubali maswali wakati alipoulizwa kuwa anaweza kufukuzwa na akasema yupo tayari kwa hilo.

"Kocha wakati wowote yupo tayari, huwezi kupaniki kwa hilo," alisema akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wake wa jana Jumanne wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Genk.

"Nafikiri kwa kocha ni suala la kawaida kuulizwa swali la kufukuzwa, hivyo mimi nimejiandaa kwa hilo.

"Sina hofu na wala siwezi kuwa na hofu, kwa sababu kocha ukishateuliwa, wakati wowote unaweza kufukuzwa na hilo lipo wazi kabisa."

# Ljungberg aeleza kilichoibeba Arsenal

**LONDON,** England

FREDDIE Ljungberg amebainisha kwamba imani ndio nguzo kuu ya kuiwezesha Arsenal kumaliza ukame wa kutoshinda mechi saba na kupata ushindi wa 3-1 dhidi ya West Ham juzi, Jumatatu.

Huku Ljungberg akiwa ameanza kuiongoza timu hiyo kwa kutoka sare na Norwich City nyumbani na kufuatiwa na kipigo kutoka kwa Brighton and Hove Albion tangu achukue mikoba ya kuinoa klabu hiyo kutoka kwa Unai Emery, juzi alipata ushindi wa kwanza.

Katika mchezo huo Arsenal walianza kufungwa kwa bao la Angelo Ogbonna dakika ya 38, kabla ya Gabriel Martinelli kusawazisha na Nicolas Pepe akafunga la pili na Pierre-Emerick Aubameyang akatupia la tatu.

Ushindi huo umeifanya Arsenal kujivuta hadi nafasi ya tisa katika msimamo, ikipitwa pointi saba kwenye nne bora.

Baada ya mchezo huo, Ljungberg aliiambia Sky Sports: "Ina maana kubwa kwa wachezaji. Wamekuwa wakiishi kwenye presha kubwa na uliona kwenye kiwango chao.

"Niliona West Ham walionekana kuchoka na pasi za wachezaji walionekana kucheza kwa kujiamini.

"Vijana hawakuwa na tatizo, walionekana kucheza kwa kujiamini na kwa kiasi kikubwa imani ndio ilikuwa nguzo kubwa ya kuhakikisha tunashinda mchezo wa leo (juzi)."



# Barca: Hakuna mrithi wa Messi



**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA haitaweza kupata mrithi wa Lionel Messi, kwa mujibu wa Rais wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu, ambaye ameongeza kuwa Pep Guardiola anakaribishwa wakati wowote kurudi pale Camp Nou.

Messi baada ya kushinda kwa mara ya sita tuzo ya Ballon d'Or aliweka rekodi nyingine ya kufunga hat-trick 35 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, wakati Barca wakiibuka na ushindi wa 5-2 dhidi ya Real Mallorca Jumamosi.

Licha ya kutumia fedha nyingi kuwasajili, Antoine Griezmann na Frenkie de Jong wakati wa dirisha la majira ya joto, Barca bado wanamtegemea mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ambaye amefunga mabao 14 katika mechi 15 kwenye mashindano yote msimu huu.

Bartomeua amebainisha kwamba, itakuwa vigumu kwa Barca kupata mrithi wa Messi wakati mshambuliaji huyo atakapoamua kuondoka kwenye klabu hiyo, lakini akaeleza mpango wa kuendelea kuimarisha wachezaji vijana kutoka kwenye akademi yao ya La Masia.

"Sisi mashabiki wa Barca tuna bahati kubwa kwa kufurahia siku za Messi," alisema Bartomeu, ambaye anataka kumpa Messi "mkataba wa maisha" akiliambia gazeti la Italia la La Repubblica.

"Leo ni vigumu kumpata mrithi wake na wakati ambao hatakuwapo hapa, tutalazimika kucheza kwa tofauti kubwa.

"Siwezi kusema kwamba tayari tumejiandaa kwa kuondoka kwa Messi, lakini ni ukweli kwamba tayari tumeandaa wchezaji vijana ili kuwatumia kwa muda mrefu."

Bartomeu pia alithibitisha kwamba, Guardiola – ambaye aliondoka Barca mwaka 2012 baada ya misimu minne kabla ya kwenda Bayern Munich na sasa Manchester City, mara zote atakaribishwa nyumbani Barca.

"Uwezekano wa kurudi Guardiola? Hakunitegemei mimi," aliongeza.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BARCA: VIDAL SAHAU KUONDOKA JANUARI

●●● Tunakikosi chenye uwiano, hatuna upungufu wowote, lakini pia hatuwezi kumudu kumpoteza...

**BARCELONA,** Hispania

Barcelona "haiwezi kumudu" kumruhusu kiungo ambaye hajazoea maisha ya hapo Camp Nou, Arturo Vidal kuondoka katika dirisha la Januari, kwa mujibu wa Rais wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu.

Vidal ameanza mechi nne tu za Barca kati ya 20 msimu huu na mwezi uliopita alipaza sauti yake akitaka kuachana na mabingwa hao wa Hispania mwaka ujao kama haitaweza "kumuona muhimu".

Kocha wa Barca, Ernesto Valverde amefungua mlango kwa nyota huyo wa kimataifa wa Chile kutafuta timu mpya, na Mkurugenzi Mtendaji wa Inter, Giuseppe Marotta hivi karibuni alifunguka kikosi chake kuvutiwa na kiungo huyo.

Hata hivyo, Bartomeu anatarajia Vidal - aliyeripotiwa kujiunga na klabu hiyo kwa euro milioni 18 akitokea Bayern Munich Agosti mwaka jana, kumuona akibaki Camp Nou angalau hadi mwishoni mwa msimu.

**"Hakuna harakati zi nazotarajiwa Januari," aliliambia Gazeti la La Repubblica. "Tunakikosi chenye uwiano, hatuna upungufu wowote, lakini pia hatuwezi kumudu kumpoteza yeyote.**

"Mara kadhaa kabla ya mchezaji kuonyesha utashi wa kuondoka, lakini kamwe si Januari. Katika hali nyingine tumekuwa tukiwaacha waondoke, katika mazingira mengine tumekuwa tukiwashawishi kubaki."

Barcelona jana usiku ilikuwa na kibarua kigumu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Inter wakati tayari ikiongoza Kundi F huku ikiwa na tiketi mkono ya kutinga hatua ya 16-Bora, wakati miamba hao wa Italia wakishuka dimbani wakiwa na lengo la kuishika Borussia Dortmund ambayo nayo jana ilivaana na Slavia Prague.

Lautaro Martinez ambaye amekuwa kwenye kiwango bora msimu huu kwa miamba hao wa Serie A, Inter, amekuwa akihusishwa kuwapo katika rada za Barca, lakini Bartomeu hakutaka kutoa maoni yake kuhusu tetesi hizo.

"Hili ni swali la mtego," alisema. "Ninachoweza kukisema ni kwamba Inter inacheza vizuri sana na si mchezaji huyo pekee ambaye amenivutia mimi. Siyo bahati mbaya kwamba Inter ipo kileleni mwa Serie A."

## KWA UFUPI

### MCTOMINAY KUFUNGWA UNITED
Manchester United inapaga kumpa mkataba mpya kiungo wao Mscotland, Scott McTominay, 23, ambao utakuwa ukimfanya kulipwa pauni 60,000 kwa wiki. (Sun)

### BENITEZ AKATAA KUREJEA EPL
KOCHA wa Dalian Yifang, Rafael Benitez ametupilia mbali yeye binafsi suala la kurudi Ligi Kuu England kwa muda huu. (Sky Sports)

### EVERTON YAMFUATA EMERY
Everton imebisha hodi kwa kocha aliyetimuliwa Arsenal, Unai Emery ikimtaka kwenda kuinoa miamba hiyo ya Goodison Park. (Sky Sports)

### ERIKSEN AIPASUA KICHWA UTD
Manchester United bado imebaki na lengo lake la muda mrefu la kumsajili kiungo wa Tottenham Hotspur, Christian Eriksen, 27, katika dirisha la Januari, lakini inakabiliwa na ushindani wa kumpata Mdenmark huyo. (90min)

### BARCA YAMKARIBISHA GUARDIOLA
RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amesema mlango siku zote upo wazi kwa kocha wa Manchester City, Pep Guardiola kuamua kurudi kuinoa klabu yake hiyo ya zamani. (La Repubblica, via Goal)

### SOLSKJAER ATOLEWA HOFU UTD
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amekuwa akielezwa kuwa kibarua chake kipo salama na wamiliki wa klabu hiyo na kwamba hawatamuajiri kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino. (Mail)

### ARSENAL, INTER KWA SMALLING
Arsenal inakabiliwa na ushindani kutoka Inter Milan na Juventus kwa beki wa Manchester United, Chris Smalling, 30, anayeichezea kwa mkopo Roma. (Mirror)

### LAMPARD AJIULIZA SOKO LA JANUARI
KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard ana hofu kuhusu kutumia fedha nyingi sokoni katika dirisha la Januari baada ya 'Blues' kufutiwa kifungo cha usajili. (Evening Standard)

### BESIKTAS YAMKANA TOSUN
RAIS wa Besiktas, Ahmet Nur Cebi ametupilia mbali uwezekano wa kwenda kumsajili mshambuliaji wa Everton na Uturuki, Cenk Tosun, 28. (Hayatta Besiktas Radio station, via Liverpool Echo)

### HAALAND APOTEZEA TETESI USAJILI
MSHAMBULIAJI wa Red Bull Salzburg na Norwey, Erling Braut Haaland, 19, amesema hapati wakati mgumu wa kushugulikia tetesi za usajili zinazomzunguka. (Goal)

### ARSENAL KUMCHUNIA NKETIAH
Arsenal haitakatisha mkataba wa mkopo wa muda mrefu wa Eddie Nketiah pale Leeds licha ya mshambuliaji huyo Muingereza kutoanza mechi hata moja ya Championship tangu alipotua hapo Elland Road. (Sun)

### NEWCASTLE, BOURNEMOUTH VITANI
Newcastle na Bournemouth zinamfuatilia mshambuliaji wa Hull City, Muingereza Jarrod Bowen, 22. (90min)

HABARI MICHEZO

# MRITHI WA AUSSEMS SOKONI NA MIL.70/- AKITANGAZWA LEO

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI uongozi wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, leo ukitarajia kumtangaza rasmi kocha mkuu atakayerithi mikoba ya Mbelgiji Patrick Aussems, imeelezwa kuwa tayari kitita cha Sh. milioni 76 kuelekea usajili wa dirisha dogo kimetengwa kwa ajili ya kufanya fujo zisizo na madhara sokoni.

Shirikisho la Soka nchini (TFF), linatarajia kufungua usajili wa dirisha dogo kuanzia Jumatatu ijayo Desemba 16 hadi Januari 15, mwakani na tayari tetesi za usajili hususan kwa klabu za Ligi Kuu zimeanza kuvuma kila kona nchini.

Hata hivyo, akisoma mapato na matumizi ya klabu hiyo katika mkutano mkuu wa Simba uliofanyika wiki iliyopita kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, Mhasibu wa klabu hiyo, Mathiew Asunga, alithibitisha kutengwa kwa kiasi cha Sh. milioni 76 za kukiimarisha kikosi hicho kipindi hiki cha dirisha dogo.

Na wakati uongozi huo umetangaza rasmi kuwa leo utamtangaza kocha mkuu, imeelezwa anatarajiwa kutoa mapendekezo makubwa ya usajili baada ya kukisoma kichwa hicho kinachoongoza msimamo wa Ligi Kuu kwa sasa.

Kwa mujibu wa tetesi zilizozagaa mitandaoni, kocha anayepewa nafasi kubwa kutangazwa kubeba mikoba ya Aussems ni Mzambia, Beston Chambeshi aliyekuwa akiinoa Nkana FC ya Zambia, ambaye tayari inadaiwa ameshavunja mkataba na klabu hiyo.

Aidha, imeelezwa kuwa tayari kamati maalum ya ufundi ndani ya klabu ya Simba imeundwa kwa ajili ya kukisoma kikosi hicho na kuangalia wachezaji wanaoweza kukiimarisha kabla ya kocha mkuu kutoa mapendekezo yake.

"Tayari kamati maalum ya ufundi imeundwa na kupitia ripoti zote za kila mechi Simba ilizocheza kabla ya kuelekea sokoni kutafuta wachezaji wa kuiimarisha timu," kilieleza chanzo chetu.

SHEREHEKEA...



Mchezaji wa Kiyombo Veteran, Moshi Malula (kulia), akimiliki mpira dhidi ya mchezaji wa Kitunda Veteran, wakati wa mchezo wa kirafiki uliopigwa katika Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda kusherehekea miaka 13 ya Kitunda Veteran na miaka 58 ya Uhuru wa Tanzania Bara iliyoadhimishwa jana na timu hizo kutoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Shime ataka burudani na ushindi wakiivaa Burundi leo

**Na Somoe Ng'itu,** JINJA

KOCHA Mkuu wa timu ya soka ya Taifa ya Tanzania Bara ya Wasichana ya umri chini ya miaka 17, Bakari Shime, amesema anahitaji kuona wachezaji wake wanaonyesha kiwango kizuri katika mchezo wa Kombe la Chalenji dhidi ya wenzao kutoka Burundi utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Njeru mjini hapa.

Yosso hao wa Tanzania Bara watashuka uwanjani leo kuanzia saa 7:30 mchana wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 5-0 walioupata dhidi ya Eritrea wakati Burundi ilichapwa 4-0 na wenyeji Uganda, kwenye michuano ya Chalenji inayoendelea nchini hapa.

Akizungumza na Nipashe mjini hapa jana, Shime, alisema hataki kuona kikosi chake kinapata ushindi tu, bali pia wachezaji wanacheza katika kiwango kilichozoeleka na hii ndio itamsaidia kuona kiufundi, mahali wanapoelekea.

Shime alisema anahitaji kuona wanaingia katika mchezo wa leo wakiwa imara zaidi, lakini pia wakicheza kwa tahadhari kwa sababu wapinzani wao Burundi pia wana kikosi chenye wachezaji wazuri.

Alisema anafahamu kila timu imekuja kushindana, lakini ni vizuri wakaangalia malengo ya kuwaendeleza wachezaji chipukizi wasichana kwa kutoa nafasi kwa kila mmoja kucheza.

"Tumefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo wetu dhidi ya Burundi, kikosi kiko katika hali nzuri, isipokuwa mchezaji mmoja, Emiliana Mduma, ambaye amepata majeraha kidogo, tuliwaona Burundi na wao wametuona, walifungwa mechi ya kwanza, sisi tulishinda ila hakutucheza katika kiwango chetu kilichozoeleka, tumelifanyia kazi, hivyo kesho tunatarajia kuwa na mechi nzuri," alisema Shime.

Naye Kocha Mkuu wa timu ya Burundi, Daniella Niyibimenya, alisema anatarajia mechi ya leo itakuwa nzuri, tofauti na mchezo wao wa kwanza ambao walipoteza dhidi ya Uganda.

"Sisi tulifika hapa saa tisa usiku, na kuamkia mechi, wachezaji walichoka, naamini kesho (leo), tutaonyesha mchezo mzuri, wasichana wamepumzika kidogo," alisema kocha huyo.

Mechi nyingine za mashindano haya yanayofanyika chini ya usimamizi wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), ni kati ya Kenya dhidi ya Eritrea wakati Uganda watawakaribisha Djibouti.

# Mwadui yavizia wanaotemwa

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA usajili wa dirisha dogo kufunguliwa Jumatatu ijayo, uongozi wa timu ya Mwadui FC umesema hautakurupuka kufanya kusajili na badala yake wataufanya kwa utulivu wa hali ya juu.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Khaleed Adam, alisema watafanya usajili wakiwa wametuliza akili ili aweze kupata wachezaji wazuri.

Alisema anatarajia kuongeza wachezaji sita kwa ajili ya kuleta ushindani kwenye timu yake na kusema, amelenga kupata nyota watakaotemwa kutoka klabu kubwa.

Kocha huyo idara anayotajia kuiboresha zaidi ni ile ya ushambuliaji pamoja beki ya kati.

"Kila safu nitaongeza wachezaji wawili idadi ya wachezaji nitakaowaacha nitawatangaza pindi usajili utakapoanza," alisema.

Aliwataka wachezaji wake kuongeza juhudi wanapokuwa mazoezini pamoja kufuata maelekezo anayowapa kwa makini ili kuweza kulinda nafasi zao.

"Naomba wachezaji waongeze nidhamu pamoja na umakini hilo litawasaidia wao kufanya vizuri zaidi," alisema.

# Joyce asahau hat-trick ataka kombe Cecafa

**Na Mwandishi Wetu, JINJA**

MSHAMBULIAJI tegemeo wa timu ya wasichana wa umri chini ya miaka 17 ya Tanzania Bara inayoshiriki mashindano ya Kombe la Chalenji, Joyce Charles, amesema mabao matatu aliyofunga katika mchezo wa kwanza dhidi ya Eritrea yamemwongezea nguvu zaidi ya kupambana katika mechi inayofuata lakini anachowaza ni kombe na si kingine.

Joyce alifunga hat-trick ya kwanza kwa timu yake na mashindano hayo wakati Tanzania Bara ikipata ushindi wa mabao 5-0, mengine yakifungwa na Aisha Masaka.

Akizungumza na gazeti hili jana, Joyce, alisema amefurahi kuisaidia timu yake kupata ushindi katika mchezo huo wa kwanza, lakini anataka kuona wanafanya vizuri zaidi.

Mshambuliaji huyo alisema malengo yake ni kuona Tanzania Bara inarejea nyumbani na kikombe cha mashindano hayo na kila mchezaji ameahidi kupambana.

"Mashindano ni magumu, halafu timu zote zinatuangalia sisi, hii inatufanya tuongeze bidii, tutapambana kwa sababu tunataka ubingwa tu," alisema mshambuliaji huyo.

Michezo
Jumatano Desemba 11, 2019
Nipashe

## Barca: Vidal sahau kuondoka Januari



HABARI UK. 30

## MO achagiza Kili Stars kuiua Z'bar

**Na Somoe Ng'itu, KAMPALA**

AHADI iliyotolewa na mfanyabiashara maarufu nchini na mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohammed "MO" Dewji, kufuatia kuahidi kuwapa jumla ya Sh. milioni 100 na boda boda moja kwa kila mchezaji wa Kilimanjaro Stars endapo watatwaa ubingwa wa Kombe la Chalenji katika michuano inayoendelea nchini hapa, imeonekana kuwa chachu ya ushindi dhidi ya ndugu zao wa Zanzibar (Zanzibar Heroes) kwenye mechi ya jana.

Kabla ya ushindi wa bao 1-0 ambao Kili Stars iliupata jana dhidi ya Zanzibar Heroes, juzi usiku, Mo aliitembelea kambi ya timu hiyo na kuwataka wachezaji kutokata tamaa kutokana na matokeo waliyopata ya kupoteza mechi ya kwanza dhidi ya mabingwa watetezi, Harambee Stars ya Kenya.

MO alisema anaamini timu hiyo ina uwezo wa kufanya vizuri na wanachotakiwa ni kupambana na kuhakikisha wanashinda mechi zilizosalia za hatua hiyo ya makundi.

"Hata timu za Ulaya huwa zinaanza vibaya katika mashindano makubwa, lakini baadaye wanaamka na kufanya vizuri, mimi siangalii mechi na Zanzibar, nawaahidi endapo mtatwaa ubingwa, nitawapatia Sh.milioni 100 na boda boda, pia tutakutana katika ile kamati ya Taifa Stars tuangalie nini tutafanya zaidi, kuwapatia zawadi nyingine," alisema MO.

Naye nahodha wa timu hiyo, Aishi Manula, alisema wanamshukuru mfanyabiashara huyo kwa kuwatembelea na kuahidi zawadi endapo watabeba kombe, lakini amewaambia Watanzania kwamba kikosi hicho kimedhamiria kufanya vema katika mechi zilizosalia.

Katika mechi hiyo ya jana iliyopigwa kwenye Uwanja wa KCCA jijini hapa, Kilimanjaro Stars ilipata bao lake pekee kupitia kwa mshambuliaji wa Polisi Tanzania, Ditram Nchimbi dakika ya 38 akiunganisha nyavuni krosi ya Eliuter Mpepo.

Mechi hiyo ilikuwa na ushindani dakika zote 90, hasa kufuatia timu hizo kufahamiana vema na kuwa na ushindani wa muda mrefu.

Hata hivyo dakika ya 35, Kilimanjaro Stars ilipoteza nafasi ya kufunga bao kupitia kwa kiungo wake, Jonas Mkude, ambaye alipiga shuti pembeni na kushindwa kuipa timu yake bao huku dakika nne baadaye Ali Ali wa Zanzibar Heroes akipiga shuti dhaifu liloishia mikononi mwa Aishi Manula.

Dakika ya 70, Miraji Athumani akiwa amebakia jirani na kipa wa Zanzibar Heroes, alipiga pembeni na kukosa bao huku dakika 80, Mwinyi Mgwali wa Zanzibar Heroes naye akiwa ndani ya 18 alishindwa kumalizia kazi nzuri iliyoanzia kwa Mudathir Yahya na hatimaye alidondoka akiwa peke yake na mpira kutoka nje.

Kwa ushindi huo, Kilimanjaro Stars imejikusanyia pointi tatu muhimu, hivyo kupanda hadi nafasi ya pili katika msimamo wa kundi hilo linaloongozwa na mabingwa watetezi, Harambee Stars walioichapa Sudan mabao 2-1 na kukata tiketi ya nusu fainali.

MILIKI...



Mfungaji wa bao pekee la Kilimanjaro Stars wakati ikishinda 1-0, Ditram Nchimbi, akimiliki mpira dhidi ya beki wa Zanzibar Heroes, Abdallah Kheri 'Sebo', katika mechi ya Kundi B ya mashindano ya Kombe la Chalenji iliyopigwa jana nchini Uganda. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# YANGA: TUMEELEMEWA MADENI, SADNEY ONDOKA

### ●●● Lamine azuiwa Simba, watangaza kusaka mwekezaji huku wakimtaja Pluijm anadai mil. 100/- ...

**Na Shufaa Lyimo**

HATIMAYE uongozi wa Klabu ya Yanga umetangaza baadhi ya wachezaji inaotarajiwa kuachana nao, jina la kwanza kwa nyota wa kigeni aliyetangazwa kutemwa akiwa ni mshambuliaji Mnamibia Sadney Urikhob, huku pia ukikiri klabu hiyo kuelemewa na madeni.

Aidha, umesema kutokana na ukata wa pesa unaoiandama klabu hiyo, sasa imeanza rasmi kutafuta mwekezaji lengo likiwa hadi ifikapo Mei mwakani awe amepatikana.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mshindo Msolla, akianza na tuhuma za kutowalipa wachezaji wao mishahara hadi baadhi kuamua kuandika barua za kuomba kuvunja mikataba, Msolla alikiri kweli klabu hiyo kutowalipa mishahara ya miezi miwili, ambapo alisema endapo mambo yatakuwa mazuri leo [jana] walitarajia kuwaingizia mishahara yao.

"Kweli hatujawalipa mishahara ya miezi miwili kwa sababu ya hali mbaya tuliyokuwa nayo, lakini leo jana) mambo yakikaa vizuri tutawaingizia mishahara yao kwa sababu ni haki yao kuwalipa," alisema.

Alisema mchezaji Sadney wameachana naye rasmi na kudai Lamine Moro, ambaye amekuwa akihusishwa na kutakiwa Simba, bado wanamtambua ni mchezaji wao kutokana na kuwa na mkataba na klabu hiyo sambamba na David Molinga.

Kwa upande wa mchakato wa kuinasua klabu hiyo kutoka katika wimbi kubwa la madeni, alisema wanalazimika kutafuta mwekezaji ili kuubadilisha mfumo wa klabu hiyo kwa ujumla.

"Mpaka Mei mwakani tunataka tuwe tumempata mwekezaji wetu ambaye naamini atabadilisha mfumo wa klabu yetu kwa sababu hali tuliyonayo kwa sasa kiuchumi si nzuri," alisema Msolla.

Kwa upande wa malalamiko kutoka kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo wanaodai klabu hiyo inapata pesa na kuzitumia vibaya, Msolla alisema si kweli na kwamba walipoingia madarakani walikutana na zigo kubwa la madeni lililoachwa na uongozi uliopita.

"Wanachama na mashabiki wetu waelewe kuwa wakati tunaingia madarakani tulikutana na madeni mengi zaidi ya bilioni mbili, tunataka tuyaandike na kuyachapishe ili umma utambue na uone tuliyoyakuta," alisema.

Alitaja miongoni mwa madeni waliyoyakuta ni la aliyewahi kuinoa timu hiyo Hans van der Pluijm ambaye anawadai Sh. milioni 100, Mzambia George Lwandamina Sh. milioni 22, huku kwa upande wa wachezaji akigoma kutaja kiasi wanachowadai lakini akiwataja wanaodai kuwa ni Donald Ngoma, Obrey Chirwa,Thabani Kamusoko, kocha Juma Mwambusi pamoja na watu binafsi, madeni ambayo wanaendelea kuyapunguza kidogo kidogo.

Alisema mapato ambayo wanayapata hayaendani na matumizi yao kwani wamekuwa wakiingiza Sh. bilioni 2.2 wakati matumizi yakiwa ni Sh. bilioni nne hali inayosababisha madeni kuongezeka kila uchao.

Aliongeza kuwa, ahadi za pesa ambazo watu waliahidi kuzitoa kwenye kilele cha "Kubwa Kuliko" mpaka sasa bado hazijakamilika.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
770856 541002 >